(b) Kwa ufasaha na ueledi atasimamia vitengo vya Inteligesia takwimu, polisi wa Kimataifa Intepol kiteengo cha madawa ya kulevya na kusafilisha mali za magendo.

Kazi na majukumu ya mkuu wa kitengo Y

Atafanya kazi chini ya mkuu wa mkurugenzi wa makosa ya Jinai na atafanya yafuatayo:

(a) Kwa ufasaha atasimamia na kuongoza upelelezi wa makosa yote yanayohusiana na makosa ya binadamu kama mauaji, makosa yanayohusiana na ngono (ubakaji) na mambo ya ushirikina

(b) Kupeleleza malalamiko yote zidi ya polisi kazi na majukumu ya mkuu wa kitengo 2

Atafanya kazi chini ya mkurugenzi wa makosa ya Jinai na atafanya yafuatayo:

(a) atafanya kwa ufasaha na kusimamia upelelezi wa makosa yote yahusuyo mali kama WIZI wa fedha, unyan'anyi wa mali na wizi

wa mifugo.

(b) Upelelezi wa makosa yote yahusuyo fedha haramu na makosa mengine makubwa ya kimataifa yahusuyo fedha haramu

Kazi na majukumu ya mkuu wa kitengo cha silaha na usajili

14 Atatekeleza majukumu ya majukumu yafuatayo:

(a) Kutunza kumbukumbu zote za usajili wa silaha zote

(b) Kusimamia usajili wa silaha Tanzania,kuandaa na kugawa orodha ya silaha hizo

(c) Usimamizi wa masuala yahusuyo silaha binafsi maghala ya silaha ya binafsi na ya serikali na silaha zilizoibiwa na zile ambazo hazina wenyewe

(d) Kuandaa taarifa za mwezi, robo mwaka na mwaka kutoa taarifa za usajili wa silaha na kuzipeleka kwa mkurugenzi wa makosa ya jinai.

(e) Atakuwa afisa mahusiano kuhusu silaha ndogondogo kwa ajili ya kuzuia uingiaji na uthibiti wake nchini.

<u>Matumizi ya kitengo cha upelelezi</u>

Kitahusika na upelelezi wa makosa yote ya Jinai yaliyoorodheshwa katika kiambatanisho ‘’C’’ pamoja na upelelezi mwingine ambao hautakuwa umependekezwa vizuri na askari wa kazi za kawaida kama kanuni kuu isemayo makosa yote madogomadogo yatapelekewa na askari wa kitengo cha kazi za kawaida isipokuwa pale itakapohitajika ifanyike na kitengo cha upelelezi

Mkuu wa polisi na mkuu wa kituo watatoa uamuzi bila kuchelewa watahakikisha Taarifa zinazotolewa kama hazita weza kupelelezwa na askari wa kawaida atazipeleka kwenye kitengo cha upelelezi au kulifunga jalada hilo.

Makosa ambayo yanatakiwa kupelelezwa akiwepo mkuu wa upelelezi wa mkoa na mkuu wa upelelezi wa wilaya.

1. Makosa yote ya madai ,ubaguzi na ya kidini

2. Makosa yote yahusuyo mambo ya kisiasa

3. Makosa yote ambayo yanataka kibali cha mashtaka kutoka kwa mwanasheria mkuu wa serikali
4. Makosa yote yanayohusisha watu muhimu kisiasa ambaye anakuwa mtuhumiwa au mshtakiwa

5. Kesi zote zinazohusu wabunge

6. Kesi zote ambazo zitaendeshwa na mahakama kuu.

7. Matukio yote ambayo yatahusisha Askari polisi kufyatua risasi au mambo ya kutoa machozi katika kutuliza ghasia /fujo

8. Makosa yote makubwa yatakayofanywa na wageni au watoto

9. Makosa yote yahusuyo wizi wa risasi na milipuko

10. Makosa yote makubwa yahusuyo askari yakihusisha kuwaokoa wahalifu kutoka polisi au magereza au sehemu

yoyote ya kuwahifadhi inayokubalika kisheria

11. Makosa makubwa ndani ya jeshi, ikiwemo kuwatorosha washtakiwa chini ya ulinzi wa polisi wafungwa au amri halali ya kufungwa
12. Makosa yote yaliyomo katika sehemu ya 5 na 6 ya polisi Order Act cap 385 RE 2002.
13. Uhujumu.
14. Makosa yote ya Jinai ambapo Askari polisianahusika
15. Makosa yote yaliyopo katika Idara Union Act, Cap 244 RE 2002
16. Kubaka
17. Kuchoma nyumba moto
18. Unyang'anyi wa kutumia nguvu
19. Makosa yote yanayoendana na maumbile
20. Kuharibu makusudi mali za serikali
21. Wizi uliokithiri wa mali ambapo wafanyakazi wa serikali wa ubalozi wanahusika
22. Makosa yote ya kugushi.
23. Kesi zote zilizopo katika sheria ya Rushwa Cap 229 RE 2002
24. Wizi wa vifurushi vya posta na wizi ndani ya posta
25. Makosa yahusuyo
26. Makosa makubwa ya uvunjaji
27. Kesi zote zilizopo katika sehemu ya 41 na 42 ya sheria ya polisi na polisi wasaidizi RE 2002
28. Kesi yoyote kubwa ambayo kwa ushauri wa mkuu wa upelelezi mkoa au mkuu wa upelelezi wilaya utahitaji uchaguzi wa kina kama itakavyoshauriwa na mkurugenzi wa makosa ya Jinai

PGO - 9

KITENGO CHA AFYA CHA POLISI.

MUUNDO, UTAWALA NA MAJUKUMU.

MUUNDO:

1. Mkuu wa kitengo cha afya Polisi atakuwa msimamizi mkuu wa kitengo cha afya.

2. Afisa msimamizi wa huduma ya afya ya Polisi (ZBR) atatoa taarifa kwa (kamanda) mkuu wa kitengo cha afya cha Polisi kupitia kwa Kamishina (ZBR) katika mambo yote yanayohusu huduma afya Polisi (ZBR).

MAJUKUMU MAKUU YA KITENGO CHA AFYA CHA POLISI.

Yafuatayo yatakuwa majukumu ya kitengo cha afya cha Polisi

a) Kutoa humuda ya afya kwa wanachama na vitengo vingine katika jeshi la Polisi na pale itakapohitajika kwa wananchi hasa inapotokea dharura.

b) Kusambaza huduma za afya vituoni na katika vitengo na kuhakikisha huduma hiyo inatumika kutokana na taratibu zilizowekwa .

c) Kupendekeza sera sahihi kwa Jeshi la Polisi kwa Inspekta Jenerali wa Polisi na kusimamia pale itakapokubalika.

d) Kuboresha utayari miongoni mwa askari dhidi ya umuhimu wa huduma za afya kama vile kuzuia na kutibu magonjwa ya kuambukiza na kuwahudumia wale ambao wameadhirika na

magonjwa hayo.

e) Kuhifadhi kumbukumbu na takwimu za afya kwa ajili ya askari.

f) Kushiriki katika shughuli zinazohusu utatuzi wa majanga na oparesheni za uokoaji na

g) Kushirikiana na vyombo vingine vya afya Wizara ya afya na shirika la afya ulimwenguni kufanya utafiti na maendeleo katika sekta ya afya.

UTAWALA:

4 (a) Kitengo cha afya cha Polisi kimegawanywa katika sehemu kuu chini ya kitengo cha afya makao makuu.

i. Kitengo cha afya cha mkoa kwa Tanzania bara na

ii. Kitengo cha afya cha Polisi(ZBR-PHQ)

iii. Hospitali ya polisi ya kilwa Road

(b) Muundo wa utawara katika kitengo cha afya umeonyesha katika (Appendix A) kielelezo A.

5. Inspekta Jenerali wa Polisi atachagua idadi ya Maafisa ambao watasaidia kitengo cha utawala

kutokana na mahitaji.

KIELELEZO ”A”

(PGO NO .9)

MUUNDO WA AFYA

MKUU WA KITENGO CHA AFYA

UTAWALA KITENGO CHA AFYA

MKUU WA KITENGO CHA AFYA (ZBR).

MKUU WA KITENGO CHA AFYA CHA MKOA.

PGO - 10

KIKOSI CHA KUTULIZA GHASIA

MUUNDO NA KAZI ZAKE

1. Kikosi cha kutuliza ghaasia ni tawi la jeshi ambacho kimepewa mafunzo maalumu yakushughulika na dharura na kufanya operasheni kwa kusaidiana na polisi wa kazi za kawaida.

2. (a). Kikosi cha kutuliza ghasia kinaundwa na afisa mmoja,(afisa aliyetangazwa kwenye gazeti la serikali), Mkaguzi wa polisi mmoja,staff sajini mmoja, na askari 60 wa vyeo mbalimbali pamoja na madereva na askari wa simu na mawasiliano. Kikosi kimegawnyika kama ifuatavyo;

MAHALI	IDADI YA VIKUNDI
Dar es Salaam	12
Unguja Mjini Magharibi	4
Kusini Unguja	1
Kaskazini Pemba	2
Kusini Pemba	2
Arusha	3
Dodoma	3
Singida	2
Sumbawanga	2
Bukoba	3
Songea	2
Mtwara	2
Morogoro	3
Tanga	2
Mbeya	2
Kigoma	3

Iringa	2
Tabora	2
Lindi	1
Moshi	2
Mwanza	4
Musoma	4
Manyara	2
Shinyanga	2
Pwani	1

(b). Kikosi cha kutuliza ghasia ukonga, pia kitaweka kikosi cha akiba kama itahitajika kufanya hivyo.

3.makao makuu ya kikosi cha kutuliza ghasia yapo makao makuu ya polisi. Watahiniwa wote kwa ajili ya kufanya kazi za kuzuia ghasia watapata mafunzo katika chuo cha mafunzo ya polisi moshi, kabla ya kupelekwa kwenye matawi mikoani

4. Kikosi cha kutuliza ghasia kipo chini ya usimamizi na utawala wa kamanda mkuu wa kikosi cha kutuliza ghasia Tanzania ambaye anawajibika kwa Inspekta Jenerali Wa Polisi.

(a) usimamizi na utawala wa kikosi cha kutuliza ghasia

(b) kutoa na kutekeleza programu ya mafunzo maalumu na kutilia mkazo yale mahitaji ya kikosi cha kutuliza ghasia. Mfano, gwaride la kuzuia fujo na ghasia na mafunzo ya kivita.

(c) suala la kanuni kamili za utendaji zinazohusu kikosi chote na kazi za kila siku.

(d) Mambo yote ya uhamisho kama inavyoelezwa katika kanuni ya utendaji ya polisi No.59, aya ya 5(e).

5. Vikosi vya mikoani vipo chini ya usimamizi kamili wa makamanda wa polisi wa mikoa ambao pia wanawajibika moja kwa moja kwa ufanisi na

nidhamu nzuri ya kikosi kinachotoa huduma chini yake.

6. Mawasiliano yote kati ya kamanda wa kikosi taifa na kamanda wa kikosi wa mkoa yapitishwe na kamanda wa polisi mkoa na anawajibika kumjulisha kamanda wa kikosi cha kutuliza ghasia Tanzania masuala yote yanayohusu kikosi.

7. Makamanda wa polisi wa mikoa watatumia kikosi cha kutuliza ghasia kusaidia askari wa kazi za kawaida kufanya doria za umbali mrefu, misako ya watu wenye tabia mbaya na aina mbalimbali za operasheni zinazofaa kwa kazi za kikosi cha kutuliza ghasia.

8. Asilimia 25 ya kikosi mara zote kibakie kambini kama akiba kwa ajili ya kukabiliana na dharura. Kamanda wa polisi mkoa anawajibika kuhakikisha idadi ya askari wa akiba inaongezeka sambamba na hali ya usalama ilivyo katika mikoa yao ya kazi. Wakati huo huo askari wa kikosi cha kutuliza ghasia wasiwekwe kambini bila sababu ya msingi wakifanya mafunzo muda wote.

9. Kikosi cha kutuliza ghasia kitafanya kazi moja kwa moja chini ya utawala wa afisa wao, ambaye atawajibika kupokea;

(a) Amri zote zitolewazo na kamanda wa polisi wa mkoa au au anayekaimu mamlaka ya kamanda wa mkoa.

(b) Amri za afisa wa ngazi ya juu aliyepo ilimradi amri hizo ziendane na maelekezo yaliyokwishatolewa na kamanda wa polisi wa mkoa.

10. Askari wa kikosi cha kutuliza ghasia wasiazimwe kwa kazi za malindo au kazi za askari wa kawaida za kila siku, lakini waweza kutumiwa kufanya kazi mahsusi hii ni pamoja na kufanya doria mtaani kama askari wa cheo cha konstebo hawatoshi wakiwa chini ya afisa wao.

11 Kipindi cha kawaida cha kufanya kazi katika kikosi cha kutuliza ghasia ni miaka mitatu kwa askari wa vyeo mbalimbali. Isipokuwa kipindi chaweza kuongezwa au kupunguzwa na Inspekta Jenerali Wa Polisi kulingana na anavyoona inafaa.

12. Askari wa vyeo mbalimbali kwa kawaida hawataruhusiwa kufanya kazi katika kikosi cha kutuliza ghasia kwa kipindi cha kwanza cha mkataba. Lakini sheria hii yaweza kulegezwa muda hadi muda kutegemea na maelekezo ya Inspekta Jenerali Wa Polisi.

PGO - 11

DIVISHENI YA POLISI RELI

MUUNDO NA MAJUKUMU

1. Divisheni ya Polisi reeli Tanzania kwa mujibu wa amri hii itajumuisha mashirika yote mawili ya reli hapa nchini, Shirika la Reli Tanzania na TAZARA.

2. KOMANDI: Makamanda wa divisheni ya reli kwa desturi watahusika na majukumu ya reli katika eneo la Dar es salaam, japo wakati mwingine kwa maelekezo ya Makao Makuu ya Polisi wanaweza kutakiwa kuongeza nguvu za kiutendaji kwa kamanda wa mkoa husika hasa wakati wa dharura.

3. Makamanda wa mikoa watawajibika na reli katika maeneo yao, isipokuwa katika majukumu ya kiutendaji ambayo yatabakia kuwa majukumu ya kamanda wa divisheni ya reli:

    a) Kazi za kisera za Polisi reli.

    b) Mpango wa kazi, likizo na uhamisho katika maeneo ya reli.

    c) Upelelezi wa kesi na matukio katika maeneo ya reli.

4. (a) Kamanda wa mkoa na Mkuu wake wa Polisi wa wilaya wwtawajibika na mwenendo wa askari wa kikosi cha reli, kazi, nidhamu na kuhusika moja kwa moja na utawala juu ya askari wa reli wanaofanya kazi katika maeneo yao. Watawasimamia kuhakikisha kwamba wanafanya kazi ipasavyo na kuwaendeleza usalama kwa kuzingatia matakwa ya utawala wa reli husika. Ukaguzi wa kikosi cha reli utafanyika kama ilivyoamrishwa katika PGO namaba 47. Mkuu wa Polisi wa wilaya atahusika na malipo na shughuli zote za uhasibu na kuwahusisha moja kwa moja askari wa reli katika huduma nyingine zainazo husu jamii ya kipolisi katika wilaya hiyo.

    (b) Makamanda wa divisheni ya reli watatoa taarifa mara kwa mara kwa makamanda wa mikoa na wilaya katika maeneo ya reli juu ya

taarifa zinazohusu divisheni ya reli na askari wa reli walio chini yao.

KAZI NA MAJUKUMU

5. Kazi na majukumu ya Polisi reli ni kama ifuatavyo:

    a) Uslama na ulinzi wa mali za mashirika yote awili (TRC na TAZARA), na upelelezi wa makosa yaliyoripptiwa ndani ya majukumu ya mashirika haya.(Kumbuka: Majukumu ya kipolisi katika makazi ya TRC na TAZARA yataripotiwa na kushughulikiwa na mkuu wa polisi wa wilaya husika.)

    b) Kusimamia sheria na amri ndani ya garimoshi na vituo vyake.

    c) Kusindikiza pesa za TRC na TAZARA, na milipuko (silaha) zinaposafirishwa kwa reli au njia nyingine ya barabara, na

    d) Doria za usala kwa ajili ya abiria mizigo na vitu vingine vinavyoweza kusafirishwa kwa reli.

MUUNDO WA POLISI RELI

6. (a) Muundo wa TRC umegawanywa katika makundi yaliyokusudia udhibiti wa uhalifu , na kamanda wa Polisi TRC atawajibika katika maeneo yafuatayo:

    i. Dar es salaam- Reli ya kati: Dar es Salaam hadi Dodoma na Singida

    ii. Tabora – Reli ya Kati: Itigi – Kigoma ;Tabora – Shinyanga na Kaliua –Mpanda.

    iii. Mwanza – Mwanza – Shinyanga (bila kuihusisha shinyanga)

    iv. Tanga – Tanga _Moshi-Arusha

    (b) Muundo wa TAZARA umegawanyika katika makundi matatu, yakiwa ni makundi ya kudhibiti uhalifu (kipolisi) ambapo Kamanda wa Polisi TAZARA atawajibika katika maeneo yafuatayo:

    i. Dar es Salaam: Dare s salaam (Pugu) – Kisaki

    ii. Mlimba: Kisaki – Msolwa

    iii. Makambako: msolwa – Uyole-Mbeya

    iv. Mbeya: Uyole-Mbeya-Tunduma

7. (a) Taarifa zote za makosa, ajali na matukio(pamoja na taarifa zisizo rasmi) yanayotokea katikareli yatashughulikiwa kwa mujibu wa PGO 309, bila kujali kwamba katika eneo hilo kuna askiari polisi reli. Mahala ambapo kuwa Polisi reli, kwa kawaida watafanya upelelezi chi ya maelekezo na usimamizi wa kamanda wa polisi wa wilaya.

   (b) taarifa ya kazi zinazohusisha ajali zinazotokana na makutano ya reli na barabara zitatumwa kwa divisheni ya reli Dar es Salaam.

   Ada ya malipo ya ajali(*rejea PGO 292 aya ya 9*) imeondolewa katika kesi za reli. Majalada ya kesi za ajali za namna hiyo yatatumwa kwa divisheni ya reli mara baada ya taratibu zote za kesi kukamilika.

PGO - 12

KIKOSI CHA INTELIJENSIA

MUUNDO NA MAJUKUMU

Kwa ujumla

1. Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai atawaajibika kwa Inspekta Jenerali au, kama hayupo, kwa afisa anayefanya kazi za Inspekta Jenerali kwa ufanisi wa utawala, muundo, na majukumu ya kikosi cha Intelijensia pamoja na utawala, maendeleo, maelekezo, n ausimamizi wa jumla wa Kikosi cha Inelijensia kilichopo idara ya Upelelezi. Makao mmakuu na kikosi cha intelijensia nchi nzima ya Tanzania. Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Headquarters and Crime Intelligence Units throughout Tanzania. Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai atawajibika pia katika dissemination ya intelijensia kwa Insipekta Jenerali mwenyewe au kwa mwakilishi wake au kwa serikali kama itakavyotakiwa au kama atakavyoelekeza Insipekta Jenerali.

2. Mkurugenzi wa Upelelezi atatoa taarifa za mara kwa mara kwa Insipekta Jenerali, mawasikliano na mambo mengine ambayo Mkurugenzi wa upelelezi atakuwa ataelekezwa au vinginevyo kwa niaba ya Insipekta Jenerali.

3. Vikosi vya intelijensia vya mikoa na wilaya vitakuwa chini ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinaina wakuu wa uplelezi wa mkoa na wilaya watakuwa wanamjulisha taarifa za kiintelijensia ikiwa ni pamoja na masuala ya kijinai,yanayoathili usalama wa maeneo yao.

4. (a) Mkuu wa Kikosi cha intelijensia Makao makuu ya CID, na wakuu wa vikosi vya intelijensiawanawajibu wa kuhakikisha kuwa wakuu

wa upelelezi mikoa waanajulishwa matukio ya kiopereshsheni na mambo yote mhimu yanayoathili maeneo yao. Vipengele vya hatua zifuatavyo vitatumika kufanikisha hii : - (i) Mawasiliano yote ya kiusalama yanayopelekwa kwa mkuu wa kitengo cha intelijensia wa mkoa yatakuwa yanapitishwa bila kuchelewa kwa kutumia majalada ya kitengo cha intelijensia kwa mkuu waupelelezi wa mkoa kwa taarifa na maoni.

(ii) Taarifa na tathimini zinazotoka kwa mkuu wa kitengo cha intelijensia wa mkoa kwenda mkuuwa kitengo cha intelijensia makao makuu ya CID yatakuwa yanapitia kwa wakuu wa upelelezi wa mikoa ili waweze kutoa maoni yao kama inahitajika kabla ya kupelekwa kwa mkuu wa intelijensia makao makuu ya CID. maoni hayo yatakuwa yanapelekwa kwa mkuu wa intelijensia makao makuu pamoja na taarifa husika.

(iii) Taarifa toka Zanzibar zitatumwa kupitia kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar

(b) Wakuu wa upelelezi mkoa wanawajibu kuhakikisha kuwa hakuna ucheleweshaji wa vifurushi vya makaratasi ya kitengo cha intelijensia kupitia ofisi zao.

5. Maelezo ya maelekezo ya kuripoti kwa intelijensia kwa mjibu wa para 4 juu yatatolewa na Mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai mara kwa mara.

6. Bila ya kuathili para 3 juu, wakuu wa upelelezi wa mikoa wanamamlaka ya kutoa maelekezo kwa wakuu wa intelijesia wa mikoa kaa itakavyokuwa na lazima ya uharaka na maelekezo hayo yatazingatiwa na wakuu wa intelijensia. Wakuu wa upelelezi wa mikoa watatakiwa kumujulisha Mkurugenzi, idara ya upellezi wa makosa ya jinai mapema iwezekanavyo aina ya amri iliyotolewa, sababu iliyopelekea amri au maelekezo hayo kutolewa.

7. Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kwa niaba ya Insipekta Jenerali wa polisi, anamamlaka ya kutoa amri/maelekezo kwa wakuu wa intelijensia wa mikoa na kama kuna ulazima kufanyia marekebisho maelekezoyaliyotolewa na wakuu wa upelelezi wa mikoa kwa wakuu intelijensia. Katika hali ya kawaida maelekezo hayo yatapitia kwa wakuu wa upelelezi wa mikoa. Wakuu wa upelelezi wa mikoa watahakikisha kuwa amri na maelekezo yanapelekwa kwa wakuu wa intelijensia husika na wanatii.

PGO - 13

POLISI WA KIKOSI CHA WANAMAJI

MUUNDO, MPANGILIO NA MAJUKUMU

Majukumuna mipaka

1. (a) Kikosi cha wanamaji cha Tanzania kipo chini ya Jeshi la Polisi Tanzania.

(b) Mipaka ya Kikosi cha Wanamaji kinatokana na mipaka ya Maji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mipakaya Bahari kutoka kwenye eneo la bahari lililochini ya umiliki wanchi.

(c) Mipaka ya maji ya kikosi cha wanamaji imeoneshwa kwenye kiambatanisho A cha amri hii.

Wajibu mkuu na majukumu

2. kikosi kitakuwa na wajibu na majukumu yafuatavyo:-

(a) kulinda doria eneo la maji lililo ndani ya mipaka ya nchi.

(b) kusaidia hatua za kioperesheni katika maeneo ya nchi.

(c) kufanya shughuli za uokoaji Bajharini

(d) kuhaakikisha usalama na ulinzi wa mali za serikali kwenye milki yao.

Muundo

3. Mkuu wa kamandi ya wanamaji atawajibika kwa Insipekta Jenerali na atakuwa mkuu wa kikosi cha wanamaji Dar es salaam.

4. (a) Makamanda wa Polisi mikoa wanasimamia vikosi vya wanamaji katika mikoa yao isipokuwa masuala ya kiufundi, uhamisho na mgawanyo wa vituo ambayo ni majukumu ya kamanda wa kikosi cha Wanamaji.

(b) Masuala ya kifedha kuhusiana na kikosi cha wanamaji yatatolewa na Insipekta Jenerali mara kwa mara.

5. Wakuu wa vikosi vya wanamaji mikoa watatoa taarifa na za kina kwa Makamanda wa Polisi Mikoa na wilaya kuhusu maeneo yao ya kazi na masuala yote yanayohusu askari wa kikosi cha wanamaji wanaofanya kazi kwenye himaya zao. Watakuwa maofisa wanadhimu kwa makamanda wa polisi mikoa kwa masuala yanayohusu kikosi cha wanamaji na masuala ya kiufundi kwa mkuu wa komandi.

6. (a) ukiondoa Dar es salaam na Zanzibar, makamanda wa mikoa na wakuu wa polisi wa wilaya na wakuu wa vikosi vya wanamaji watawajibika na mwendendo wa utendaji kazi wa kikosi cha wanamaji na nidhamu na usimazi wa karibu kwa askari wa kikosi cha wanamaji wali katika maeneo yao. Watahakikisha wanawasimamia ili utendaji wa majukumu yao yanatekelezwa kwa ufanisi na ufasaha.

(b) ukaguzi wa kikosi cha wanamaji utafanyika mara kwa mara kwa mjibu wa kanuni namba 47. .

(c) wakuu wa polisi wa wilaya watashughulikia malipo na fedha zinazohusiana na askari wa kikosi cha wanamaji.

(d) Stahiki za askari wa kikosi cha wanamaji na huduma za maduka ya polisi zitasimamiwa na makamanda wa polisi wa mikoa.

MAKAMANDA POLISI MIKOA

MPANGILIO WA KIKOSI CHA WANAMAJI

7. Mpangilio wa kikosi cha wanamaji utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Bahari ya Hindi – Dar es Salaam, Zanzibar, Mtwara na Tanga

(b) Ziwa Victoria – Bukoba, Shirati na Mwanza

(c) Ziwa Tanganyika – Kigoma na Kipili

(d) Ziwa Nyasa – Bandari ya Itungi

8. Kikosi cha Wanamaji kiundwa na vitengo vifuatavyo:-

(a) mabaharia

(b) mafundi

(c) wapigambizi

9. (a) Kitengo cha mabaharia kitakuwa na mgawanyo ufuatao, nahodha, wasoma ramani, mabaharia, askari wabeba mitutu, wapaka rangi, waongoza meli, na mafundi.

(b) Nahodha atawajibika kama ifuatavyo:-

(i) Msimamizi mkuu wa meli bila kujali cheo chake au umbele na ni marufuku kwa ofisa yeyote Yule kuingilia kwa namna yeyote ile masuala ya kitaalamu zinazohusiana na chombo.

ANGALIZO: - ofisa yeyote mwenye cheo cha juu kuliko nahodha atakuwa ni msimamizi wa mambo ya kinidhamu tu.

(ii) uratibu wa mawasiliano wa chombo

(c) wasoma ramani watawajibika kwa nahodha katika uendeshaji wa chombo;

(d) kiongozi wa mabaharia atawajibika kwa nahodha katika mambo yafuatayo:-

(i) msimamizi wa shughuli za kila siku zinazofanyika katika meli;

(ii) usimamizi wa jumla wa usafi wa chombo;

(iii) kuhakikisha wanatoa msaada wa kutosha wakati wa safari;

(iv) usimamizi wa bunduki na usafi;

(v) kuwa na askari wa kutosha kwa ajili ya ulinzi na kuweka nanga;

(vi) uratibu wa vyeo mbalimbali na maofisa chomboni.

(vii) mafunzo na kwata kwa askari wa silaha;

(viii) mafunzo ya ubaharia.

10. msimamizi wa kitengo cha ufundi ambacho kinajumisha , mafundi, watu kitengo cha chakula na mafundi umeme watawajika kwa mambo yafuatayo:-

(a) kuandaa mitambo kabla ya kuanza safari;

(b) kukagua uimara wa chombo;

(c) kumjulisha nahodha pindi anaporidhika kwamba mitambo iko

tayari kwa safari;

(d) kuhakikisha usafi wa mitambo, na

(e) kuhakikisha huduma ya chakula yakutosha na huduma ya kwanza inapatikana kwenye chombo.

11. wapigambizi wa watawajibika kwa nahodha na majukumu yao yatajumisha yafuatayo:

(a) shughuli za uokoaji;

(b) kukagua uimara wa chombo;

(c) msimamizi wa wapigambizi, na

(d) kusimamia mafunzo ya mabaharia wapya walioajiliwa katika kikosi pamoja na askari wengine ambao siyo wapiga mbizi.

chakula

12. (a) chakula kitaandaliwa na wapishi waliosomea na kufuzu watakuwa chini ya fundi mkuu.

b) mafundi watakaoajilwa katika chombo lazima wawe na tuzo zinazotambuliwa, kutoka kwenye taasisi zinazotambulika.

(c) ugavi wa chakula utakuwa kama ilivyoelekeza na Insipekta Jenerali kwa kufuata miongozo ya kiuanamaji.

3. huduma ya chakula katika chombo itajumuisha vyakula vikavu kwa ajili ya wakati wa dharula kwa kiwango kinachostahili kwa mjibu wa miongozo ya kiuanamaji.

Utendaji kazi wa meli za kikosi cha wanamaji

(a) Meli ya wanamaji itatumika katika safari ndefu tu chini ya kanuni ya safari za majini FP222 iliyosainiwa a kamanda wa kikosi cha wanamaji Dar es salaam au Makamanda wa polisi mikoa na kwamba Inspekta Jenerali atajulishwa kuhusiana na opersheni na safari hizo mara moja.

(b) Operesheni itahesabika kuwa ni kubwa endapo itavuka umbali wa maili 12 toka usawa wa Bahari.

(c) Amri za safari za majini kwa meli ya wanamaji inayofanya safari katika doria za kawaida na operesheni za dharura itasaininiwa na kamanda wa kikosi cha wanamaji.

Mafunzo ya awali

15. Ili mtu aweze kuingizwa katika kikosi cha Marini lazima awe amepitia mafunzo katika Nyanja zifuatazo:-

(a) ubaharia na uaskari

(b) Usafiri wa majini

(c) Uhandisi wa wanamaji

(d) Kupiga mbizi

(e) Umeme

(f) kutengeneza boti

(g) ufundi wa rada

(h) matumiozi ya rada

(i) kupaka rangi

(j) upishi

Marupurupu

16. askari wa polisi idara ya wanamaji wa vyeo vyote wanastahili kulipwa fedha ya ujuzi maalum kwa wataalamu katika viwango ambavyo vitawekwa na Insipekta Jenerali kila mara na kutangazwa kwenye fosi oda.

Mambo ya ujumla

17. Mkuu wa komandi ya kikosi cha wanamaji atahakikisha kuwa boti zote zilikochini ya himaya yake ni kavukwa ajili ya ukaguzi wa vifaa vyake vikiwa majini na kufanyiwa matengenezo angalau mara moja kila baada ya miezi sita.

KIAMBATANISHO 'A'

To P.G.O. No. 13

MIPAKA YA BAHARI NA SEHEMU ZA KWENYE MAJI

(Mipaka ya bahari na isipokuwa mipaka ya kiuchumi, sura ya Sheria 238 iliyofanyiwa malekebisho 2002)

KIFUNGU 1

MWENENDO WA KISHERIA

IBARA 2

Kwa mujibu wa sheria za mipaka ya bahari, anga, ardhi na kingo za bahari.

1. Mamlaka ya ukanda wa Pwani yapo zaidi ya mipaka ya ardhi na ndani ya maji; kama ni visiwa basi maji yanayozunguka visiwa na ukanda wa bahari kama ilivyo elezewa katika mipaka ya bahari.
2. Mamlaka hayo yanaendelea hadi katika anga zaidi ya mipaka ya bahari,kingo na ardhi.
3. Mamlaka zaidi ya mipaka ya bahari yapo katika mikataba ya kisheria na sheria nyingine za kimataifa.

KIFUNGU 2

MWISHO WA MIPAKA YA BAHARI

IBARA 3

UPANA WA MIPAKA YA BAHARI

Kila Taifa linalo haki ya kuanzisha upana wa mipaka ya bahari kwa kiwango kisichozidi maili 12

kutokana na mikataba ya kisheria.

IBARA YA 4

MWISHO WA MIPAKA YA NJE YA BAHARI

Mwisho wa mipaka ya nje ya bahari ni mstali unaounganisha sehemu yenye umbali toka karibu ya

sehemu ya mstali wa vipimo ambao nia sawa na upana wa mipaka ya bahari.

IBARA YA 5

MSTALI WA VIPIMO

Isipokuwa vinginevyo katika mikataba ya kisheria, mstali wa vipimo kwa ajiri ya upimaji wa mipaka

ya bahari itakuwa ni kina kifupi cha maji ufukweni kama ilivyo chorwa kwa vipimo vikubwa (scale)

na kutambulika

IBARA YA 6

MIAMBA

. Katika kesi ya visiwa hali ya atolls au ya visiwa kuwa miamba iliyo ukingoni, msingi kwa ajili ya kupima upana wa mipaka ya bahari ya taifa seaward za maji mstari wa miamba, kama inavyoonekana kwa alama sahihi kwenye chati na kutambuliwa rasmi na Serikali ya pwani .

IBARA YA 7

Mstari mnyofu wa upimaji.

1. Katika maeneo ambapo ukanda wa pwani kwa undani indented na kukatwa katika, au kama kuna pindo la visiwa katika pwani katika maeneo ya jirani yake ya mara moja, njia ya msingi kujenga moja kwa moja pointi sahihi wanaweza ikatumika katika kuchora msingi ambao upana wa mpaka wa bahari wa taifa ni kwa kipimo.

2. Ambapo sababu ya kuwepo kwa hali ya delta na mengine ya asili katika ukanda wa pwani si imara, pointi sahihi inaweza kuchaguliwa mbali kando

ya sehemu ya bahari kutoka mstari wa chini ya maji, bila ya kujali kurudi nyuma baada ya mstari wa chini ya maji, mstari mnyofu wa upimaji utabakia imara mpaka ubadilishe na uongozi wa pwani kwa kuzingatia mapatano .

3. Kuchora mstari mnyofu wa upimaji si lazima uondoke toka ulekeo wa pwani, na maeneo ya bahari ulala ndani ya mstari ujitoshereze karibu na uwanja wa ardhi kuwa chini ya utawala wa maji wa ndani.

4. Mstari mnyofu wa upimaji usichorwe chini ya wimbi mwinuko, isipokuwa lighthouses au mitambo hiyo ambayo ni ya kudumu juu ya usawa wa bahari imejengwa juu yao au isipokuwa katika matukio ambapo mstari wa upimaji upo katika mwinuko na kimataifa kutambuliwa.

5. Ambapo njia nyofu ya mstari wa upimaji inatumika katika aya ya 1, sababu inaweza kuchukuliwa, katika kuamua mstari wa upimaji, ya maslahi ya kiuchumi pekee kwa mkoa husika, ukweli na umuhimu ambapo ushahidi upo wazi kwa matumizi ya muda mrefu.

6. Mfumo mnyofu wa mstari wa upimaji unaweza kutotumika na Serikali kwa namna ya kukatwa mipaka ya bahari ya taifa jiingine kutoka bahari ya juu au ukiondoa mipaka ya kiuchumi.

IBARA YA 8

ndani ya maji
1. Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya IV, maji upande wa nchi kavu wa mstari wa vipimo wa mipaka ya bahari toka sehemu ya ndani ya maji ya taifa.

2. Ambapo uanzishwaji wa msingi kwa moja kwa moja kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa katika ibara ya 7 ina athari ya kujumuisha kama maeneo ya ndani ya maji ambayo hapo awali hayakuchukuliwa kama vile, haki ya kifungu wasio na hatia kama zinazotolewa katika Mkataba huu, zipo katika maji hayo .

IBARA YA 9
Midomo ya mito
Kama mto unapita moja kwa moja ndani ya bahari, msingi utakuwa mstari moja kwa moja katika mdomo wa mto kati ya pointi kwenye mstari wa chini ya maji na kingo zake.

IBARA YA 10

FUKWE

1. Ibara hii inahusika pekee na fukwe za pwani ambazo ziko chini ya Taifa moja.

2. Kwa mikataba hii, fukwe ni sehemu kubwa ya maji iliyo zungukwa na nchi kavu ikiwa na nafasi inayoruhusu maji ya bahari kupita.

3. Kwa ajiri ya upimaji, fukwe ni eneo lililopo kati ya eneo dogo la maji kuzunguka pwani na mstali unaounganisha alama ya maji madogo katika sehemu ya kuingilia. Kwasababu ya visiwa, fukwe zina zaidi ya sehemu ya kuingilia, nusu duara ni lazima lichorwe kwa urefu toka visiwa tofauti tofauti.

4. Umbali kati ya eneo dogo la maji katika sehemu ya kuingilia ya fukwe kama halitozidi 24 mwendokasi, kutachorwa mstali ambao utaunganisha sehemu mbili za eneo dogo la maji na majiya eneo hilo yatashukuliwa kama maji ya sehemu hiyo.

5. Kama umbali kati ya eneo dogo la maji katika sehemu ya kuingilia itazidi 24 mwendokasi, kutachorwa ndani ya fukwe kwa maana ya kuchukua eneo kubwa la maji.

IBARA YA 11

BANDARI

Kwa madhumuni ya kutozuia mipaka ya bahari kwa mipaka ya nje ya bandari ambayo ni

sehemu ya mifumo inayotengeneza sehemu ya pwani. Visiwa ambavyo siyo vya halisi

havijumuishwi kama sehemu za kudumu za kazi ya bandari.

IBARA YA 12

GATI

Gati linatumika kupakia, kutelemshia mizigo na kufungia meli, linaweza kuwa ni sehemu au

lotelipo nje ya mipaka ya bahari lakini linajumuisha katika mipaka ya bahari.

IBARA YA 13

KUPWA

1. Kupwa ni ile hali ya maji yanapokuwa machache na kuhacha eneo la wazi na kuzama pindi maji yanapojaa. Pia kupwa ni hali ya ujumla au sehemu kwa umbali usiozidi upana wa mipaka ya bahari toka nchi kavu hadi visiwani. Kupwa huku ndiyo chanzo cha kupimia upana wa mipaka ya bahari.
2. Kupwa endapo kutazidi umbali wa upana wa mipaka ya bahari toka nchi kavu au visiwa kutakuwa hakuna mipaka ya bahari.

IBARA YA 14

Njia mbalimbali za kutambua mwanzo wa upimaji.

Ukanda wa pwani unaweza kutambua mwanzo wa upimaji kwa njia yeyote iliyo tumika kukidhi

hali tofauti tofauti.

IBARA YA 15

Mipaka inayoonyesha mipaka ya bahari sanjari au kinyume na pwani.

Wakati pwani ya Mataifa mawili yanayotizamana au ambayo yapo sanjari kwa kila moja, hakuna

Taifa ambalo limemilikishwa au kushindwa mapatano kati yao na kupanua mipaka ya bahari zaidi

ya nusu toka kwa kila eneo la upimaji. Hali hiyo haikubaliki isipokuwa kama kunaulazima kutokana

na umiliki wa kihishoria au mazingira maalumu.

IBARA YA 16

MICHORO NA MIPAKA YA KIJOGRAFIA


1. Mwanzo wa upimaji wa upana wa mipaka ya bahari inatambulika toka Ibara ya 7, 9 na 10 na mistari ya mipaka iliyochorwa kwa mujibu wa Ibara ya 12 na 15 ni lazima ichorwe kwa vipimo (scale).

2. Ukanda wa Pwani lazima uonyeshe mahitaji ya jamii ndani ya mchoro au maali halisi juu ya ardhi na kuweka nakala ya kila mchoro kwa Katibu Mhutasi wa Umoja wa Mataifa.

APPENDIX B

To P.G.O. No 13

MPANGILIO WA UONGOZI KATIKA KIKOSI CHA WANAMAJI



PGO NO.14

KIKOSI CHA BENDI

MUUNDO NA MAJUKUMU YAKE.

MUUNDO;

1. (a) kikosi cha bendi kitakuwa chini ya Mrakibu wa kikosi ambaye makao makuu yake yatakuwa Dar –es-salaam.

   (b)Maswala yote yanayohusu kikosi cha bendi Zanzibar yatakuwa chini ya kamishna wa Zanzibar.

MUUNGOZO;

2.Kikosi cha bendi kitafanya kazi katika maeneo yafuatayo;-

(a) Polisi bendi Dar es salaam.

(b) Polisi bendi cha T.P.S Moshi.

©Polisi bendi cha ZBR.

3.Muundo wa uendeshaji wa kikosi cha bendi kama inavyoonekana katika jedwali ‘A’.

4.Majukumu ya mkurugenzi wa Muziki:-

(a)Mkurugenzi wa muziki atakuwa na majukumu ya kutoa mafunzo,nidhamu,ustawi na malipo ya watumishi waliopo Dar es salaam.Pia usimamizi wa kikosi cha bendi ikiwa ni pamoja na nguoa na vifaa vinavyohusu watumishi wa kikosi cha bendi cha Dar es salaam.Mpangilio na majukumu kwa ujumla.

(b)Atakuwa na jukumu la kuongoza na kupangilia safari zote kwa njia ya reli au barabara na kushughulikia vibali.

(c) Atakuwa muangalizi wa hesabu zote za kikosi cha bendi,Fedha,mali na sehemu za kuhifadhia.

5.Kamishna wa Zanzibar atakuwa na majukumu ya kusimamia nidhamu,ustawi na malipo ya watumishi wa kikosi cha bendi Zanzibar.

6.mkurugenzi wa muziki atafanya ukaguzi wa bendi zote za Polisi mara nne kwa mwaka hii ni kulingana na P.G.O. 47 na kumshauri Inspekta Jenerali wa Polisi maswala yote yanayohusiana na muziki.

7.Mkurugenzi wa muziki atakuwa na jukumu la kuagiza vifaa vipya na kubadilisha vilivyochakaa.

8.Mkuu wa chuo cha P.T.S.Moshi atasimamia PTS bendi akisaidiwa na msimamizi wa P.T.S bendi Moshi.

Appendix

A

MUUNDO WA KIKOSI CHA BENDI

Mkurugenzi wa muziki

Mkuu wa kikosi Zanzibar Mkuu wa kikosi PTS Mkuu wa kikosi Moshi Dar es salaam.

PGO - 15

MWONGOZO NA AMRI ZA UTENDAJI WA KAZI – JESHI LA POLISI

KITENGO CHA MBWA NA FARASI – KATIBA TAASISI NA WAJIBU WA KATIBA.

1. Kitengo cha Mbwa na Farasi kinapata maelekezo chini ya Kamanda wa Mbwa na Farasi ambacho kimeundwa na Jeshi la Polisi kwa mafunzo maalum na kimejiimalisha kufanya kazi za operasheni ili kutoa msaada katika utendaji kazi za polisi na upelelezi.

2. TAASISI
   Kitengo cha Mbwa na Farasi kimeanzishwa katika Mikoa kwa maelekezo ya Inspekta Jenerali wa Polisi.

3. Makao Makuu ya kitengo cha Mbwa na Farasi kipo Mkoa wa Dar es Salaam na kitengo cha operation kitafanya kazi chini ya maelekezo ya Inspekta Jeneral wa Polisi.

4. Wanachuo/wanafunzi wote wa Mbwa na Farasi watapata mafunzo kwenye chuo cha MPA/CCP kabla hawajahamishwa kwenda kwenye vitengo vyao vya Mikoani.

5. Mawasiliano yote ya kitengo cha Mbwa na Farasi kimkoa yatafanywa kupitia kwa Kamanda wa kikosi cha Mbwa na Farasi kwenda kwa Inspekta Jenerali wa Polisi ambaye atapewa taarifa zote muhimu na changamoto kuhusu kitengo.

6. Kitengo cha Mbwa na Farasi wakati wote kitafanya kazi chini ya maelekezo ya kamandi husika, wakati mwingine watawajibika kutii.
   (a) Amri zote zinazotolewa na Kamanda wa Mkoa au Afisa anayekaimu ofisi hiyo.

   (b) Amri kutoka kwa Afisa aliyopo kwa wakati huo sizipingane na maelekezo yaliyokwishatolewa na Kamanda wa Mkoa

7. <u>MAJUKUMU YA KIONGOZI WA MBWA NA FARASI</u>
   Mkuu wa kikosi cha Mbwa na Farasi anawajibika kwa Inspekta Jenerali wa Polisi

   (a) Mafunzo na uhamisho wa Askari Polisi wote wa kikosi cha mbwa na farasi
   (b) Utaratibu wa ukaguzi wa kikosi cha Mbwa na Farasi utafuata kama ulivyoainishwa katika kitabu cha mwongozo na amri za utendaji kazi wa Jeshi la Polisi (PGO) namba 47.

   (c) Matumizi ya Mbwa na Polisi yafanyike kwa mujibu wa sheria.

   (d) Hakikisha kwamba Mbwa na Farasi wanafanya mazoezi na wanapata chakula na matibatu ya kutosha ili wawe na afya njema kwa muda wote.

   (e) Utoaji na utekelezaji wa mafunzo maalumu uwekewe msisitizo kwa kuzingatia mahitaji ya Mbwa na Farasi.

   (f) Amri zote za utendaji zinazotolewa mara kwa mara zihusishe vitengo vyote.

   (g) Taratibu zote za uhamisho zifuate maelekezo yote yaliyopo kwenye mwongozo wa amri za utendaj wa kazi za jeshi la Polisi


(PGO) namba 59 (5) (c).

8. Makao Makuu ya Mkoa kitengo cha Mbwa na Farasi yapo chini ya usimamizi wa Kamanda wa Mkoa husika ambae tena anao wajibu kuangalia utendaji na nidhamu ya kitengo kinachotoa huduma katika komandi yake.

9. Kamanda wa Mkoa atalazimika kutumia kitengo cha Mbwa na Farasi ili kusaidia askari wa CID kufanya doria kwenye misafara mirefu, misako, na utambuzi wakati wa kufuatilia vitu vinavyosafirishwa, mfano milipuko na vitu vitakavyotiliwa mashaka.

SURA “A”

UTAWALA - KITENGO CHA MBWA NA FARASI



PGO - 16

KIKOSI CHA ANGA

MUUNDO,MPANGILIO NA MAJUKUMU,

MUUNDO:

1.Afisa mkuu wa kitengo cha anga atawajibika kwa inspekta jenerali wa polisi katika kusimamia na kurakimu askari wa kikosi cha anga.

2.stesheni ya kikosi cha anga itakuwa dsm au sehemu yeyote km itakavyoelekezwa na Inspekta jenerali nawa polisi

3:Afisa mkuu wa kitengo cha Anga atakuwa na usimamizi wa moja kwa moja juu ya shughuli /kazi zifuatazo za kiutawala:-

[a]Kutoa usafiri wa anga katika jeshi

[b]Kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za serikali zinazoendana na kikosi cha anga.

[c]Kusimamia operesheni zinazohusu mafunzo ya anga kwa polisi

[d]Kusimamia kujiamin na ueledi wa watu waliopo katika himaya yake.

[e]Kuendesha doria za anga kama itakavyoelekezwa kutoka kipindi hadi kipindi.

MUUNDO:-

4.Kikosi cha anga kitakuwa na mgawanyiko wa marubani, injinia mafundi na maafisa wa polisi wenye vyeovyeo mbalimbali kama itakavyoamuliwa na Inspekta jenerali wa polisikutoka kipindi kimoja hadi kingine.

5.Kikosi cha anga kitakuwa na muundo wa sehemu zifuatazo:-

[a]Marubani

[b]Mainjinia

[c]Utawala

[d]Stoo

MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA KIKOSI CHA ANGA

6.Majukumu ya kikosi cha Anga ni kama yafuatavyo:-

{a}Kikundi cha marubani

Kitakuwa na jukumu la kupangilia urukaji wa ndege,kutoa maelekezo katika usimamizi wa ndege na mizigo wakati wa urukaji na usafi wa ndani ya ndege na abiria wakati wa urukaji chini ya amri ya Rubani Mkuu ambaye ataaidiwa na mkufunzi mkuu ambaye atasaidiwa na mkufunzi mkuu na afisa mitambo.

{b}Kikundi cha Mainjinia

Kitakuwa na jukumu la maandalizi ya ndege kabla haijaruka na hanapojiridhisha kwa ndege kuruka kmjulisha Rubani mkuu .Kikundi hiki kitakuwa na jukumu la usafi wa ndege kiujumla .Kikundi hiki kitakuwa na shughuli ya utengenezaji wa ndege mara kwa mara kuendana na sheria za Anga

{c}SEHEMU YA UTAWALA

Itakuwa na jukumu lakusimamia utawala kiujumla,nidhamu kwa wafanyakazi na mawasiliano ya kipolisi ndani ya kikosi cha Anga na itaongozwa na staff Mkuu wa polisi atakayeteuliwa na Inspekta jenerali wa polisi.

{d}SEHEMU YA STOO

Itakuwa na jukumu la kuhifadhi vifaa mbalimbali viusuvyo ndege na kupeleka vifaa vilivyopo kwenye ndege kwa watengenezaji wa ndege hiyo kwa

matengenezo na itaongozwa na afisa boharia mwenye elimu ya uboharia na upokeaji na upelekaji wa bidhaa

7.{a}Kwa vile polisi aitoi mafunzo ya anga ,uajili katika sehemu hii ya kiutaalamu utatoka kwa wahitimu waliomaliza mafunzo ya Anga kwa taasisi husika .

{b}Uajili wa ndani ni chanzo kingine cha wafanyakazi wa kikozi cha Anga ambapo waliochaguliwa kutoa huduma wake kwa waume hupelekwa kwenye Taasisi za kimafunzo kabla ya kuhamishiwa kikosi cha Anga .

POSHO:

8.Wafanyakazi wa kikosi cha Anga wa vyeo mbalimbali wanahitajika kulipwa posho kuendana na viwango mbalimbali vitakavyoelekezwa na Inspekta jeneraliwa polisi kutoka muda hadi muda .

CHATI INAYOONYESHA MUUNDO WA KIKOSI CHA ANGA

KAMANDA KIKOSI CHA

.

.

. ---------- AFISA MNADHIMU KIKOSI CHA ANGA

; ----------.----------: .

/ . /

SEHEMU YA MARUBANI / SEHEMU YA MAINJINIA / SEHEMU YA STOO

KIKOSI CHA USALAMA BARABARANI

Imetafsiriwa na: Insp. Mohamed Kilongo na Insp.Mohamed Salum wa GO 2

DPA
[Pick the date]

PGO - 17

KIKOSI CHA POLISI VIWANJA VYA NDEGE

MUUNDO MPANGILIO MAJUKUMU

MUUNDO

1. Kamanda wa Kikosi Viwanja vya Ndege atasimamia vituo vyote vya polisi Viwanja vya Ndege Tanzania.

2. The commanding officer airports police unit will exercise direct control over division units in the regions, subject to the following general administrative duties which will still be the responsibility of the Airports Commanding Officer:-

(a) Sera ya kazi za kawaida kwa askari wa Viwanja vya Ndege.

(b) Utaratibu wa mgawanyo wa vituo vya kazi, likizo na uhamisho.

(c) Mapendekezo ya mgawanyo wa fedha kutoka Kikosi cha Viwanja vya Ndege kwa utaratibu ufuatao :-

(i) mshahara binafsi;

(ii) usafiri na safari;

(iii) safari wakati wa likizo;

(iv) ofisi na mengineyo;

(v) umeme;

(vi) matengenezo na uendeshaji wa magari;

(vii) bohari;

(viii) chakula kwa mashahidi na watuhumiwa;

(ix) simu na simu za maandishi, na

(x) stahiki za askari wa vyeo mbalimbali.

(d) ikizingatiwa kwamba mkuu wa polisi wilaya na kituo wanatakiwa kupatiwa taarifa kamili juu ya masuala yahusuyo askari wa viwanja vya Ndege wanaofanya kazi kwenye himaya zao.

(e) ikizingatiwa kuwa askari wa idara ya upelelezi wa kiwanja

wanatakiwa kupatiwa msaada kwa kesi kubwa na zile zenye utata

3. (a) Kamanda wa Polisi Viwanja vya ndege na mkuu wa polisi wilaya na wakuu wa vituo wanawajibika kwa mwenendo wa kazi wa kikosi cha viwanja vya ndege na nidhamu ya askari na usimamizi wa karibu wa askari wa kikosi waliopangiwa kwenye maeneo yao. Watawasimamia kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na wanaendelea kulinda maslahi ya utawala ya viwanja vya Ndege.

(b) ukaguzi wa vikosi viwanja Ndege utafanyika mara kwa mara kwa mujibu wa PGO 47

(c) Mkuu wa polisi wilaya na kituo atashughulikia malipo yanayohusu kikosi cha viwanja vya ndege na itajumuisha askari wa viwanja vya ndege na utaratibu wa stahiki zao.

Mpangilio na maeneo ya polisi

Mfumo wa viwanja vya ndege umegawanyika katika sehemu nane kwa ajili ya uthibiti wa kipolisi na kikosi cha viwanja vya ndege kitawajibika kwa kazi za kipolisi kama ifuatavyo:-

(a) DAR ES SALAAM- Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere

(b) KILIMANJARO -Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro

(c) MWANZA - Uwanja wa Ndege wa Mwanza

(d) DODOMA - Uwanja wa Ndege wa Dodoma

(e) MTWARA - Uwanja wa Ndege wa Uwanja wa Ndege wa Mtwara

(f) ARUSHA - Uwanja wa Ndege wa Arusha

(g) ZANZIBAR - Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar

(h) PEMBA - Uwanja wa Ndege wa Chake Chake

5. Viwanja vingine vya Ndege vitatolewa huduma na askari wa kawaida na matukio yatakayokea kwenye kiwanja cha ndege yatashughulikiwa na kituo kilicho karibu’

Wajibu na majukumu

6. Kikosi cha Viwanja vya Ndege kinawajibika kwa kutekeleza majukumu ya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulinda usalama wa anga dhidi ya uvamizi.

7. Wajibu mahsusi wa Kikosi cha Viwanja vya Ndege katika maeneo ya usalama wa anga ni kama ifuatavyo:-

(a) kuzuia na kubaini makosa katika maeneo ya uwanja wa ndege.

(b) Ufuatiliaji wa mara kwa mara na doria za maeneo ya Viwanja vya Ndege katika maeneo yote.

(c) Ufuatiliaji wa abiria wanaofika na kuondoka au watu wanaoweza kuhatarisha usalama wa anga;

(d) Mipango mathubuti ya ushirikiano na uratibu ya ushirikiano na uratibu kwa kushirikisha utawala wa viwanja vya Ndege, Mamlaka ya usalama wa Anga Tanzania, Kikosi cha Zima Moto Viwanja vya Ndege, Komandi ya Anga ya Jeshi kala Wananchi Tanzania, kwa ajili ya kukabiliana na kuthibiti vitendo vya utekaji nyara, hujuma,mabomu,au matishio mengine yeyote uvamizi wa nchi kavu pamoja na uvunjifu wa amani;

(e) Utoaji huduma ya kitaalamu inayojumuisha sio tu huduma zinazohusiana na kitengo cha kupambana na ugaidi na mbinu za kukabiliana na kutegua mabomu kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania;

(f) Kujenga uwezo wa kukabiliana na matukio makubwa kwa haraka katika viwanja vya ndege vyote kwa kushirikiana na kikosi cha Anga cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania;

(g) kutoa mafunzo ya kutosha kwa askari polisi kuhusiana na usalama wa anga na taratibu zinazohusu shughuli hizo;

(h) Kuwakamata waharifu wanaovunja sheria na kanuni za usalama wa anga;

(i) kushirikiana na Polisi wa Kimataifa katika masuala ya usalama wa Anga;

(j) Kushirikiana na kuratibu kwa pamoja na kitengo cha usalama wa anga;

(k) kushiriki kwenye upekuzi na uokoaji wa abiria waliokatika ndege zilizopata ajali zna zile zilizo katika matatizo;

(l) Kuzuia na kupambana na madawa yak ulevya kwa kushirikiana na kitengo cha Kuzuia madawa ya kulevya;

(m) Usindikizaji wa viongozi wa serikali na watu mashuhuri.

8. Taarifa zote zinazohusu makosa, ajali na matukio (ikijumuisha kasoro, dosari itashughulikiwa kwamjibu wa PGO 309 bila kujali uwepo wa askari wa viwanja vya ndege. Askari polisi viwanja vya ndege wanapokuwepo watafanya upelelezi chini ya maelekezo na usimamizi wa mkuu wa polisi wa wilaya na vituo.

10. Taarifa zote za kesi za ajali zinazotokea katika njia ya ndege zitatumwa kawa kamanda wa viwanja vya ndege Dar es salaam. Malipo ya ada za ajali (kwa mjibu wa PGO 292 aya 9 zimeondolewa kwa viwanja vya Ndege. Majalada yahusuyo ajali za magari yataandaliwa na kutumwa kwa Kamanda wa Kikosi cha Viwanja vya Ndege inayohusu mwisho wa mwenendo wa shauri.

PGO - 18

KIKOSI CHA USALAMA BARABARANI

MUUNDO, MFUMO NA KAZI ZAKE

MUUNDO:

1. Kamanda Mkuu wa kikosi cha Usalama barabarani atawajibika kwa mkuu wa jeshi la Polisi kwa mambo yote yanayohusiana na utawala

na usimamizi wa usalama barabarani.

2. (a) Mambo ya Usalama barabarani kwa Zanzibar yataratibiwa na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani (ZBR) ambaye atawajibika kwa kamishna wa Polisi Zanzibar.

   (b) taarifa zote juu Usalama barabarani kutoka Zanzibar kwa Inspekta Jenerali zitanakiliwa kwa kamanda wa Kikosi cha usalama Barabarani.

3. Kamanda wa Kikosi cha Usalama barabarani pia atakuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na ofisi yake itakuwa kamati ya utendaji ya baraza hilo.

Muundo:

4. Kikosi cha usalama Barabarani kitagawanyika kama ifuatavyo:
   a) Kikosi cha Usalama barabarani (Makao Makuu ya Polisi)
   b) Ofisi za Usalama barabarani ngazi ya Mkoa
   c) Kikosi cha Usalama barabarani ngazi ya wilaya
5. Muundo wa Kikosi cha Usalama barabarani umewekwa katika kiambatanisho “A” kwa utaratibu huu:

KAZI ZA KAMANDA MKUU WA KIKOSI CHA USALAMA BARABARANI.

6. (a) Kamanda Mkuu wa Kikosi cha Usalama barabarani atawajibikwa kwa mambo yafuatayo;
   i. Amri zote, utawala na usimamizi wa kikosi cha usalama barabarani nchini.
   ii. Upangaji wa kazi katika maeneo, uhamishaji wa watendaji wa kikosi hicho ndani ya jeshi
   iii. Kutoa maelekezo na amri za utendaji kiufasha kwa maafisa wa mikoa wa kikosi hicho kupitia kwa makamanda wa mikoa ambao pia watahakikisha kuwa amri na maelekezo hayo yamepitishwa kwa makamanda wa kikosi hicho wa mikoa kwa utekelezaji.
   iv. Ukaguzi wa kawaida wa vituo vya mikoa vya usalama barabarani, kuhakikisha kwamba usimamizi wenye tija wa shughuli za usalama barabarani, utendaji na utii wa sheria na taratibu zinafuatwa.

v. Maendeleo juu ya utekelezaji wa program ilyojikita kwenye unyambulishaji wa ajali.

vi. Kuhakikisha utekelezaji wa sheria za usalama barabarani na miongozo inafuatwa kwa nchi nzima.

vii. Kutoa elimu kwa jamii na mpango mahususi kwa taadhari juu ya mambo ya usalama barabarani.

viii. Kumtaarifu Mkuu wa Jeshi la Polisi kuhusiana mna mambo uya usalama barabarani nay ale yenye manufaa maalum kwa maendeleo ya miongozo ya usalama barabarani nchini.

ix. Kumshauri Mkuu wa Jeshi la Polisi juu ya mambo ya usalama barabarani na sera.

x. Ni kiungo kwa taasisi zingine na wadau wa mambo ya usalama barabarani kwa mtazamo wa kuendeleza usalama barabarani kwa ujumla.

xi. Kusimamia na kunyambulisha mambo ya usalama barabarani panapotokea ajali, kuelekeza eneo, siku, muda na usababishaji wa ajali za barabarani na kushiriki katika matokeo hayo na taasisi zingine zinazohusizna na usalama wa barabara kama vile baraza la Taifa la usalama barabarani

xii. Kusimamia ukusanyaji na uratibu wa takwimu za mambo ya usalama barabarani na kuwasilisha taarifa kwa kila kipindi kama ilivyoelekezwa na PGO 59.

xiii. Kukagua, kuidhinisha na kusajili vibali vya uendeshaji vyombo vya kimataifa.

xiv. (a) Kukagua, kuidhinisha na kusajili shule za kufundishia udereva na shule za uelekezi.

(b) katika kusimamia nidhamu na shughuli za utawala, Kamanda mkuu wa Kikosi cha usalama barabarani atasaidiwa na mnadhimu, na maafisa wengine kama hao au wakaguzi katika sehemu ifuatayo:

i. Kitengo cha utafiti na takwimu

ii. Elimu, mafunzo na kitengo cha utoaji habari kwa umma.

iii. Usafirishaji kwa njia ya barabara, sheria na kitengo kihusucho ajali na,

iv. Kitengo cha Usalama barabarani Zanzibar

(c) Mkuu wa kitengo cha utafiti na takwimu atawajibika moja kwa moja kwa kamabda wa kikosi cha usalama barabarani kwa kuweka kumbukumbu na kutunza Takwimu za ajali, kuandaa na kuwasilisha marejesho ya kila mwaka.

(d) mkuu wa kitengo cha elimu, mafunzo na utoaji habari kwa umma atawajibika moja kwa moja kwa umma, kwa kamanda mkuu wa kikosi cha usalama barabarani kwa kuifahamisha jamii kuihamasisha na kuisisitiza katika mambo ya usalama barabarani.

(e) kitengo cha ajali na usafirishaji kitawajibika moja kwa moja kwa kamanda wa kikosi cha usalama barabarani kwa kutambua vyanzo vya ajali na mapendekezo ya malipo stahiki ikiwa ni pamoja na matumizi,tafsiri na maendeleo ya sheria barabarani.

KAZI ZA KAMANADA WA USALAMA BARABARANI WA MKOA

7. (a) Makamanda wa mikoa Usalama barabarani watawajibikwa kwa Kamanda Mkuu wa kikosi cha Usalama barabrani kupitia kwa kamanda wa Polisi wa mkoa kwa mambo yafuatayo:

   i. Kusimamia mambo ya usalama barabarani katika mikoa yao husika .

   ii. Kufanya ukaguzi wa magari kama itakavyohitajika na hasa kutokana na ajali au kwa sababu zingine itakavyoelekezwa na Kamanda wa Kikosi cha usalama barabarani kwa kila itakapohitajika.

   iii. Kusimamia ufaulu wa majaribio ya uendeshaji wa magari kwa waomba leseni.

   iv. Kusimamia adhabu kwa njia ya faini,ukiukwaji wa sheria na uendeshaji.

   v. Kuratibu na kusimamia usindikizaji wa misafara ya viongozi.

   vi. Kufuatilia na kusimamia barabara, doria za barabara kuu za mwendo kasi.

   vii. Kufanya na kusimamia upelelezi wa uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

viii. Kudhibiti usalama barabarani na doria za barabara kuu.

ix. Uangalizi wa vizuizi barabarani

x. Uangalizi na usimamizi wa matumizi ya alama za punda milia na vivuko vya waenda kwa miguu katika taa za barabarani na mahali penginepo.

xi. Kuhakikisha kwamba mwenendo wa vyombo vya usafiri vinaenda kwa hali nzuri kwa nyakati tete.

xii. Usimamizi na upasuaji wa kitaalam hospitalini kwa watu waliokufa kwa ajali.

xiii. Kuhakikisha kwamba usalama barabarani unakuwepo kwa umma kwa wakati wote; katika jambo hili, kama kutakuwepo na upungufu wa watendaji kazi, nguvu kazi itahitajika apatiwe nguvu kazi ya askari wengine wa kazi za kawaida toka kwa kamanda wa polisi wa mkoa.

xiv. Wepesi wa kufanya marejesho kwa mujibu wa PGO 375, 376,286,309 na 320.

xv. Kupangilia usindikizaji wa mizigo na mizigo isiyokuwa na ukubwa wa kawaida iliyozoeleka.

xvi. Kufanya oparesheni kwa kutumia vifaa vya kupima mwendo kasi; na

xvii. Kufanya oparesheni kwa kutumia vifaa vya kupimia pumzi au upumuaji.

(b) Makamanda wa mikoa wa usalama barabarani watatekeleza kazi zao wakisaidiwa na vitengo vifuatavyo:

i. Kitengo cha doria barabarani

ii. Kitengo cha ukaguzi wa magari

iii. Kitengo cha upelelezi kesi za usalama barabarani

iv. Kitengo cha kumbu kumbu

(c) Mkuu wa kitengo cha doria barabarani atawajibika kwa kamanda wa mkoa wa usalama barabarani kwa mambo yafuatayo;

i. Kufanya doria kwa barabara kuu na za kawaida

ii. Kutawala na kusimamia maeneo ya ajali

iii. Kusimamia mtiririko na kumudu barabara za mwendo kasi na za kawaida.

iv. Kusimamia misafara ya viongozi

v. Kuwasilisha taarifa kw viongozi wao wa juu kuhusiana na mambo yaliyojitokeza nje ya doria za barabarani.

(d) Mkuu wa kitengo cha ukaguzi wa magari atawajibika kwa kamanda mkoa usalama barabarani kwa mambo yafuatayo:

i. Kukagua magari chakavu na kuyatolea taarifa zake,

ii. Kukagua magari yaliyohusika na ajali na kuyatolea taarifa,

iii. Kufanya majaribio na mitihani kwa waomba leseni za kuendeshea, na

iv. Kufanya marejesho kuhusiana na ukaguzi wa magari.

(e) mkuu wa upelelezi wa kitengo cha usalama barabarani atawajibika kwa kamanda wa mkoa wa usalama barabarani, kwa mambo yafuatayo:

i. Kupeleleza kesi za usalama barabarani,

ii. Kusimamia upasuaji wa kidaktari hospitalini kwa watu waliokufa kwa ajali,

iii. Kupangilia vizuri majalada ya kesi za usalama barabarani,

iv. Kuratibu na kuandaa mashtaka ya kesi za usalama barabarani kwa kushirikiana na kitengo cha uendeshaji mashtaka ya kesi za usalama barabarani,

v. Kusimamia kuitwa shaurini na kuwalinda mashahidi katika kesi za usalama barabarani,

vi. Kajalidi marejesho kuhusiana na upelelezi wa kesi

(f) Mkuu wa kitengo cha kumbukumbu cha usalama barabarani atawajibika kwa kamanda wa mkoa wa usalama barabarani kwa mambo yafuatayo:

i. Kutunza kumbukumbu za majalada yanayohusu mambo ya usalama barabarani

ii. Kuandaa na kuwasilisha marejesho kwa mujibu wa PGO 372; na


iii. Kuandaa fomu za usalama barabarani kuhusiana na ajali zilizotokea.

KAZI ZA MKUU WA KIKOSI CHA USALAMA BARABARANI WA WILAYA

8. Mkuu wa kitengo cha usalama barabarani wa wilaya atawajibika kwa kamanda wa mkoa wa usalama barabarani kupitia kwa kamanda wa polisi wa wilaya kwa utekelezaji wa mambo yote yanayohusu usalama barabarani ya wilaya husika.

Kiambatanisho "A"
Kwa PGO 18

CHATI YA MUUNDO WA KIKOSI CHA USALAMA BARABARANI



PGO - 19

TUO NA VIKOSI – MADARA

1. Uanzishwaji wa vituo vya polisi (kM vituo vilivyoINISHWA NA Makao

WAKUU WA VITUO VYA USALAMA BARABARANI

Makuu ya Polisi) vitakuwa na madaraja "A", "B" au "C" kulingana na orodha ya kiambatanisho "A".

2. (a) Vituo daraja "A" vinatakuwa kuwa na askari zaidi ya 100 wa vyeo vya Rank&file

(b) Vituo daraja "B" vinatakiwa kuwa na askari zaidi ya 50 lakini chini ya 100 Rank & File.

(c) Vituo daraja "C" vitakuwa na askari 50 au chini yake wa Rank & File.

2. Jina "vituo vidogo vya polisi" vitatumika tu kwa matumizi ya muda mfupi

APPENDIX "A" To

P.G.O. No. 19

VITUO VYA POLISI DARAJA "A"

Arusha
Babati
Bagamoyo
Bariadi
Bomang'ombe
Buguruni
Bukoba
Bukombe
Bunda

Central P.S. (DSM)
Chakechake

Chang'ombe (DSM)
Chunya
Dodoma
Geita
Ifakara
Ileje
Iringa
Kahama
Kasulu
Katesh
Kibaya
Kibondo
Kigamboni
Kigoma
Kigoma Kati
Kilosa
Kilwa
Kisarawe
Korogwe
Kwimba Ngudu
Kyela
Lindi
Liwale
Madema

Magomeni
Magu

Mahenge

Mahonda
Malindi

Malindi/Traffic

Masasi

Maswa

Mazizini

Mbeya
Mbinga
Meatu
Mkokotoni
Mkuranga
Mkuu Rombo
Morogoro
Moshi
Mpanda
Msimbazi (DSM)
Mtwara Kati
Mugumu

Musoma
Mwadui
Mwanakerekwe
Mwanga
Mwanza Kati
Mwera
Nachingwea
Namanyere

Nansio Ukerewe

Newala

Ngambo

Oysterbay (DSM)
Railways (DSM)
Same
Shinyanga
Singida
Songea
Sumbawanga
Tabora
Tanga
Tarime

Traffic (DSM)
Tukuyu
Tumbi
Tunduru
Usa River
Utete
Vwawa
Ngara
Muleba

VITUO VYA POLISI DARAJA "B"

Bandarini

Biharamulo
Bububu

Buhemba
Butiama
Chalinze
Dar es SalaamChuo
Kikuu

DIA Airport
Fuoni
Handeni
Himo
Igogo
Igunga
Ikwiriri
Ilala
Inyala
Iramba
Kamachumu
Karagwe
Karatu

Kawe
Kawe
Kengeja
KIA
Kiabakari
Kibiti
Kigoma Reli

Kijitonyama

Kilimatinde

Kilwa Road (DSM)
Kimamba
Kiomboi
Kirumba
Kondoa
Kongwa
Kwerekwe

Kyaka
Loliondo

Longido

Lushoto
Mabandampakani
Majengo

Makambako
Makunduchi
Manyoni
Manyovu
Maswa

Mbozi
Mbulu
Mfenesini
Micheweni

Mikumi

Mingoyo
Mkoani
Mlandizi
Mombo
Monduli
Mpwapwa
Mtama

Mtwara Airport
Mufindi
Muheza
Mwanza Airport
Mwanza North
Mwera

Nachingwea

Newala
Ngamiani (Tanga)
Ngare Nairobi
Ngerengere
Ngorongoro
Ngudu
Njombe
Nyamwaga
Nyaronga

Nzega
Pangani
Rombo

Ruangwa

Sanya Juu
Selander Bridge
Sengerema
Shirati
Shirati Wanamaji
Sikonge Nzega
Sirari
Stakishari
Sumbawanga (Ufipa)
Tabora Railway,
Tarakea
Tunduma
Tunduru
Ujiji
Urafiki
Urambo
Wazo Hill

VITUO VYA POLISI DARAJA “C

Amani
Basuto

Bayagu

Bereko

Bisumwa

Borega

Borogonja

Buckreef

Bugarama

Buhemba
Bukene

Bukima

Bukoba Railway

Bukoli

Bukumbi

Bulamba

Busangi

Busisi

Butundwe

Bwanga

Bumbwini

Chala

Chato

Chikuyu

Chimala

Chipogoro

Choma

Chwaka

Dabalo

Dodoma Airport

Dodoma Railway

Dumila

Dunga

Fuoni

Gairo

Gamasara

Gingilian
Gonja
Halungu

Haneti

Heka Azimio

Ibaga

Iboja

Igalula

Igirubi

Iguguno

Igurusi

Ihanja

Ikungi

Ilongero

Ilula

Inyonga

Isaka

Isaka Reli

Iselamagazi

Isenye

Itigi

Kabanga

Kagunga

Kagwe

Kakonko
Kalango

Kalema

Kaliua

Kalya

Kamachumo

Kamsamba

Kanyigo

Kara

Karumwa

Kasamwa

Kasanga

Kashasha

Kasseya

Kasulo

Kasumulu

Kate

Katoro

Katumba

Katunguru

Kaunda

Kayisho

Kegonga

Kemondobay Reli

Kengeja

Kenkombyo

Kenyana

KIA

Kiabakari
Kiabalisa

Kiagata

Kibakwe

Kibara

Kibaso

Kidatu

Kigeraetuma

Kigongo Ferry

Kijingu

Kilimarondo

Kilombero

Kimali
Kimamba

Kinampanda

Kingolwira

Kingwe

Kintinku

Kipeta

Kirongwe

Kisaki

Kisanga

Kisesi

Kishanje

Kisorya

Kiwira

Kogaja

Komaswa

Konde

Korotambe

Kwamtoro

Kyerwa (Kagenyi)

Laela

Lalago

Lamadi

Lionjo

Litembo

Liuli

Lizaboni

Lugalo

Lukumbule

Lunguru

Lunguya

Lupembe

Lusewa

Lwangwa

Mabanda Mjini

Machochwe

Madaba

Madibira

Mafia
Maganzo

Magugu

Mahembe

Mahonda

Mahurunga

Mahuta

Mailimoja

Majimoto

Makanda

Makele

Makongolosi

Makuyu

Malampaka
Malangali

Malinyi

Malya

Manda

Mandawa

Mang’ula

Mangaka

Manyoni

Masumbwe

Matamba

Matarawe

Matayi

Matemanga

Matombo

Matongo

Mavota

Mbambabay

Mbarali

Mbekenyera

Mbingu

Mererani

Mfenesini

Mgambo Kigoma

Mgandu

Mgango

Mgeta

Mgololo

Migoro

Mikese

Mikindani
Mikumi

Milepa

Milola

Mingoyo
Minziro

Misasi

Mishamo

Misungwi
Mkuyuni

Mkwajuni

Mlimba

Mlowo

Morogoro Reli

Mose

Moshi Railways
Mpuyi

Msamala

Mtambile

Mtera

Mtibwa

Mtimbira

Mtimko

Mtitu

Mtomara

Mtowisa

Mtukula

Muganza

Mugeta

Mugoma

Muhange

Muhenze

Muhoro

Muhukuru

Muhutwe

Muriti

Murongo

Murusagamba

Murutunguru

Muyama

Mvomero

Mwamapalala

Mwampembe

Mwandiga

Mwese

Mwimbi

Mwanza Railway
Mzumbe

Nalasi

Namabengo

Namasi

Namtumbo

Nanga

Nanyamba

Nasa Darajani

Natta

Ndago

Ndanda

Nduguti

Negezi

Ngamu

Ngare Nanyuki
Ngarenairobi

Ngasamo

Ngerengere

Nguliati

Nguruka

Nkungi

Nshamba

Nyakabindi

Nyakahanga

Nyakahura

Nyakalilo

Nyakanazi

Nyamilembe

Nyamongo

Nyamswa

Nyang’wale

Nyangae

Nyantira

Nyumba ya Mungu

Nzela

Oldonyo Olobaiye
Oldonyo Sambu
Olmoloq

Omukariro

Paje

Panyakoo

Peramiho

Puge

Robanda

Rongai

Ruaha/Mbuyuni

Ruamchanga

Rubale

Ruhembe

Rulenge

Runazi

Runzewe

Rusumo

Rutamba

Sangamwalugesha

Sanza

Sao Hill
Sapiwi

Saragana

Sepuka

Seronera

Shelui

Sigunga

Simbo

Songea Bus Stand

Songwe

Stamico

STPU Moshi

Suguti

Sumve

Sungwizi

Tanga Railway,
Tegeruka

Turiani

Ujiji

Ukiriguru

Ukumbisiganga UlyankuluUnguja UkuuUngujaukuuUsenyaUsokeUtegiUvinza

PGO - 20

VITUO VYA POLISI VINAVYOHAMISHIKA

1.Vituo vitembeavyo vitatumika katika mikoa kulingana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa atavyoona inafaa. Vitatumika kuhusu kuimarisha nguvu katika maeneo ya pembezoni mwa miji au vijiji, au msingi wa kufanya upelelezi wa kina katika maeneo maalum.Pia katika mazingira maalum,vitatumika kama operesheni na Makao Makuu.

2.Vituo vitembeavyo kawaida vinakuwa chini ya uangalizi wa Mkaguzi wa Polisi akisaidiwa na -

Askari wa uongozi wa chini 1

Askari wa kawaida 2

Dereva 1

Askari wa simu 1

<u>Wapelelezi</u>

Askari mpelelezi wa uongozi wa chini 1

Askari mpelelezi wa kawaida 1

Askari Wang'amuzi

Askari Mng'amuzi wa kawaida 1

3.Kila kituo kitembeacho kitaongozana na askari wakikosi cha kutuliza ghasia au askari wa kawaida kwa ajili ya usindikizaji, ambao hawatapungua seksheni moja.Kikundi hichi cha usindikizaji kitakuwa kimejikamilisha na kitatumia usafiri wa Kikosi cha Kutuliza ghasia kama utakuwepo.

4.Magari ya kutosha yenye madereva yatatolewa kusafirisha askari, mahema,vitanda, vyandarua,vifaa vya kupikia na vya binafsi.Kama lazima gari la kuchukulia maji litakuwepo.Maji yatatolewa na kujazwa mara mbili kwa kila wiki.Haitaruhusiwa kwa yeyote kusafiri ndani ya gari la kituo kitembeacho.Gari la Kituo kitembeacho halitahusika na ubebaji wa vifaa vya kambi.

5.Gari la Kituo kitembeacho litabeba vifaa kwa maelekezo ya Kamanda wa Polisi Mkoa.

6.Kumbukumbu zifuatazo zitatunzwa pamoja na zingine kama itavyoelekezwa na Kamanda wa Mkoa.

a. Kitabu cha matukio PF 162, PGO 309

Kitabu kimoja cha kuhifadhia taarifa kitakachokuwa kimetolewa katika kituo cha polisi kilichopo wilayani ambapo shughuli hizi zinafanyika, kitahifadhiwa kwa mujibu wa aya 23 ya PGO 209.Kitabu hichi kitatunzwa na Kamanda wa Polisi Wilaya wakati wa kuondoka kwa kituo kitembeacho na kitabu hichi kitatunzwa hadi kituo kitembeacho kitakapokuwa kinarudi wilayani kwake.Hakikisha kuwa kituo kitembeacho hakitakuwa na kitabu chake chenyewe cha kujitegemea lakini makosa yatayotolewa taarifa yataingizwa kwenye vitabu vya kituo kikuu cha wilaya ambapo kundi kazi linafanyia kazi.Mashitaka ambayo yanatakiwa kufikishwa mahakamani au kufanyiwa uchunguzi na kituo kitembeacho yatafikishwa katika kituo kikuu cha wilaya husika kwa mujibu wa aya 22 ya PGO 309.Kesi zote ambazo zitakabidhiwa wakati wa kuondoka kituo kitembeacho kutoka wilayani zipewe nambari kwa uangalifu katika kitabu cha upelelezi cha wilaya na hatua zote zitazochukuliwa zitaorodheshwa katika kitabu cha taarifa cha kituo kitembeacho kwa mujibu wa aya 22-b – ya kanuni za jeshi za polisi 309.

b. Kitabu cha kumbukumbu cha kituo PF 51 PGO 284

Taarifa zote zitazotolewa katika kituo cha polisi kitembeacho aidha kwa njia ya mdomo au maandishi lazima ziandikwe kwa kifupi katika kitabu cha kumbukumbu cha kituo,rejea PGO 284 aya ya 4 [e pamoja na kuandikwa katika kitabu cha taarifa cha kituo kama nyongeza ya ingizo katika kitabu

cha taarifa.

c.Kitabu cha Mahabusu PF 20

Lazima kitunzwe kulingana na kitabu cha kanuni cha jeshi la polisi PGO 353.Endapo ni muhimu kuweka watu chini ya ulinzi katika kituo kitembeacho, wote watakaowekwa chini ya ulinzi wahamishiwe katika kituo cha polisi cha wilaya kwa kuwekwa ndani.Na wasiwekwe ndani wakati wa usiku katika kituo kitembeacho.

d.Kitabu cha kuhifadhi mali za Watuhumiwa PF 63

Kitatunzwa kama ilivyoelekezwa na kitabu cha kanuni za jeshi la polisi 357.

e.Kitabu cha Ukaguzi cha Maafisa PF 187

Kitatunzwa kwa mujibu wa maelekezo yaliomo kwenye PGO 303.

7.Makamanda wa Polisi wa Mikoa watatoa maelekezo kwa maandishi kwa wakaguzi dhamana wa vituo vya polisi vitembeavyo na kuweka wazi nija zinazopaswa kutumiwa nakazi za kufanywa na pamoja na kudhibiti mawasiliano ya redio.Pamoja na mazingatio mengine vituo vitembeavyo vya polisi vitaendeshwa kwa utaratibu ule ule wa kituo cha polisi cha kawaida kama itakavyowezekana.Matukio makubwa na makosa mengine taarifa zake zitashughulikiwa kama ilivyoelekezwa kwenye PGO 311.Makamanda watafanya ukaguzi wa kawaida wa vituo hivi vitembeavyo katika maeneo yao.

8.Endapo kituo kitembeacho kutoka wilayani ni muhimu taarifa zote za ung'amuzi pamoja na taarifa nyengine ambazo kwa kawaida zitalazimika kurekodiwa katika kituo cha polisi cha wilaya zitatolewa kwa afisa dhamana wa kituo.

PGO - 23

KANUNI ZA MUUNDO WA JESHI LA POLISI

1 Amri zote zitolewazo kwa jeshi kulingana na mwongozo mkuu wa jeshi la polisi(PGO) ni kwa matumizi ya jeshi la polisi tu na hayawezi kutolewa kwa raia.

2 Mwongozo wa jeshi la polisi (PGO) ni amri za kudumu zitolewazo na mkuu wa jeshi la polisi (IJP).

3 Maafisa na wakaguzi polisi wanapaswa kuuelewa vyema mwongozo huu.

4 .Makamanda wanapaswa kuhakikisha kwamba:

a) Mwongozo wa jeshi la polisi (PGO) unasisimamiwa na kufuatwa na askari wa vyeo vyote.

b)Askari wa vyeo mbalimbali (R&F)watapewa maelekezo ya kutosha juu ya mwongozo huu kwa jinsi unavyowahusu kwaq namna mbalimbali.

5 Nakala za kanuni za mwongozo wa jeshi la polisi (PGO)zitatolewa kwa maafisa na wakaguzi na kwa vituo kwa muundo ulioorodheswa hapa chini.

Polisi Makao Makuu	20
Polisi Zanzibar	100
Makao Makuu ya upelelezi wa makosa ya jinai	10
Chuo cha taaluma cha polisi moshi.	70
Kamanda wa kikosi cha kutuliza ghasia	2
Chuo cha taaluma cha polisi Zanzibar	40
Makao makuu ya polisi mikoa	20
Vituo vya polisi daraja A	10
Vituo vya polisi daraja B	10
Vituo vya polisi daraja C	5
Kikosi cha kutuliza ghasia	5

Mkuu wa chuo cha taaluma polisi Dar Es Salaam 100

Kikosi cha mawasiliano 28

6 Wakuu wote wa vituo (OCS)kwa muundo uliotolewa katika kitabu cha kanuni za jeshi la polisi(PGO) na maafisa wote waliopewa nakala za mwongozo huo,watahakikisha nakala hizo zinakwenda na wakati pindi zifanyiwapo marekebisho mbali mbali kwa amri za jeshi.

7 Marekebisho katika (PGO) yatatolewa na Inspekta Jenerali na kila rekebisho litapewa namba.Marekebisho yataingizwa katika (PGO) kwa mpangilio ufuatao.

(a)Kwa wino mwekundu kama marekebisho na mabadiliko ya maneno ni mawili au moja au namba moja au mbili.

(b)Kwa kuweka mkabala kifungu cha (PGO) kinachofanyiwa marekebisho yanayokadiriwa kuwa na aya ndefu.

(C)Kwa kuondoa ukurasa mzima katika kitabu kama marekebisho hayo ni makubwa zaidi.

(d)Kwa kila rekebisho ambalo litaandikwa kwa wino mwekundu upande wa pembeni wa sehemu inayorekebishwa na maelezo ya marekebisho pia yataonyeshwa katika rejeo la marekebisho mwishoni mwa kitabu.

8 Inspekta Jenerali kwa kadirio la muda utakavyokuwa atatoa matoleo yenye mabadiliko yote yaliyofanywa miaka mingi na matoleo mengine anayodhani ni lazima kwa utekelezaji thabiti kwa manufaa ya jeshi. Itachukuliwa kwamba mwongozo mzima wa jeshi la polisi (PGOs) ni mali ya serikali.Maafisa wanaohodhi nakala hizi binafsi watazirejesha kwa boharia mkuu pindi wanapokoma kuwepo katika utumishi wa jeshi la polisi.

AMRI ZA UTENDAJI

9 Amri za utendaji sehemu moja ni amri za muda au muda mrefu kidogo zitolewazo na Inspekta Jenerali wa polisi.

Kanuni za kudumu.

10 Kanuni za kudumu ni kanuni za muda mrefu hasa katika baadhi ya vituo vya polisi na vikosi mfano,doria za mtaa,ratiba ya doria,majengo ya biashara yenye leseni,uongozi wa serikali za mitaa n.k,marekebisho na sio marudio ya mwongozo mzuri wa jeshi ka polisi au machapisho ya maelekezo ya jeshi.Hakuna mazingira yatakayofanya kanuni za kudumu zihitilafiane na mwongozo mzima wa kanuni za jeshi la polisi PGO.

11 (a)Makamanda watahakikisha vituo na vikosi vyote vilivyo katika himaya zao zinakuwa na seti za kanuni za kudumu zinazokidhi matakwa yao ya kiutendaji.Kanuni hizo zitajulikana kama kanuni za kudumu za mkoa,Wilaya,kituo na kikosi.

(b)Kanuni za kudumu zitatolewa tu na

(1)Kamanda wa mkoa RPC au kikosi.

(11)Mkuu wa polisi wa wilaya OCD.

(111)Kamanda wa kikosi cha kutuliza ghasia

(1V)Mkurugenzi wa muziki.

12 Mkuu wa polisi wa wilaya na kikosi cha kutuliza ghasia watapeleka kanuni za kudumu zilizoandaliwa kwa kamanda wa polisi wa mkoa kwa kuthibitishwa kabla hazijatolewa kutumika ila Mkurugenzi wa muziki atazipeleka moja kwa moja kanuni hizo sehemu inayohusika.Lakini lazima kanuni zote zilizoandaliwa zinazoathiri amri nyingine zipelekwe makao makuu ya polisi kuthibitishwa kabla hazijatolewa kwa matumizi.

13 Kanuni zote za kudumu zitatolewa kwa kuandaliwa kwa lugha za kiingereza na kupewa namba na kuwekwa kwenye jalada kwa kufuata mpango wa numeral na mnyumbulisho wa vifupisho vitaandikwa kwa Kiswahili na kiingereza na kutolewa kwa mrejeo rahisi.

14 Majalada ya kanuni za kudumu yawe wazi kwa askari wa vyeo vyote ili kwa uhamisho mpya wa askari wasiofahamu kanuni za ndani ambazo sio sawa kwa vituo na vikosi vingine waweze kuzifahamu.

PGO 32

UTAWALA WA KIKOSI CHA BENDI

Utawala

1. Mkurugenzi wa muziki atakua na majukumu yafuatayo:

    a) Kusimamia mafunzo,nidhamu, ustawi na stahili mbalimbali za watumishi wa bendi na vikundi vya utamaduni.

    b) Kusimamia mavazi na vifaa kwa ajili ya matumizi ya watumishi wa bendi na vikundi vya utamaduni.

    c) Kuratibu mpangilio wa shughuli za bendi na vikundi vya utamaduni.

    d) Kusimamia mipango yote ya kiutawala inayohusiana na usafiri wa reli au barabara na maandalizi ya hati za kusafiria.

    e) Atawajibika kutunza fedha na rasilimali zote zilizopo chini ya bendi na vikosi vya utamaduni.

Bendi-Polisi Zanzibar

2. Kamishna wa Polisi Zanzibar atawajibika kusimamia nidhamu, ustawi, stahili na mavazi ya watumishi wa bendi upande wa Zanzibar.

3. Mkurugenzi wa muziki atafanya ukaguzi wa bendi kila baada ya miezi mitatu kwa kuzingatia PGO.47 na atashauri kuhusiana na masuala yanayohusiana na muziki.

4. Mkurugenzi wa muziki atakua na wajibu wa kuagiza vifaa vyote vya muziki na kubadilisha vifaa.

5. Mpangilio wa kazi binafsi za bendi unaweza kukubaliwa iwapo utaridhiwa na Kamishina wa Polisi Zanzibar. Michango na asilimia 50 ya kipato kitakachotokana na maonesho itatumwa kwa Mkurugenzi wa Muziki, ambaye ataiwasilisha kwenye mfuko wa bendi wa polisi. Asilimia 50 ilyobaki itagawanywa kwa kiwango sawa kwa wanabendi walioshiriki kwenye onesho na watasaini wakati wa kupokea.

Bendi-Chuo cha Polisi Moshi

6. Mkuu wa Chuo cha Polisi Moshi atawajibika kusimamia nidhamu, ustawi,stahili na mavazi ya watumishi wa bendi iliyopo Chuo cha Polisi Moshi.

7. Mkurugenzi wa Muziki atafanya ukaguzi wa bendi kila baada ya miezi mitatu kwa mujibu wa PGO.47 na atashauri kuhusiana na masuala yote yanayohusiana na muziki.

8. Mkurugenzi wa Muziki atawajibika kuagiza vifaa vipya vya muziki au kubadilisha vilivyopo.

9. Mpangilio wa kazi binafsi za bendi unaweza kukubaliwa iwapo utaridhiwa na Mkuu wa Chuo cha Polisi Moshi. Michango na asilimia 50 ya kipato kitakachotokana na maonesho itatumwa kwa Mkurugenzi wa Muziki, ambaye ataiwasilisha kwenye mfuko wa bendi wa polisi. Asilimia 50 ilyobaki itagawanywa kwa kiwango sawa kwa wanabendi walioshiriki kwenye onesho na watasaini wakati wa kupokea.

Mfuko wa Bendi ya Polisi

10. Kanuni zinazoongoza usimamizi,mapato na matumizi ya mfuko wa bendi wa polisi zimetajwa hapa.

11. Mfuko utajulikana kwa jina la Mfuko wa Mfuko wa Bendi wa Polisi Tanzania, na fedha zote zitawekwa kwenye akaunti ya benki iliyopo Dar es salaam.

12. Michango na mapato yatakayotokana na na maonesho mbalimbali yaliyolipwa kwa kazi binafsi za bendi zitawekwa kwenye mfuko huu kwa viwango vilivyoainishwa kwenye kanuni hizi.

13. Fedha za mfuko huu zitatumika kwa kununulia vifaa vya muziki na matumizi ya dharura yanayohusiana na bendi. Mfuko utasimamiwa na Mkurugenzi wa Muziki kwa mujibu wa kanuni hizi.

14. Mkurugenzi wa muziki:

    a) Atatunza taarifa sahihi na kwa wakati kuhusiana na;

        i. Kitabu cha akaunti cha bendi.

        ii. Kitabu cha matumizi madogo madogo (petty cash book), na

        iii. Rejista ya malipo ya wanabendi.

    b) Hapaswi kwa wakati wowote ule, kujihusisha na mkopo au makubaliano ambayo hayawezi kulipwa na na mfuko.

    c) Anaweza kuidhinisha matumizi yanayofikia Sh.50,000/- na kudhibiti akaunti ndogo isiyozidi 50,000/-

    d) Ataomba kwa Inspekta Jenerali wa Polisi ridhaa ya matumizi yote yanayozidi Sh.50,000/-

    e) Atahakikisha kwamba malipo na michango yote ya bendi inaingizwa kwenye akaunti ya mfuko wa bendi wa polisi mara moja.

    f) Atatuma stakabadhi zinazothibitisha upokeaji wa malipo au michango.

    g) Atathibitisha usahihi wa ankara zote kabla ya malipo kufanyika.

    h) Atatunza kitabu kinachoonyesha ushiriki wa wanabendi na viwango wanavyostahili kulipwa, na kutoa fedha benki na kuwalipa baada ya kusaini kulingana na viwango vyao.

    i) Atawasilisha akaunti, muktasari wa mzunguko wa fedha kwenye akaunti na stakabadhi kwa ajili ya ukaguzi wa Inspekta Jenerali wa Polisikila baada ya miezi mitatu.

Stahili na Ada za Bendi

15. Mkurugenzi wa Muziki, wakaguzi na wanabendi watalipwa stahili zao

kila mwezi kwa mujibu wa viwango vilivyoihinishwa na serikali.

16. Kwa maonesho binafsi ya bendi, malipo yatakua kama ifuatavyo:-

    a) Bendi nzima - 150,000/-

    b) Bendi ya Jazz - 100,000/-

    c) Gharama za usafiri- Isipokua pale tu ambapo itaidhinishwa na Inspekta Jenerali wa Polisi, gharama za usafiri zitafuata taratibu za serikali za kukodi magari, pale ambapo safari itakua inazidi kilomita 20 kutoka Kambi ya Polisi ya Barabara ya Kilwa, Dar es salaam, au Chuo cha Polisi Moshi au kutoka kwenye makazi ya muda ya bendi inapokua safarini.

17. Hakuna gharama zitakazotozwa kwa maonesho yoyote yatakayofanywa kwa amri ya Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, au sherehe zozote za kitaifa itakapoidhinishwa na Inspekta Jenerali wa Polisi. Gharama zitatozwa kwa maonesho binafsiyatakayohudhuriwa na Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania iwapo onesho halikufanywa kwa amri ya Raisi kama shughuli rasmi ya kiofisi.

18. Iwapo onesho litahusisha shughuli binafsi ya kijamii na waandaaji wameomba kupunguziwa gharama, maombi yao yatapelekwa kwa Inspekta Jenerali ambaye atatoa uamuzi.

19. Fedha zitakazopatikana na maonesho binafsi zitagawanywa kama ifuatavyo:-

    a) Bendi nzima

        Asilimia 50 - Mfuko wa bendi.

        Asilimia 40 - Kwa wanabendi walioshiriki (tazama k/f 22)

        Asilimia 10 - Kwa Mkurugenzi wa Muziki au Mkuu wa Kikosi cha Bendi.

    b) Bendi ya dansi

Asilimia 20 - Kwenye mfuko wa bendi

Asilimia 70 - Kwa wanabendi washiriki (kwa kiwango sawa)

Asilimia 10 - Kwa Mkurugenzi wa Muziki au Mkuu wa Kikosi cha Bendi.

20. Asilimia 40 za wanabendi walioshiriki zitagawanywa kama ifuatavyo:-

Wakaguzi - Hisa 4

Washiriki daraja la 1 - Hisa 3

Washiriki daraja la 2 - Hisa Hisa $2^{1}/_{2}$

Washiriki daraja la 3 - Hisa 3

21. Iwapo Mkurugenzi wa Muziki au Mkuu wa Kikosi cha Bendi hatakuwepo,asilimia 10 zilizoainshwa kwenye K/f. 19 (a) na (b) kitaongezwa kwenye mgao wa wanabendi alioshiriki.

22. Bendi haitaruhusiwa kufanya maonesho binafsi iwapo shughuli hio itakua inaingiliana kwa namna yoyote ile na shughuli rasmi za kiofisi.

PGO NO. 33

KITABU CHA AMRI YA KUONDOKA (PF. 58)

1. Amri ya kuondoka (PF.58) inawapa mamlaka ya kuondoka katika sehemu zao za kazi za kawaida, lazima itolewe kwa askari wote wenye cheo cha konstable wa polisi hadi Mkaguzi wa polisi ambao wanatakiwa kuondoka katika vituo vyao au vikosi vyao kwa muda au moja kwa moja kwa sababu ya

   (a) Uhamisho

   (b) Likizo

   (c) Kupangiwa kufanya kazi sehemu fulani kwa muda

   (d) Kozi maalum ya maelekezo

   (e) Kazi ya usindikizaji

   (f) Kazi nyingine zozote ambazo zitasababisha askari hao kuwa nje ya vituo vyao vya kazi au Wilaya ambazo walipangiwa isipokuwa doria za mbali ambazo zinafanyika kwa PGO namba 302.

2. Amri ya kuondoka lazima iandaliwe katika nakala mbili na itatolewa na Mkuu wa Kituo au Kikosi ambaye ataeleza wazi mambo yafuatayo: -

(a) Maelekezo yanayohusu safari ikiwa ni pamoja na njia itakayotumika.
(b) Mshahara pamoja na posho kwenda likizo au uhamisho kwa mujibu aya ya 33 na 34 ya PGO namba 48.
(c) Kiasi cha posho ya safari anachostahili kupewa afisa muhsika pia na marupurupu mengine ambayo afisa huyu anayategemea toka kwa maafisa hao wawapo safarini au mwisho wa safari.
(d) Chini ya kichwa cha habari "maelezo kwa undani" uzito wa mizingo ya afisa huyo anayehama moja kwa moja na
(e) Stahili za safari za afisa huyo endapo familia yake itakuwa imetangulia kwenda likizo pale itakapoonekana ni vigumu kupata hati ya usafiri ya kurudia kwa ajili yao kabla afisa huyo hajaoondoka kwenda likizo.

3. Hati ya Amri ya kuondoka itatolewa moja tu kwa maafisa wa polisi ambao watakuwa katika safari moja ya kikazi lakini majina ya wahusika yataingizwa katika fomu hiyo ambayo ni PF. 58.

4. Maofisa wa polisi wanaosafiri chini ya mamlaka ya amri ya hati ya kusafiria watafanya yafuatayo:

(a) Onyesha hati ya amri ya kondoka kwa kiongozi wa juu itakapotakiwa na kiongozi wa juu.
(b) Wataripoti kituo cha polisi (kama kipo) katika maeneo yote watakayosafiri (kupitia) na kupata sahihi ya mkuu wa kituo katika hati yao ya amri ya kusafiria.
(c) Kuomba afisa yeyote wa serikali wanakoripoti kuhusiana na kazi

yao kuweka sahihi katika hati ya amri ya kuondoka na

(d) Kuripoti kwa Mkuu wa Kituo au kikosi, bila kuchelewa mara wanapokuwa wamefika mwisho wa safari yao na kukabidhi hati ya amri ya kuondokea.

5. Mkuu wa kituo au kikosi ambako askari hao wameripoti kwa mujibu wa aya ya na 4(d) . Atafanya yafuatayo:-

(a) Atarekodi muda sahihi wa kufika ndani ya hati ya amri ya kuondokea na katika kitabu cha kumbukumbu kituoni.

(b) Atafanya uchunguzi kama kuna uchelewaji katika safari yao.

(c) Atachukua na kuihifadhi iwapo safari iliyokusudiwa imekamilka, na

(d) Atawarudishia hati ya amri ya kuondokea kama safari haijakamilika na atatoa maelekezo sahihi jinsi ya kuendelea na safari hiyo.

6. Hati ya amri ya kuondokea ya afisa aliyepangiwa kazi ya muda usiozidi siku 28 itahidadhiwa na mkuu wa kituo au kikosi na kuitoa tena wakati wa kuondoka ikiwa imesainiwa wakati afisa anaporudi katika kituo chake cha kudumu.

7. Mkuu wa kikosi atatunza hazi hizo za amri ya kuondoka kwa muda wa miezi 6 baadaye ataziharibu.

PGO - 34

VITABU – KITABU CHA TAARIFA ZA WAGONJWA

1. Kitabu cha taarifa za wagonjwa (PF- kitatunzwa katika kituo cha polisi ambacho kitakuwa na mambo muhimu yafuatayo:

   (a) Tarehe
   (b) Namba na jina la mkaguzi au askari wengine wa vyeo mbalimbali kuanzia Konstable wa polisi hadi RSM wanaotaarifu kuugua.
   (c) Aina ya ugonjwa.
   (d) Idadi ya siku alizotumia hospitali.
   (e) Idadi ya siku za likizo ya ugonjwa.
   (f) Idadi ya siku za mapunziko.
   (g) Idadi ya siku kufanya kazi nyepesi.

2. Kila mkaguzi na askari wengine wa vyeo mbalimbali kuanzia konsteble wa polisi hadi RSM atapewa kitabu cha historia ya matibabu ya wagonjwa (PF.31C) kwa siku atakayopangiwa kuonna na daktari

3. Vitabu vya historia ya matibabu ya wagonjwa vitatunzwa na mkuu wa kituo au kikosi atakayekuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba vitabu hivyo vitatunzwa kwa mujibu wa utaratibu huu.

4. Inapotokea muhusika anatoa taarifa za ugonjwa atapewa kitabu chake cha taarifa za matibabu ya mgonjwa na ataelekezwa kukitoa kwa daktari au Clinic atakayohudhuria ambapo taarifa kuhusiana na ugonjwa unaohitaji kulazwa au likizo ya ugonjwa zitarekodiwa. Atarudisha kitabu kwa Mkuu wa Kituo haraka iwezekanavyo.

5. Mkuu wa kituo atakamilisha taarifa katika rejista ya wagonjwa ambazo atazitoa katika kitabu cha historia ya matibabu ya mgonjwa husika.

6. Kitabu cha historia ya matibabu ya mgonjwa atakwenda nacho anapokwenda uhamisho, kitapelekwa Makao ya Polisi andepo muhusika atakuwa ameachishwa kazi

PGO NO 35

VITABU VYA REGISTA

1. Vitabu na regista zote za polisi zilizokamilika (fanyiwa kazi) isipokuwa tu

(a) Vitabu uhasibu ,kumbukumbu za stoo, ambazo ni lazima vitunzwe kwa mujibu wa kanuni namba 140 ya kanuni ya fedha za umma.

(b) Vitabu maalum vya ofisi ambayo ni lazima vitunzwe kwa muda maalum chini ya kifungu maalum cha PGO ni lazima viharibiwe baada ya miaka miwili baada ya ingizo la mwisho la ukurasa wa mwisho.

2. Uharibifu huo katika hali yoyote ni lazima uidhinishwe na Gazetted Officer. Vitabu na regista ambavyo vipo tayari kwa ajili ya kuharibiwa vitatolewa kwa ajili ya Ukaguzi na Gazetted Officer atahakikisha zile zisizohijika hazihifadhiwi.

PGO - 36

HATI YA MAKABIDHAINAO NA MAPOKEZI

2. Afisa anayepokea atakuwa makini kwenye makabidhiano ya anayeondoka na atachukua hatua zote muhimu kuhakikisha kuna muendelezo wa sera na hatua za utawala

KITENDO CHA KUKABIDHIWA NA KUPOKEA

3. Afisa anayekuja kwa kawaida atapokea eneo la Makao Makuu la

himaya . Lakini kama kuna mabadiliko yeyote katika mipango ambapo fedha za serikali au stoo vinahusika mpangilio wa makabidhiano hayo utafanyika kulingana na sehemu ya Xiii (d) na kanuni 248 – 249) ya kanuni ya fedha za umma.

4. Makabidhiano ya vituo vyote na mipango mingine lazima visimamiwe na (ofisa) kutoka Makao Maku ya Mkoa ambaye atashuhudia kutiwa sahihi kwa hati ya makabidhiano na yeyey ataweka sahihi yake katika hatia hiyo.

5. Utaratibu wa maandalizi ya hati ya makabidhiano, ulioandliwa katika haya zifuatazo hautatumika katika kikosi cha intelejensia, ambacho kitakuwa kinafuata utaratibu wa makabidhiano wa kanuni za muda za Mkurugenzi wa Upelelezi wa Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

6. Baada ya kukamilisha makabidhiano hati (… …….hati halisi Tf 153 na Sf 17), ambayo injitokeza katika ambatanisho " A" na "B"cha PGO hii na PF. 168 inayojitokeza katika kitabu kinachotunza mali za serikali, itakamilishwa na maafisa wahusika.

7. Wakati Makao Makuu ya Mkoa au Makao Makuu ya himaya yeyote inapokabidhi nakala tatu za hati ya makabidhiano zitaandaliwa na nakala mbili zitapelekwa Makao Makuu ya Polisi

8. Wakati kituo cha polisi na himaya nyingine za Mkoa zinapokabidhi, hati za makabidhiano zitaandaliwa katika nakala nne, na nakala tatu zitapelekwa Makao Makuu ya Mkoa. Kamanda wa mkoa atabaki na nakala moja na nakala mbili zilizo baki atazipeleka Makao Makuu.

9. Hati lazima zikamilishwe vizuri na hakuna lazima ijazwe katika sehemu yakukabidhi au kupokea ambayo haijakamilika katika kituo husika mfano kifungu kinachohusika na fedha na stempu katika kituo ambacho vitu hivyo havitumiki.

10. Hati ambayo ipo kwenye fomu ambayo inaonyeshwa kiambatanisho “C” litakamilishwa kwa utaratibu wa majalada ya siri na hati ya kupeleka kwa kuyatenganisha, kutokana na aina ya siri. Mgawanyo unaohitajika ni sawa na ule wa hati za makabidhiano na mapokezi, isipokuwa Makao Makuu ya Polisi itahitaji nakala moja tu

11. Mapungufu yote na upotevu wa mali za serikali lazima yaingizwe kwenye hati. Afisa yeyote atakayekataa kutia sahihi kwenye kutokana na kutoridhika na hati ya makabidhiano atalazimika kutoa taarifa kwa kamanda wake.

Ukaguzi baada ya kukabidhiwa

12. Afisa anayekabidhwia haraka iwezekanavyo baada ya kupokea, atakagua vituo vyote chini ya himaya yake. Atafanya juhudi za kuzifahamu kanuni zote zinazotawala vituo husika, kwa kuzirudia kadri mazingra yatakavyoruhusu.

KIAMBATANISHO “A”

(KWA PGO NAMBA 36)

TFN 153

TANZANIA

……KITUO

Maelezo ya makabidhiano ya :……..

Wizara/Idara/Kituo tarehe:…….

Fedha taslim		Sh	Sent
Noti			
Sarafu			
Hundi			
Salio katika benki kwa mujibu wa taarifa ya benki			
Hundi zinzodaiwa		Sh	sent
“Kodi” stempu (kama iliyoanishwa katika regista			
Stempu za mapato kama ilivyoainishwa katika regista			
Karatasi ya mapambo (Kama ilivyoainishwa katika rejista			
Vitabu vya mapato (kama ilivyoanishwa kwenye vitabu vya marejesho ya mapato			
	Namba zilizojadiliw	Idadi ya vipande	uzito

	a		
Pembe (kama ilivyoainishwa katika rejista			
(a) Ndovu			
(b) Kiboko			
Pembe za faru			
Ngozi za wanayama pori (fafanua aina)			
Mifugo (kama iliyoainishwa katika marejesho ya kiambatanisho Mifungo			
Kasiki, vyumba imara, makasha ya fedha (chuma na mbao) funguo.			
Aina na ukubwa wa kasiki n.k	Namba ya mtengenezaji wa kasiki n.k	Namba ya mtengenezaji wa funguo n.k	Mahali funguo ya akiba inatunzwa.
Maelekezo ya kifedha n.k.			Idadi ya nakala
Kanuni za serikali ……..			
Kanuni za fedha, sehemu ya I…….			
Kanuni za fedha, sehemu II …….			
Kanuni za fedha, sehemu ya III…….			
Kanuni za Jumla ……..			
Sheria ya Tanzania (Seti)			

Muongozo wa hazina
Mali, samani n.k (kama ilivyofafanuliwa kwenye regista)
Fomu ya mali namba 17 imekamilika (imejazwa)

Kitabu cha kasma ya Idara.

Ninathibitisha kwamba nimekabidhi kitabu cha kasma cha Idara kilichjazwa kikamilifu kwa tarehe husika na kwamba kinaonyesha wzi kiwango halisi cha matumizi sambamba na kasma au kasma za Idar yangu pia matumizi yaliyoidhinishwa kutumika kwa mujibu wa …… Kanuni Na. 236

…… Sahihi ya } Afisa anayekabidhiwa

……cheo }

Nimepokea kitabu cha kasima cha Idara

…… Sahihi ya } Afisa anayekabidhiwa

……cheo }

Kwa pamoja tunathibitisha kwamba tumekabidhi na tumepokea fedha taslimu, stempu, vitabu vya mapato, kasisi, vifaa n.k. kama ilivyoonyeshwa hapo juu na kwamba kiasi kinacholingana na salio kama inavyoonyehwa kwenye vitabu mbalimbali vya kihasibu , rejista n.k.

* Isipokuwa vitu vilivyotolewa maelezo kwenye kiambatanisho ambacho afisa anayekabidhi ametoa …….. 201` ……..

Sahihi ya afisa anayekabidhi

……..201……

Sahihi ya afisa anayekabidhiwa

* Futa kama haihitajiki.

Angalizo: Nakala ya hii hati ya makabidhiano itumwe kwa Afisa msimamizi wa fedha za serikali wa Wizara /Idara na Mkurugenzi wa ukaguzi na nakala moja ibaki kwenye ifisi husika.

KIAMBATANISHO “B”

MALI

Hati ya makabidhiano ya (S.F, 17)

……..Idara ……za…….. kituo

Mimi nathibitisha kwamba leo nimemkabidhi bwana:……. ya …….Idara/Wilaya, baada ya kulinganisha mali halisi zilizoko stoo na idaid ya mali ilyoko kwenye leja na kuona kwamba zinalingana, sahihi na ziko kwenye mapangilio; sahihi isipokuwa vitu vilivyoorodheshwa katika jedwali linaloonyesha mapungufu.

…….

Saini ya Afisa anayekabidhiwa

Kwa: ……..

……..

……

KIAMBATANISHO “C”

(CHA PGO NAMBA 36)

SIRI:

HATI YA KUKABIDHI NA KUPOKEA NYARAKA ZA SIRI

…….. Kituo

Mimi nithibitisha kwamba leo nimemkabidhi bwana:…… majalada na nyaraka za siri zolitajwa :-

Madaraka…….

Kumb Na:…….

……..201

Saini ya afisa anayekabidhi

Mimi nathibitisha kwamba leo nimepokea majalada ya siri na nyaraka zilizotajwa hapo juu, nimesoma maelekezo yaliyomo katika maelekezo ya Ualama ya Serikari.

…….

Saini ya afisa anayekabidhiwa ……201.

PGO - 37

SIFA NA ZAWADI

1. Wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali watakaofanya kazi zenye sifa za upekee/sifa za kipekee(sio za kazi za kawaida) wanaweza kupendekezwa: -

   (a) Kupata tuzo kutoka kwa Mheshimiwa Rais;

   (b) Kupata tuzo kutoka kwa Inspekta Jenerali wa Polisi.

2. Tuzo ya fedha yaweza kutolewa kwa nyongeza ya sifa iliyotolewa na Rais au Inspekta Jenerali waPolisi.

3. Mapendekezo kutoka kwa wakuu wa kamandi au vikosi watatuma nakala ya mapendekezo kwa Inspekta Jenerali wa Polisi wakiambatanisha na kifani chenye sababu ya mapendekezo hayo vikiwa ndani ya jalada husika.

4. Mapendekezo kwa maafisa waliokataa kupokea rushwa pamoja na thamani ya rushwa iliyotaka kupokelewa pamoja na taarifa za mashtaka za mtoa rushwa.

5. Afisa Mnadhimu anawajibika kuandaa na kutuma mapendekezo kupitia fomu ya polisi namba 159 na 160 na kuyatangaza mapendekezo hayo katika utaratibu wa kijeshi, sehemu ya kwanza

mapendekezo yote yatasainiwa na Inspekta Jenerali wa Polisi.

6. Fomu za mapendekezo zitakabidhiwa kwa wapokeaji kwa gwaride na wakuu wa kamandi.

7 Mapendekezo yote yataingizwa kwenye vitabu vya kumbukumbu vya Utumishi kwa wino mwekundu.

8. Mapendekezo yasiyokuwa ya kiofisi yanayotolewa na Mahakama au wananchi ambayo hayakidhi mapendekezo ya kiofisi yaweza kuwasilishwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa taarifa na kumbukumbu.

Kiambatanisho “A”

(Kwa P.G.O. Na. 37)

MAPENDEKEZO KWASIFA NA/AU ZAWADI

Na. Cheo Jina Kituo Mkoa	Maelezo mafupi ya kumbukumbu mfano mpelelezi makini na mvumilivu kwa kesi ya wizi wa mali yenye thamani ya Tshs 2,000,000/=alisababisha kupatikana kwa mali na kukamatwa kwa watuhumiwa wanne(4) hatimae kufungwa.	Mapendekezo ..... Mkuu wa Kituo Tarehe: .....
	MAELEZO 1 Februari, 2004, n.k., n.k. Endelea na ukurasa unaofuata kama kuna ulazima wa kufanya hivyo:	..... Kamanda wa Polisi wa Mkoa Tarehe: .... Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai *Tarehe:* .... Maamuzi ya Inspekta Jenerali

		Tarehe*:* .... Inspekta Jenerali Tarehe: .....

PGO - 38

MAWASILIANO YA SIRI YA KIMAANDISHI – YALIYOAINISHWA

1. Utaratibu huu wa kipolisi umetangazwa kuwa mwongozo rahisi kwa maelekezo ya Serikali kiusalama na Taasisi za kijeshi(nyaraka za siri za Inspekta Jenerali wa Polisi nama 19 “Maelekezo ya utunzaji wa nyaraka za siri na mawasiliano yake) Wahusika katika kutunza nyaraka hizo za siri wawe na ujuzi kamilifu wa maelekezo yanayohusika na nyaraka hizo. Wasiohusika na kazi hiyo wanatakiwa kuwajulisha wakubwa wao kwa maelekezo yanayostahiki.

Mgawanyo wa kiusalama

2 Kuna aina nne za mgawanyo wa kiusalama ndani ya Jeshi la Polisi, ambao ni: -

(a) Siri sana.

(b) Siri.

(c) Yenye kuamini mno

(d) Kwa matumizi ya polisi tu.

Kwa nyongeza, mgawanyo huu unatakiwa utumike ndani ya Jeshi la polisi pekee, na inapobidi kutolewa nje yawe na mwongozo maalum vinginevyo yaweza kuleta madhara au ugumu wa kiutawala.

3. Mawasiliano ya kimaandishi kutoka taasisi za nje yanaweza kuchukuliwa kuwa yenye masharti

Alama za mgawanyo wa mawasiliano ya kimaandishi

4. Mgawanyo wa hati unaweza ukaandikwa na kugongwa muhuri kwa wino mwekundu juu na chini ya kila ukurasa. Mgawanyo huo lazima tu uchapishwe au uandikwe kwa mkono kama hakuna nyenzo zingine zilizopo, na alama hizo ziwe za wino mwekundu.

5. Hati za siri haziwezi kubadilishwa bila mamlaka ya ofisi iliyotoa hati hiyo.

Kuhifadhi nyaraka

6. Hati za siri zitahifadhiwa kwenye majalada kulingana na mgawanyo wa nyaraka husika. Juu ya jalada la nyaraka za siri kutakuwa na alama na namba ya kumbukumbu vinginevyo kuwepo na majalada yanayoonyehs utofauti kati ya jalada moja na linguine kwa mgawanyo ufuatao: -

SIRI SANA: Nyekundu yenye 1” ufito mweusi kwenye mgongo wa jalada.

SIRI: Kijani yenye 1” ufito mwekundu kwenye mgongo wa jalada and diagonal red band.

YAKUAMINIKA MNO: Bluu yenye 1” ufito wa zambarau kwenye mgogo wa jalada.

7. Kichwa cha habari cha jalada la siri hakitawekwa nje ya jalada la siri bali litaonyeshwa ndani kwenye ukurasa wa mbele.

8. Jalada la siri sana litakuwa na muhtasari upande wa kushoto wa jalada likitaja folio zote zilizopo ndani ya jalada.

Uwajibikaji wa usalama wa hati

9. Mwandaaji wa hati anawajibika kwa usalama wa hati kimamlaka. Wapokeaji wanawajibika kuhakikisha utunzaji wa hati kwa kipindi kilichoainishwa sio chini ya mara moja kwa mwaka. Mfano wa kawaida wa uwajibikaji katika utunzaji wa hati ni maandishi ya kimafumbo na alama za siri zinazotumika ndani ya Jeshi la polisi.

Usajili wa nyaraka zinazoingia na kutoka

10. Jalada tofauti la hati zinazoingia na kutoka la mawasiliano ya siri litatunzwa kulingana na mgawanyo wa nyaraka. Alama za tofauti zitawekwa kulingana na kifungu kinachohusika na nyaraka hizo. Mara nyingi ni lazima kutunza alama hizo kwenye daftari la kumbukumbu la nyaraka za mawasiliano ya siri, lakini ikumbukwe kwamba alama za kumbukumbu zihifadhiwe kwa usiri wa hali ya juu.

Usalama wa vitu vya siri

11 Afisa mtunza nyaraka za siri atawajibika kwa usalama wa nyaraka hizo zikiwa mikononi mwake na kuhakikisha kuwa hazifikiwi na wasioidhinishwa.

12. Kwa namna yoyote ile nyaraka za siri haziruhusiwi kupelekwa katika nyumba binafsi n.k, isipokuwa kama kuna mwongozo wa kufanya hivyo na kuwe na kibali cha Inspekta Jenerali wa Polisi kwa kitendo hicho.

13. Majalada ya nyaraka za siri yasiachwe bila uangalizi kwa muda wowote ule vinginevyo yafungiwe kama ilivyoelekezwa katika kipengele cha 14 cha mwongozo huo.

Kiasi cha wastani cha utunzaji wa hati za siri

14. Yafuatayo ni masharti yanayotakiwa katika utunzaji wa nyaraka za siri: -

Asili ya kitu	Kama yakihifadhiwa katika mazingira yasiyo salama	Kama yakihifadhiwa katika mazingira salama
SIRI SANA na alama zote za siri na vitu vya mafumbo.	Kasha la chuma lililojengewa matofali.	Kasha la chuma.
SIRI	Kabati la chuma lililojengewa matofali na kuchomewa nondo za usalama na kufuli madhubuti.	Kabati la chuma la majalada
YAKUAMINIKA MNO	Kabati la chuma la majalada lenye nondo na kufuli	Kabati la chuma la majalada.

15 Kwa lengo la kiwango cha chini cha utunzaji “eneo salama” litafsiriwe kwamba ni chumba imara chenye mlango wa chuma na kufuli imara au jengo lenye walinzi.

Utunzaji na makabidhiano ya hati za siri

16 Wakati wa kubadilishana eneo la utunzaji wa hati za siri, maofisa wote wawili anayeingia na anayetoka watakagua majalada yote na hati zilizomo kama ifuattavyo: -

(a) Majalada yote yataangaliwa kulingana na vielelezo husika.

(b) Madhumuni yatachunguzwa na kuangaliwa na maafisa wote wawili. Wote wawili wakiridhika na maudhui ya majalada hayo kuwa ni sawa, wataandika tarehe na ufupisho wa folio ya mwisho na muda waliokagua.

(c) Hati ya makabidhiano itasainiwa kwa mujibu wa utaratibu na kushughulikiwa kama ilivyoainishwa na P.G.O namba 36.

Usambazaji wa vitu vya siri

17. Utaratibu kamili wa usambazaji wa nyaraka za siri umetajwa/umeainishwa katika waraka wa siri wa Inspekta Jenerali wa

Polisi namba 19 “Maelekezo ya utunzaji wa mawasiliano wa hati za siri” yaliyotolewa kwa maofisa wote waliotangazwa kwenye gazeti la Serikali, lakini kwa lengo la mwongozo huu maelekezo yafuatayo lazima yazingatiwe: -

(a) SIRI SANA: Yasitumwe vinginevyo zaidi ya kutumia mfuko maalum wa kusafirishia au yapelekwe kwa mkono na afisa aliyeidhinishwa kufikia vitu vya siri.

(b) SIRI: Kwa barua iliyosajiliwa na iwekwe ndani ya bahasha mbili(angalia kipengele cha 18 na 19 cha mwongozo huu), au na afisa aliyeidhinishwa kufikia vitu vya siri.

(c) YAKUAMINIWA MNO: Kwa barua iliyosajiliwa au kwa mkono na afisa aliyeidhinishwa kufikia vitu vya siri.

Bahasha mbili

18. Bahasha ya ndani itakuwa na anuani ya inakotumwa na jalada lenye kumbukumbu na maudhui, pamoja na tarehe upande wa chini kwenye kona ya kushoto. Mgawanyo wa kiusalama utakuwa umegongwa muhuri unaoonekana vizuri pande zote za bahasha. Bahasha lazima ifungwe kulingana na mgawanyo wa maudhui.

19. Bahasha ya nje itakuwa tu na anuani ya inakokwenda na itafungwa kwa gundi tu kama itakuwa kwa njia ya barua. Hakuna mgawanyo wa kiusalama au kumbukumbu ya jalada itakayoonyeshwa kwenye bahasha ya nje.

20. Kuna aina mbili za ufungaji zinazoweza kutumika kufungia hati za siri:

(a) Vifunguo vya usalama vya shaba nyeupe

Hizi hutumika kwa kugonga kwenye rakili ambayo hutumika kufungia bahasha na aina ya hati zote za siri wakati haitumiki itahifad.hiwa kwenye kasha.

(b) Kifungio chenye karatasi nyekundu

Hii itagongwa muhuri na ofisi iliyotoa hati ya siri au kusainiwa na afisa msambazaji. Muhuri huo au saini utazuiliwa na utepe ambao utazidi kila upande wa bahasha japo kwa nchi moja. Utepe huo utatumika tu kufungia bahasha ya ndani au bahasha moja yenye hati za siri, bahasha iliyo na vitu vya kuaminika mno. Vitu vya siri sana havitafungwa kwa njia hii..

Opokeaji wa Hati za Siri

21. Kwa kila tukio wakati wa kusambaza hati za siri sana na zile za siri, Afisa msambazaji atahakikisha kwamba amejaza (fomu 38) na

ataambatanisha hati zenye saini na kurudishwa ilipotoka.

22. Kwa Afisa mtumiwa ambae atakuwa amemwachia/amekasimu madaraka ana jukumu la kuhakikisha maudhui na taarifa wakati wa upokeaji, kama yako sawa, atasaini na kurudisha stakabadhi kwa Afisa msambazaji bila kukawia.

23 Afisa mtumaji atakapopokea stakabadhi ataweka nakala kwenye jalada.

24. Ni wajibu wa afisa mpokeaji kuhakikisha kwamba vifungio vya bahasha yenye nyaraka za siri havionyeshi kuharibiwa.

Uvunjaji wa Usalama:

25 Mashaka yoyote yanayoambatana na uharibifu wa hati za siri yatatolewa taarifa haraka kwa ofisa mkubwa aliyepo.Upepelezi utaanza wakati huohuo.

26. Kama bahasha au vibebeo vya hati ya mawasiliano ya siri kama vitaonekana kuharibiwa au kuonekana kutokukubalika wakati wa upokeaji kwa mujibu wa FP.38, afisa mpokeaji ana waajibu wa kumjulisha afisa msambazaji kwa njia yeyote ya haraka. Maafisa wote wawili wataanza uchunguzi mara moja, na kwa nyongeza afisa mkubwa aliyepo ajulishwe.

PGO - 39

UTARATIBU WA MAWASILIANO

1. Mawasiliano yote ya kikazi na ishara zote kwa Makao Makuu ya Polisi yataelekezwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi.

2. Maafisa waote waliotangazwa kwenye gazeti la serikali waliopo Makao Makuu ya Polisi watasaini mawasiliano yote yanayotoka nje ya idara “Kwa Inspekta Jenerali wa PolSisi”.

3 Mawasiliano yanayotumwa kwa Makatibu Wakuu na wakuu wa idara za serikali yatasainiwa : kwa niaba ya Inspekta Jenerali wa Polisi”. Kamishna(Utawala na Fedha), Kamishna(Operasheni na mafunzo), Manaibu Kamishna(Makao Makuu ya Polisi) Makamishna wasaidizi waandamizi(Makao Makuu ya Polisi), Makamishna wasaidizi(.Makao Makuu ya Polisi), Maafisa Wanadhimu(Makao Makuu ya Polisi) na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai ndio maafisa pekee walioidhinishwa kwa niaba ya Inspekta Jenerali wa Polisi.

4. Mawasiliano yote kutoka Makao Makuu ya Polisi yanatakiwa yarudishwe majibu Makao Makuu ya Polisi ndani ya siku kumi 10 tangu yalipopokelewa vinginevyo iwe imeelekezwa. Afisa yeyote ambaye hataweza kukamilisha ndani ya siku kumi 10 atajulisha Makao Makuu ya Polisi kwa kibali cha kuchelewa kujibu na ataeleza sababu za kuchelewa.

5. Makao Makuu ya Polisi watapokea kukiri upokeaji kwa namna ya mawasiliano yoyote ya haraka ndani ya masaa 24 ya kumbusho..

6. Maombi ya kimaandishi kwa Makao Makuu ya Polisi ya maamuzi kuhusu maelekezo yatahusisha taarifa zote, maamuzi ya nyuma, kama yapo, namba za kumbukumbu za jalada na itatolewa taarifa ya kutosha ili Polisi Makao Makuu watoe maamuzi kuhusu uwezo wa vitu vilivyotolewa..

7. Maafisa hawaruhusiwi kuwaandikia wakuu wa idara za serikali moja kwa moja katika masuala ya kikazi. Mawasiliano yote ya aina hiyo yatumwe kupitia kwa Inspekta Jenerali wa polisi, isipokuwa makamanda wa mikoa wanaweza kuwaandikia wakuu wa mikoa moja kwa moja katika utendaji wa kawaida na watamjulisha Inspekta Jenerali wa Polisi yenye umuhimu yaliyojiri kutokana na mawasiliano hayo. Maombi ya kimaandishi yenye ushauri wa kisheria kutoka kwa Mkurugenzi wa Waendesha Mashtaka yatatumwa kupitia kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai. Mawasiliano mengine yakiwemo ya alama zinazotumwa kwenda Jeshi la Polisi za himaya ya nchi nyingine zitapitia Makao Makuu ya Polisi Dar es Salaam. Kwa

mikoa inayopakana na himaya nyingine mawasiliano ya moja kwa moja yataruhusiwa katika maswala ya dharura, kuwapata wakosaji watoro, na maombi ya ukaguzi wa barabara na vitumiavyo barabara. Wakati mawasiliano hayo yanafanyika nakala zitatumwa Makao Makuu kwa taarifa.

8. Mawasiliano yote yanayokwenda au kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yanayohusiana na vocha, stakabadhi na hati zinazoambatana yatapitia Makao Makuu ya Polisi. Mawasiliano ya makamanda na Wizara ni marufuku, vinginevyo iidhinishwe na Inspekta Jenerali wa Polisi.

Kanuni za mawasiliano mbalimbali

9. Kila taarifa na muhtasari utakuwa na tarehe, mamlaka ya mwandishi au cheo baada ya saini yake. Mada kwenye chanzo cha mawasiliano lazima izingatiwe katika mawasiliano yote yanayofuata..

10. Kila taarifa itahusika na mada moja tu. Taarifa yenye mada nyingi hairuhusiwi.

11. Kila majibu ya taarifa au muhtasari utashughulikiwa kwa kila kilichotajwa na hati ya awali na kwa mpangilio wa kila hoja kama ilivyotajwa.

12. Nakala ya kila taarifa ya kiofisi au barua yatatunzwa kwenye jalada katika ofisi ya kituo ilikotoka taarifa ya awali.

13. Ucheleweshwaji usio wa lazima kujibu mawasiliano hauruhusiwi.

14. Mawasiliano yote kutoka kwa wananchi yatatambuliwa rasmi kwa tarehe ya kupokea kama majibu kamilifu au majibu ya mara moja hayawezi kutumwa.

16. Karatasi na fomu zilizotolewa kwa matumizi ya kazi zitatumika kwa uangalifu mkubwa, uharibifu usio wa lazima uzuiwe. Makamanda wa mkoa watakagua uwepo wa vifaa vya kuandikia vinavyotolewa vituoni, katika vituo vyote vilivyo chini yao na kuhakikisha hakuna matumizi ya kuzidi. Matumizi ya vifaa vya serikali ni marufuku kwa matumizi binafsi.

17. Barua zote zisizo na anuani maalum zitahifadhiwa na kutumwa kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kama kuna umuhimu.

18. Kila ombi, taarifa au matakwa yatakayotumwa kwa afisa mwandamizi yataambatana na muhtasari wa taarifa kutoka kwa afisa anayetuma. Maelekezo haya ni maalum kwa vitu vinavyotumwa Makao Makuu.

19. Askari wa vyeo mbalimbali wanaotaka kuwasiliana na Inspekta

Jenerali wa Polisi wanaweza kufanya hivyo lakini tu kwa kupitia makamanda wao. Maombi yanayoelekezwa moja kwa moja Makao Makuu ya Polisi hayatakubalika. Makamanda husika watawasilisha mawasiliano yote kwa Inspekta Jenerali wa polisi yakiwa na maoni yanayohusiana na maombi yenyewe.

Mfumo wa kuhifadhi hati jaladani

20 Makamanda watahakikisha kwamba makao makuu na wote waliochini yao na vituo vikihusisha ngazi ya wilaya, wanazingatia mfumo maalum wa utunzaji wa hati majaladani kama ilivyoainishwa na P.G.O.

21. Vituo vya daraja "C" havitakiwi kufuata mfumo huu. Watazingatia majalada ya pekee kwa barua zilizopokelewa na nakala za barua zilizosambazwa.

22. Majalada yote yaliyopo vituo vipya yatakaguliwa na afisa aliyetangazwa na gazeti la serikali katika ukaguzi rasmi na hati za zamani na makaratasi machakavu na yasiyotumika yataharibiwa. Uhifadhi wa kumbukumbu zisizo na thamani hautakiwi.

23. Tarehe ya kupokelewa itandikwa juu mbele ya ukurasa wa mawasiliano yanayoingia

24 Mawasiliano yote yanayotoka (isipokuwa siri ya kuaminika mno) kwa anuani moja yatatumwa kwa pamoja kwenye bahasha moja. Matumizi ya bahasha moja moja kwa kila mawasiliano hayaruhusiwi.

25. Kama mfumo wa kutuma hati nyingi utatumika, mawasiliano tofauti na siri yatafikishwa kwa kusambazwa kulingana na taratibu zinazotumika kwa kila kituo kama hakuna mfumo wa utumaji wa hati nyingi barua zitawekwa stampu na kutumwa kwa njia ya posta.

26. Barua pepe kama chombo cha mawasiliano inaruhusiwa kwa masharti kulingana na sera na miongozo inayotolewa na Inspekta Jenerali wa Polisi mara kwa mara.

PGO - 40

IDARA YA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI

UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

1 Kumbukumbu za makosa ya jinai zitatunzwa na vikosi vya upelelezi wa makosa ya jinai vya wilaya na mikoa kwa kufuata utaratibu uliopo katika (Kanuni za kudumu za Jeshi la Polisi) mwongozo huu na hakuna kumbukumbu wala daftari litakalofunguliwa tofauti na maelekezo yalitolewa na Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi hii au nyingine.

Majalada ya kutunza kumbukumbu za watu waliochini ya uangalizi n.k

2. Soma P.G.O. Na. 358

Majalada ya kutunza kumbukumbu za wahalifu sugu

4. Majengo, samani.miundombinu ya maji na umeme,silaha ,vifaa , mali za kituo na masanduku ya kutunzia mali za kituo lazima

viwekwe katika sehemu ya wazi wakati wa ukaguzi na maafisa wahakikishe viko katika hali ya usafi. .

5. Kambi za askari wa vyeo vya chini lazima ziwe safi.Samani na mali binafsi lazima vipangwe katika hali ya usafi ndani ya kila kambi na visitolewe na kupelekwa kokote.Familia za kambini zinatakiwa kuwa kimya na kwa utulivu hadi afisa mkaguzi atakapopita.Wake na wachumba wasio rasmi hawatakiwa kuwepo kambini wakati wa ukaguzi.

6 Silaha zote, risasi na mali za kituo zilizoorodheshwa kwenye kitabu cha mali za kudumu za kituo(PF 168) lazima zipangwe sehemu moja kwa ajili ya ukaguzi.Risasi lazima zipangwe katika mafungu ya makumi ili kurahisisha ukaguzi. Kasoro yoyote lazima ionyeshwe wazi.

7. Magari yote yatapangwa katika mstari mmoja na kila dereva atasimama mbele ya gari lake kwa ukaguzi.Boneti za magari yote lazima ziwe wazi kwa kurahisisha ukaguzi wa injini. Nati zinazofunga betrii zifunguliwe na ziwekwe juu ya betrii bila kufungwa.

8. (a) Sanduku la vifaa litawekwa nje kwenye veranda ya kila askari anaeishi kambini na kama hamna veranda liwekwenye sakafu sambamba na mlango wa nyumba anayoishi askari. Askari ambae hata kuwepo kwenye ukaguzi huu vifaa vyao havitawekwa kwa ajili ya ukaguzi.

(b) Makamanda wa polisi ndio wenye mamlaka ya kuvitawanya vitu vilivyopo ndani ya sanduku la ukaguzi iwapo ataona kuna haja ya kufanya hivyo.

9. (a) Kila ukaguzi rasmi lazima uanze na gwaride kwa mujibu wa P.G.O. No. 85.

(b) Asakari wa vyeo vyote isipokuwa walioko kazi au wagonjwa kambini watajipanga kwa ukaguzi. Pia wote watatakiwa kuwepo katika vituo vyao kwa ajili ya mahojiano na afisa anaekagua.

(e) Siku za mapumziko hazitatakiwi kutumika kwa ajili ya ukaguzi rasimi.

(d) Askari ambao hawata hudhuria gwaride bila ruhusa watashitakiwa kijeshi.

(e) Baada ya gwaride wakaguzi na askari walioteuliwa watatakiwa kuonyesha rayoti, na mafunzo ya silaha.

10. Mbwa na Farasi kama wapo hawata takiwa kukaguliwa katika paredi isipokuwa watatakiwa kuandaliwa kwenye banda lao la wazi wakiwa na askari wao kwa ajili ya kukaguliwa na afisa anaekagua.

11. (a) Baada ya gwaride majengo yote,magari, mbwa,farasi, silaha na risasi vielelezo, mali za kituo,samani za kituo pamoja na masanduku ya vifaa ya takaguliwa kasoro zitaandikwa kabla na zitatolewa ufafanuzi na Mkuu wa Kituo.

(b) Askari atakae patikana amefanya uharibifu au mapungufu katika sanduku lake atasitakiwa kijeshi na adhabu atakazo pewa ni kulipa mali aliyoharibu endapo itabainika mali aliyoharibu ilitokana na uzembe wake.

12. Vitabu vyote vitakaguliwa na kupangwa katika utaratibu maalum. Afisa anae kagua atahakikisha vitabu na mali vinatunzwa kwa mujibu wa taratibu za kijeshi.Uangalizi mkubwa uzingatiwe katika kitabu cha taarifa(RB) na kwa usahihi au vinginevyo vitavyositahili kuingizwa. Alama za mkato(Cross-references lazima ziangaliwe.

13. Askari wa vyeo vyote waliopo kwenye ukaguzi watatakiwa kuhojiwa kwa kifupi kuhusu uelewa wa amri za kudumu za jeshi la polisi/kazi za polisi na sheria za kawaida na wale wenye vipaji maalum au wasiolewa kitu kabisa. Baada ya ukaguzi askari wote watapewa nafasi ya kutoa malalamiko, maoni , ushauri hata kueleza matatizo yao binafsi. Hoja zao zitaandikwa na kushughulikiwa.

14. Afisa anaekagua baada ya kumaliza ukaguzi, kabla hajaondoka ataandaa taarifa ya majumuisho ya ukaguzi wa kituo au kikosi.

15. Taarifa ya ukaguzi rasmi itaandaliwa kwa kufuata utaratibu ufuatao; Vitajazwa na vipengele visivyo husika vitaonyeshwa kama ifuatavyo;-

I. Uanzishaji na Uimarishaji

Itaonesha yafuatayo

(a Uanzishaji

(b Jina la Mkuu wa kituo

(c Idadi ya askari ambao hawakuhudhuria ukaguzi bila sababu maalum

(d Mabadiliko yaliyopendekezwa katika nguvu iliyopo

(e Maoni yoyote katika mgawanyo wa kazi za askari.

II. Gwaride na Kwata.

(a Uwezo wa mageuko.

(b Uwezo wa kikundi na Kwata ya kutuliza ghasia.

(c Uwezo wa Mkaguzi na Viongozi wa cheo cha chini waliyojaribiwa kuongoza kikundi.

III Majengo na Viwanja

(a Mwonekano.

(b Marekebisho yanayo hitajika.

IV Magari.

(a Mwonekano,

(b Upungufu wa vifaa,

(c Kitabu cha mzunguko wa magari na matumizi ya mafuta.

V Baiskeli

(a Idadi iliyopo,

(b Mwonekano,

(c Mapungufu.

VI Vifaa vya Redio

(a Mwonekano wa Redio ,betrii na chaja zake.

(b Ubora wake,

VII Mbwa wa Polisi

(a Idadi yao.

(b Afya zao.

(c Mafanikio yaliyopatikana.

VIII Farasi wa Polisi

(a) Idadi yao.

(b) Afya zao.

(c) Mafanikio yaliyopatikana.

IX Silaha na Risasi

(a) Mwonekano.

(b) Mapungufu.

X Mabomu ya Moshi ya machozi

(a) Mwonekano.

(b) Mabadiliko yanayotakiwa kufanyika kutokana na uharibifu uliyotokea.

(c) Mapungufu.

XI Samani,mali za Kituo zilizopo.

(a) Mwonekano.

(b) Mapungufu.

(c) Matengenezo au Mabadiliko yanayohitajika.

(d) Mapendekezoya kuongeza au kupunguza.

XII Zima moto

(a) Mitungi inayohitajika kujazwa.

(b) Inatosheleza mahitaji ya kituo.

(c) Ufanisi wa kwata ya kuzima moto.

(d) Maboksi ya vifaa.

(e) Mapungufu.

(f) Mabadiliko.

XIII Vitabu vya Kituo

(a) P.F. 16 Kitabu cha vielelezo

(b) P.F. 20 Kitabu cha Maabusu.

(c) P.F. 40 Kitabu cha taarifa ya wagonjwa.

(d) P.F. 51 Kitbu cha Matukio.

(e) P.F. 54 Kitabu cha hati ya Kusafiria.

(f) P.F. 55 Kitabu cha hati za wito wa mahakama.

(g) P.F. 57 Kitabu cha likizo.

(h) P.F.59 Kitabu cha mpango kazi.

(i) P.F. 60 Kitabu cha mashitaka ya kijeshi.

(j) P.F. 62 Kitabu cha doria.

(k) P.F. 63 Kitabu cha mali za watuhumiwa

(l) P.F. 65 Kitabu cha hati za dhamana.

(m) P.F. 104 Kitabu cha matengenezo.

(n) P.F. 162 Kitabu cha taarifa za matukio.

(o) P.F. 168 Kitabu cha kutunza mali za serikali.

(p) P.F. 179 Kitabu cha kutunza kumbukumbu za watu waliopotea na wanaotafutwa.

(q) P.F. 181 Kitabu cha mali zilizookotwa.

(r) P.F. 186 Kitabu cha gwride la utambulisho.

(s) P.F. 187 Kitabu cha wageni.

(t) P.F. 200 Kitabu cha silaha.

(u) P.F. 214 Kitabu cha uangalizi wa maeneo yalioruhusiwa kibiashara.

(v) P.F. 219 Kitabu cha silaha za watu binafsi.

(w) P.F. 221 Kitabu cha upelelezi.

XIV ASKARI WALIOPO

XV Kumbukumbu za kituo.

XVI Pesa Taslimu zilizoko kituoni.

(a) Kitabu cha pesa kitakachokaguliwa.

(b) Dosari.

XVII Mahabusu

(a) Idadi iliyopo mahabusu na afya zao.

(b) Hali ya chumba cha mahabusu.

(c) PrisonersChakula cha mahabusu, upungufu na hali yake.

XVIII Uangalizi wa watuhumiwa wenye tabia mbaya.

(a) Uhakika wa kumbukumbu

(b) Uhakika wa ufuatiliaji wa police

XIX. Uhalifu na hali ya wilaya.

(a) Hali ya uhalifu ya wilaya kiujumla

(b) Kuongezeka ama kupungu kwa uhalifu tokea ukaguzi uliopita.

(c) AnyMatatizo na mapendekezo yake.

(d) Juhudi za uzuiaji makosa

XX. Doria ya eneo maalum kwa malengo yaliyopangwa.
Kiwango cha doria katika maeneo yaliyo pangwa.

XXI Mfumo wa doria.

Ubora na umuhimu wa doria mara kwa mara.

XXII Ustawi wa askari.

XXIII Ugonjwa na malaria.

XXIV Ulinzi wa kituo

Gwaride la kuhami kituo kwa ufanisi.

XXV Elimu katika amri za kudumu /kazi za polisi na sheria za kawaida.

(a Askari wenye uelewa wakutosha.

(b Askari wenye uelewa mdogo au wasio na uelewa.

XXVI Malalamiko na maombi.

XXVII Askari wenye uwezo mkubwa.

XXVIII Mengineyo.

XXIX Taarifa binafsi ya ukaguzi uliyofanywa na afisa mkaguzi.

XXX Taarifa kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa kwa hatua zake bado inahitajika.

16. Maafisa wakaguzi wanawajibu wa kuchapa taarifa zao na kuzituma mapema,mara baada ya ukaguzi kufanyika.

17 Utaratibu wa kawaida wa kila siku pamoja na ujazaji wa taarifa za ukaguzi zitashughulikiwa ka ifuatavyo:-

Aliyefanya ukaguzi	Kilicho kaguliwa	Aliyechukua hatua	maelezo ya hatua iliyochukuliwa
Mkuu wa Kikosi cha kuzuia ghasia Mkoa	Kikosi cha kutuliza Ghasia cha Mkoa	Mkuu wa kikosi cha kuzuia Ghasia Kamanda wa Polisi wa Mkoa.	Andaa nakala tatu za taarifa yake kwa kutuma nakala mbili zilizokamilika kwa Kamanda wa polisi wa Mkoa. (a) Kutoa maelekezo zaidi kwa njia ya maandishi kwa Mkuu wa Kikosi cha kutuliza ghasia (b) Nakala moja itawekwa kwenye jalada na nyingine iliyokamilika ikiwa na mapendekezo yake itatumwa kwa Mkuu wa Kikosi cha kutuliza Ghasia.
		Mkuu wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia.	Atatoa maelekezo zaidi kwa maandishi kwa Mkuu wa Kikosi cha kutuliza Ghasia kuhusiana na nakala iliyotumwa kwa Kamanda wa Polisi Mkoa.
Mkuu wa Kikosi cha kutuliza	Mkuu wa Kikosi cha Kutuliza		

Ghasia. Makamanda wa vikosi vya Reli Makamanda wa vyuo vya mafunzo ya Polisi. Kamanda wa Bendi.	Ghasia. Vikosi vyote. Vyuo vya Polisi na Kikosi cha Mbwa na Farasi. Kikosi cha Bendi cha Dar es salaam na Zanzibar.	Makanda wa Vikosi vya Reli, Vyuo vya mafunzo vya Polisi. Kamanda wa Bendi.	Ataandaa nakala moja ya taarifa na atachukua hatua zote muhimu. Ataandaa nakala mbili na atazituma kwa Kamanda wa Polisi Dar es salaam,kwa hatua zake muhimu. Ataandaa nakala moja ya taarifa ya hatua alizo chukua.

18. Maelezo ya hatua zote zilizo chukuliwa kushughulikia mapendekezo na ukosoaji kwenye ripoti ya ukaguzi ya ingizwe uapnde wa kulia mwa kila ukurasa moja kwa moja na mkabala kila kitu kwa kumbukumbu. Maafisa wa ngazi zote wa hakikishe hatua muhimu zimechukuliwa kabla ya ripoti zao za ukaguzi hazija pitishwa kupelekwa ngazi za juu. Maelezo ya kila jambo ambayo hayataweza kushughulikiwa katika ngazi ya kawaida yatakuwa chini ya kichwa cha habari XXIX cha ripoti husika. Hatua yeyote itakayo chukuliwa itawekwa katika kumbukumbu.

19. Maafisa wengine wanatakiwa kufanya ukaguzi wa kawaida kwa kutembelea kama ilivyoonyesha hapa chini, ili kuangalia uwezo wa askari moja kwa moja ama vinginevyo chini ya himaya zao.

Ofisa anae kagua	Kikosi kinacho kaguliwa	Muda wa ukaguzi
Mkurugenzi wa makosa ya Jinai	Vikosi vyote vya upelelezi mikoa.	Kila nusu mwaka.
Mkuu wa kitengo cha mawasiliano.	Vitengo vyote vya mawasiliano.	Kila nusu mwaka
Makamanda wa vikosi vya Reli.	Vikosi vyote vya reli.	Kila nusu mwaka.
Kamanda wa kikosi cha mbwa na farasi.	Vikosi vyote vya mbwa na farasi isipokuwa Chuo cha mafunzo ya polisi.	Kila nusu ya mwaka.
Mkurugenzi wa Bendi	Kikosi cha bendi Dar es salaam	Kila robo ya mwaka
Kamanda chuo cha mafunzo ya polisi	Bendi ya chuo cha mafunzo ya polisi	Kila robo ya mwaka
Boharia Mkuu	Bohari kuu na ghala la silaha	Kila robo mwaka
Mtunza silaha Mkuu.	Watunzaji wa maghala ya silaha wa Mkoa na Vikosi vya Kutuliza ghasia na Wilaya.	Kila baada ya nusu mwaka.

PGO - 48
LIKIZO

Sehemu ya kwanza

Likizo

1. Likizo lazima ziheshimike kama sehemu ya haki na isipotolewa na mwajiri muhusika anahaki ya kupata mishahara badala ya likizo. Pesa atakayo lipwa italingana na siku alizositahili kuwa likizo.

2. Likizo zitahesabika kwa kiwango cha siku 28 kila mwaka kwa maofisa isipokuwa kwa wale ambao wanatumikia mikataba ambao likizo zao zitahesabika kulingana na mikataba wanayotumikia.

Fomu za maombi ya likizo

3. Pamoja na maombi ya likizo kutolewa kwa kufuata maelekezo ya Daktari inavyoshughulikiwa katika sehemu ya nneya fomu hizi za likizo katika sehemu ya 18, 19, 24,25 na 26 maofisa wa ngazi hizi watajaza fomu moja kama inavyo fafanuliwa katika sehemu ya nne hapa chini:

Namna ya kushughulikia na kutoa likizo

4 (a) Kutakuwa na mzunguko wa likizo inayoanzia tarehe 1 kila mwaka ya Maafisa wote ambao wako katika utumishi kufuatia tarehe za ajira zao.

(b) Ofisa yeyote anapokuwa likizo anaweza akaongezwa likizo ya siku 28 ya mwaka ambao hakwenda bila kujali muda ambao amesha dumu katika utumishi isipokuwa katika mazingira yatakayo elezwa katika sehemu (c)

(c) Kufuatia idhinisho la Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Usalama wa Raia,Afisa yeyote anaweza kupewa likizo bila kuwepo ili kushughulikia matatizo yake binafsi na likizo hii itapunguzwa katika siku za likizo yake ya mzunguko wa kawaida.

(d) Likizo zitahusisha siku za jumamosi na Jumapili pamoja na siku zote za sikukuu isipokuwa siku za safari tu siku za jumamosi na jumapili zitaingizwa katika malipo isipokuwa kwenye mazingira ambayo afisa atakuwa

kwenye likizo ya kusitaafu, kuacha kazi au kuachishwa kazi au au akiwa katika likizo isiyo na malipo. Likizo za ugonjwa na uzazi zitalipwa.

(e) Kupatiwa likizo ambayo Ofisa anasitahili kwenda itatengemea uamuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania.

(f) Hakuta kuwa na kipingamizi kwa Ofisa atakayechukua likizo ndogo ndogo ilimradi mwisho wa mwaka atachukua likizo ya mzunguko wa kwanza Afisa ataruhusiwa kuendelea na likizo endepo kutakuwa na dharura kwa kipindi cha miaka miwili kama hakuna dharura likizo hiyo haitaruhusiwa ataendelea na mzunguko wa likizo pale inapoanzia na inapoishia.

(g) Ofisa aliyoko likizo hatarudi kazini kutokana na likizo hiyo kuwa niya kustaafu, kuachishwa kazi au kuondolwa kazini.

(i) Likizo za kawaida zitahesabika baada ya tarehe ya kuacha kazi kuanzia mzunguko wa mwisho wa likizo yake ya malipo.

(ii) Uwiano wa likizo za dharura kama zipo katika mzunguko wa likizo hizi za utumishi zitalipwa kwa kuzingatia siku za likizo za dharura.

(h) Endapo ofisa atakuwa amepewa pesa za malipo za mzunguko wa likizo yake kwa mujibu wa kifungu (i) – (ii) hapo juu atawajibika kurudisha serikalini mshahara kwa uwiano kufuatia siku anazo sitahili.ukokotoaji wa likizo ya uwinoutazingatia yafuatayo: nusu siku au zaidi itahesabiwa kama siku moja chini ya nusu siku haitahesabika.

(i) Maafisa walioajiriwa kama waalimu katika vyuo vya mafunzo ya Polisi watatakiwa kuchukua likizo endapo kutakuwa hakuna mafunzo yanayoendelea.

Sehemu ya II – Nauli ya likizo

Uwezeshaji wa Nauli ya likizo

5. (a) Utaratibu ufuatao utatumika katika uwezeshaji wa pesa ya likizo:

(i) Uwezeshaji wa nauli ya likizo utahusiana na

mzunguko wa likizo wa miaka miwili utakao anza tarehe moja mwezi wa kwanza kwa kila mwaka kwa afisa mhusika ambae yuko kwenye ajira kwa tarehe hiyo na tarehe ya siku ya kwanza ya kuajiriwa.

(ii) Afisa anatakiwa apewe pesa ya nauli ya likizo mara moja kila baada ya miaka miwili kulingana na kiwango cha nauli kilichopo katika huduma ya reli au usafiri wa umma wa gari unaotambulika kulingana na madaraja kama yalivyo kwenye kiambatanisho J/I la tamko la serikali kwake,mke wake na watoto wasiozidi wane kwenda na kurudi kutoka katika hudumu ya usafiri wa karibu nae.

(iii) Kwa maafisa waliopewa upendeleo kusafiri bure mara moja kila baada ya miaka miwili akitumia usafiri wake kwenda nyumbani kwake likizo anaweza kupewa pesa tasilimu,kutokana na posho ya usafiri kama ilivyo tangazwa kwenye waraka wa serikali katika kifungu L na kifungu kidogo cha (ii) kama ilivyo ainishwa hapo juu, au kulingana na kiwango kutokana na kiwango cha usafiri wa reli au barabara kutengemea kipi ni rahisi.

(iv) Pesa ya upendeleo ya usafiri inayoweza kutolewa kwa Afisa anaesafiri kwenda kwake au eneo linguine litakalokuwa limetajwa,itatengemea kiwango ambacho kitakuwa kimepangwa na serikali.

(v) Pesa ya upendeleo inaweza kutumika kwa mwaka wowote kwenye mzunguko wa likizo ya miaka miwili. Masharti ya kutosheleza kupewa pesa ya likizo ya upendeleo lazima idhinishwe na Mkuu wa Jeshi la Polisi na apewe taarifa baada ya likizo.

(vi) Hata hivyo pesa ya upendeleo ya likizo haita ondolewa kwa Ofisa mhusika kama atakuwa amezuiwa kwenda likizi kulingana na majukumu atakayo kuwanayo kwa kipindi chake cha likizo.

(Vii) Gharama za matukio zinapatikana katika amri J.34 ya walaka wa Serikali.

(b) Kwa nyongeza ya upendeleo kama ilivyo wekwa kwenye sehemu (a) hapo juu Ofisa aliyoko Mkoani kwa maoni ya Kamnda wa polisi Mkoa ambae hata tumia usafiri wa

majini ataruhusiwa kutumia usafiri mwingine kama ilivyoainishwa kwenye amri H.6 kwenye walaka wa Serikali na kuelezewa kwenye sehemu (a). Afisa anaeendelea na likizokatika Mkoa ambao unaweza kufikika kwa usafiri wa nchi kavu au majini hata pata huduma hiyo ya upendeleo.

Haki nyinginezo za Maafisa waliopo/waishio katika Mikoa ambayo haifikiki kwa usafiri wa barabara au maji.

6. Pamoja na nyongeza ya upendeleo uliowekwa katika amri No. H 5ya serikali,Maofisa waliooa na wenye watoto wanaotambulika wanne waishio katika mikoa isiyofikika na usafiri wa barabara au maji wanapo safari kwenda likizo watapewa amfao yafuatayo watakapo kuwa wakisafiiri kupitia Dar es Salaam:

(a) Maafisa waishio katika Mikoa isiyofikiwa na usafiri wa maji.

(i) Ofisa mwenye hadhi ya kusafiri katika daraja la kwanza kwa Treni atapewa usafiri wa ndege mara moja katika kila mizunguko miwili ya likizo yake na pia atalipiwa gharama zote za chaji ya uwanja kwenda Dar es Salaam, wakati wa kurudi Ofisa mhusika atapewa nauli kama gharama ya kusafiria watoto hao wakati wa kurudi.

(ii) Maafisa wanaositahili kusafiri katika daraja la pili au la tatu kwa gari moshi ukiondoa wale wanye mkataba wa bahashishi watapewa gharama za malipo za usafiri mara moja kwa kila baada ya mzunguko wa likizo kwa kila baada ya miaka miwili kutoka Dar es Salaam hadi Mkoani kwake kwenda na kurudi, kwa wanandoa na watoto wa nne wanaokubalika watasafiri kwa ndege na anapomaliza likizo Ofisa huyu atarejeshewa gharama zake alizotumia kwa usafiri wa watoto hao.

(b) Maafisa wanaositahili kupata nyongeza ya upendeleo iliyoainishwa katika sehemu (a) watapata mara moja katika mzunguko wa miaka miwili nauli ya usafiri wa anga kwenda na kurudi kati ya Dar es Salaam na uwanja wowote wa ndege uliopo jirani na anakokwenda likizo kama tuu atakuwa amesafiri kwa usafiri wa anga, meli au basi kama ilivyo katika sehemu (a) hapo juu.

(c) Mashriti.

(i) Upendeleo maalum wa safari ulioainishwa katika kifungu 6 (a) na (b) pamoja na ongezeko la kupatiwa gharama za usafiri kwa Ofisa alizotumia katika mzunguko wa likizo ya mwaka kwa kila baada ya miaka miwili kama ilivyo katika amri No H.5 ya agizo la Serikali Maofisa wanaweza wakatumia gharama zao na wakarudishiwa baada ya mzunguko wao wa likizo.

(ii) Kwa kuondoa mashaka imefafanuliwa kwamba nyongeza ya upendeleo wa usafiri kama ilivyoainishwa sehemu (a) na (b) italipwa tuu kwa Ofisa aliyesafiri katika maeneo yasiyokuwa na usafiri wa maji Maafisa hawatadai ghalama za usafiri wa anga kwenda kwenye safari nyingine. Kama afisa ataamua kusafiri eneo tofauti na makazi yake akiwa likizoni gharama ya safari hiyo ya sizidi matumizi ya usafiri aliotumia kwenda sehemu yake ya makazi kwa usafiri wa kawaida wa barabara au majini.

Mafao ya usafiri kwenye likizo ya kuacha kazi , au kumaliza mkataba wa kuacha kazi au kuachishwa kazi.

7 . (a) Ofisa anaetaka kusafiri kwenda kwake kwa kutokana na mazingira hapo juu atapata upendeleo wa kusafiri bure kama ilivyoonyesha kwenye amri No.H.5 (a) ya agizo la serikali kwa kuzingatia kwamba:

(i) Amemaliza kipindi cha miaka miwili akiwa kazini na,

(ii) Hajawahi kupata upendeleo wa usafiri wa bure kwa kipindi hicho cha miaka miwili

(b) Wakati ambao Ofisa aliyepewa pesa na kustaafu utumishi kabla ya kumaliza miaka miwili kama upendeleo wa pesa aliopokea,italazimika kurudisha gharama iliyoingiwa na serikali katika kumsafirisha yeye na familia yake toka likizo.

Gharama ya usafiri katika likizo ya kustaafu

8. Afisa anaestaafu kutoka katika utumishi anastahili kupata upendeleo wa usafiri wa bure kama ilivyoainishwa sehemu ya 5(a).

Kuongeza muda wa likizo ya dharura.

9. Katika mazingira ya kawaida kwa idhinisho la serikali, likizo ya dharura inaweza ikaongezwa kwa kipindi kifupi kwa malipo kuongezwa huko kutazingatia siku atakazo punguza katika siku alizopewa za kumaliza kazi hiyo maalum.

Maombi ya likizo

10. (a) Maombi yote ya likizo lazima ya tumwe kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi katika utaratibu unao stahili kama ilivyo ainishwa hapa chini:-

(i) Maofisa na Wakaguzi:

Fomu katika kurasa H/I kwa agizo la serikali.

(ii) Askari wa cheo cha chini

Katika P.F. 185 – "*Karatasi ya Maombi*"

(b) Askari wote wa vyeo vya chini wanakumbushwa kutuma maombi yao ya likizo mapema kabla miezi mitatu ya kuanza likizo hiyo.

(c) Ofisa huyo ataanza likizo baada ya kusomewa na Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Kadi ya urithi

11. Kila Afisa anatakiwa kutuma nakala mbili za kadi ya urithi pamoja na fomu za maombi ya likizo.

Likizo ya ugonjwa

12. (a) Kutokuwepo kazi kwa askari anae hesabika kuwa ni mgonjwa hesabika kama likizo ya ugonjwa kutokuwwe kazini kwa sababu ya ugonjwa lazima ijulishwe kwa Mkuu wa Jeshi la polisi na inatakiwa kuambatanishwa na fomu No. K 5 ya agizo la serikali utoro kazini itakuwa ni utovu wa nidhamu na utachukuliwa hatua za kinidhamu.

(b) Likizo baada ya kuungua mda wowote wa kutokuwepo

kazini baada ya kuungua kufuatia maoni ya daktari itahesabika kama likizo baada ya ugonjwa.

(c)

Likizo baada ya ugonjwa inaweza kuwa nje ya kituo cha kazi.

Kutokana na mapendek
anaweza kuruhusiwa kut
Tabibu na lazima aeleze

Likizo baada ya Ugonjwa inaweza kuthibitishwa na Katibu Mkuu au Inspekta Jenerali.

14. Likizo baada ya ugonjw
Muungano wa Tanzania
Mkuu au Inspekta Jener
cha mwombaji ,kutokana

Ukomo wa Ugoinjwa na likizo baada ya Ugonjwa.

15 (a)

(b)

16. (a)

	(b)
Likizo baada ya kupata nafuu ya Ugonjwa.	
17.	Afisa atakayepewa liki Ugonjwa atakayoitumia kupewa huduma ya Us kama ilivyoelekezwa na na Barabara utatolewa wasiopungua wanne ata
Sehemu III–Taratibu za likizo kwa askari wa vyeo mbalimbali.	
18	(a)
Aina ya Afisa:	Ukubwa wa likizo kwa m
Masajenti Meja, Masajenti, Makopolo na walio na vyeo vya chini	12-36
	(b)
	(c)
19.	(a)
	(b)
20.	Katika mazingira yoyote wa Kituo hatakiwi kuch likizo,mapendekezo yak mapendekezo yoyote ya

katika eneo husika kat
wakati anayatuma kw
kuthibitisha likizo.

Kujipa Likizo kusikozidi saa 48

21 Afisa msimamizi wa po
Gazeti la Serikali ,au Afis
Jenarali kuwa msima
lolote,anamamlaka ya ku
himaya yak e mwenye ch
masaa 48 kwa wakati
wakati wa kufuatilia liki
huyo.

Wake na Wanafamilia wanaoambatana na Mume

22. Mke na au watoto wa kid
wa cheo cha chini wa
litafanyika kwa wino mw
mafunzo katika kitabu
maelezo ya hati ya kus
Hakuna usafiri zaidi .kw
kwa kwa mke au wana
chini au askari wa cheo
ya miaka mitatu kupita .

Hati ya kusafiria.

23 Hati ya kusafiria (F.P. 5
vyeo mbalimbali pindi wa
P.G.O. No. 33.

Kuzidisha siku za Likizo

24. Askari wa vyeo mbalimb
endapo anaamini kwam
iliyopangwa itamlazimu
Polisi kilicho jirani kinac
aliye juu ya Mkaguzi akie
hati ya kusafiria aliyopew

25. Mkuu wa kituo ataandik
tarehe na muda wa kup
zinazofanana na hizo.

26. Endapo itaonekana ni

kazini kwa muda Fulani,
katika kituo alichoripoti
safari yake.

27 Ikitokea amejipa likizo n
au kutotii amri halali kw
za kinidhamu zitaanzih
kujali adhabu itakayotol
kwa siku zote ambazo
kanuni ya 65 ya Kanu
Polisi,1995.

28. Kwa mantiki ya amri hii,n
yatakatwa kwa siku amb

Sehemu ya IV—Likizo ya Ugonjwa – Vyeo vyote

Utolewaji wa Likizo za Ugonjwa.

29. Utaratibu ufuatao ni la
Likizo za Ugonjwa: -

(a)

(b)

30. Alama zifuatazo zitatu
iliyotolewa kwa Afisa hus

L.U. -

M.K. -

K.N. -

K.H. -

L.N. -

31 31. Taarifa kamili
zilizotolewa kwa mwez
katika F.P. 191 – "Taari
ambayo itapelekwa Maka

Sehemu ya V – Sheria mbalimbali

Maafisa wenye mashauri Mahakamani au Uchunguzi wa kiidara

32. Likizo haitatolewa kwa
mahakamani au wana
Idara.Maafisa wanaohita
na ambao wameshapew
likizo hiyo.Likizo haitato
mashauri ya Jinai au wa

Likizo ya Majeruhi

33. Majeruhi kwa upande w
Gazeti la Serikali ar
kubwa,kwa kawaida itab
akiba ya Afisa aliyetanga
utashi wa Inspekta Je
huduma.

34. Likizo ya akiba ya wakag
wa mamlaka katika M
hautolazimika kufanywa
Polisi.

35. Sambamba na hilo likiz
mbalimbali zimeingizwa
za mikoa,hivyo kubadi
hakuwezifanyika mpaka
uhamisho kumehidhinish
Na. 60, au pale ambapo
wilaya yeyote mojawapo
walio katika Wilaya husik

36. Kuziba mapengo ya W
shwala linalomhusu Mku

Utunzaji Salama wa Silaha na Risasi wakati wa kwenda Likizo.

37. Askari wote wa Polisi ka
silaha na risasi kwa Mk
vifaa hivyo itatolewa.

38 Maafisa wenye silaha
Chumba cha kuhifadhia
Katika mazingira hayo,
au utunzaji na madai yey
kutosha yametolewa ya
leseni ya silaha wakati w

Mapumziko baada ya kazi.

39. Askari yeyote wa vyeo
Mapumziko baada ya ku
nje ya eneo la kituo chak
wake wa Kambi madhum

Mapumziko ya kila Juma.

40 Kwa kawaida kila aska
kipindi kimoja cha mas
Mkuu wa Kituo.Hairuh
likizo maalumu ya upen
za mwisho wa Juma au

Likizo ya

41. Likizo ya Uzazi haitachu
kwa kawaida ina ukomo
Kanuni za Kudumu za Se

P.G.O - 53

TARATIBU ZA UPANDISHWAJI VYEO

Kwa kawaida
1.

(a) upandishwaji vyeo kwa askari polisi wa kada zote atazingatia umbele, uwezo na sifa nyingine zilizoainishwa. Kimsingi maofisa hawatapandishwa vyeo hadi hapo watakapo faulu mitihani iliyoainishwa katika kanuni za kudumu za jeshi la polisi namba 45 au kwa msamaha wa kutofanya mitihani hiyo.

(b) Maafisa wote wanaofanya kazi chini masharti ya muda mfupi waliopandishwa cheo cha Mkaguzi Msaidizi na kuendelea watatakiwa kutumikia cheo hicho kwa muda wa miezi sita kwa majaribio kabla ya kuthibitishwa katika cheo hicho. (tazama pia aya ya 9-11 katika Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi namba 52)

2. Makamanda wa mikoa / Vikosi na Wakuu wa Polisi wa wilaya na Vituo kwa namna ya
upekee wanawajibika kushughulikia malalamiko ya upandishwaji vyeo kwa askari wa vyeo vyote katika muda muafaka na kuhakikisha kwamba hakuna anayesahaulika.

3. Mapendekezo yote ya upandishwaji vyeo yazingatie taratibu zilizoainishwa katika kiambatisho “A”.

Upandishwaji Vyeo kwa kada ya Maafisa

4. Upandishwaji vyeo kwa ngazi ya uofisa kwa kwawaida utawahusu tu wakaguzi waliothibitishwa kazini na kufaulu mafunzo ya ngazi ya uofisa.

Upandishwaji wa vyeo katika kada ya Ukaguzi

5. Upandishwaji wa vyeo katika kada ya Ukaguzi utatolewa kwa wale tu waliotumikia cheo
cha Mkaguzi Msaidizi kwa muda usiopungua miaka mitatu kabla ya kupandishwa cheo na kuwa Mkaguzi.

Upandishwaji wa vyeo kwenda kada ya Ukaguzi

6. Upandishwaji wa vyeo toka kada ya askari wa vyeo mbalimbali kwenda kada ya Ukaguzi utazingatia tu watumishi wenye sifa zifuatazo:-

(a) Utumishi usiopungua miaka miwili
(b) Aliyehitimu kidato cha Nne
(c) Aliyefaulu vizuri mafunzo ya Ukaguzi Msaidizi.

Upandishaji vyeo kwa askari wa vyeo mbalimbali

7. Upandishwaji wa vyeo kwa askari wa vyeo mbalimbali utatolewa tu kwa wenye sifa zifuatazo:-

(a) Kwa konstebo mwenye utumishi wa miaka mitatu kabla ya kupandishwa cheo
kuwa koplo.

(b) Kwa koplo mwenye utumishi wa miaka mitatu kabla ya kupandishwa cheo
kuwa sajenti.

(c) Mwenye cheo cha sajenti kwa miaka mitatu kabla ya kupandishwa cheo kuwa
stafu sajenti.

(d) Aliyefaulu vizuri mafunzo husika ya kupandishwa cheo.

Bodi za Upandishaji Vyeo

8. (a) Upandishwaji vyeo katika kada ya Ukaguzi na askari wa vyeo mbalimbali utafanywa
na bodi ya upandishaji vyeo, ambayo itawasilisha mapendekezo yake ka Inspekta Jenerali wa Polisi.

(b) Mapendekezo mengine yote ya upandishaji vyeo yatafanywa kwa kuzingatia sheria ya tume ya utumishi ya Jeshi la Polisi na Magereza na kanuni zake.

9. Inspekta Jenerali ataunda bodi za upandishaji vyeo na kuteua maafisa watakaounda bodi hizo

10. Bodi yaweza kuwataka waliopendekezwa kufika mbele ya bodi na yaweza kuchukua hatua
yoyote ambayo inafiriki ni muhimu katika kuwezesha kufikia maamuzi.

Mapendekezo ya upandishaji vyeo

11. Kabla ya bodi ya upandishaji vyeo kukutana, Wakuu wa Polisi wa Wilaya au vikosi pamoja
na Makamanda, wataandaa taarifa ya upandishwaji vyeo (PF.175) ya kila aliyependekezwa
na itatumwa kwa kutumia majalada ya siri kwenda kwa Inspekta Jenerali wa Polisi
kupitia kwa wakuu wa idara.

Iwapo Kamanda anafikiria kumpendekeza mtumishi ambaye amefanya kazi kwenye himaya kwa muda usiozidi miezi mitatu atalazimika kuaandaa taarifa ya upandishaji cheo kama ilivyoelezwa kwenye aya ya 11 na kuituma kwa Kamanda ambaye mtumishi huyo alikuwa chini ya himaya yake hapo awali.

Kamanda aliyetumiwa taarifa hiyo ataandaa taarifa na kuziwasilisha taarifa zote kwa Inspekta Jenerali wa Polisi.

KIAMBATISHO "A" (Cha P.G.O. NO. 53)

UPANDISHAJI VYEO – KANUNI ZA MSINGI

1. Uteuzi wote katika upandishaji vyeo utazingatia umbele sifa nzuri na (isipokuwa katika mazingira maalum) kuwa na elimu maalum na ujuzi wa ziada. Matakwa ya sheria ya msingi ni kwamba kipaumbele kitolewe kwa maafisa walioonesha uwezo katika

uongozi,upeo mkubwa na juhudi za pekee katika kutekeleza majukumu yao ya kazi

2. Maofisa wenye jukumu la mapendekezo ya upandishaji vyeo hawana budi kuyafanyia kazi madai ya upandishaji vyeo ya kila mtumishi katika katika hamaya zao kwa kuzingatia umbele, lakini maamuzi yao yatolewe kwa kuzingatia sifa njema bidii ya kazi na pasipokuwa na mashaka yoyote ya mtumishi kumudu majukumu ya cheo cha hicho anachopendekezwa,bila ya kujali kigezo cha umbele cha mtumishi aliyependekezwa.Umbele pekee hauwezi kukubalika kama sifa pekee inayojitosheleza kumpandisha mtumishi cheo.

. 3. Upandishaji vyeo wa haraka na mfululizo uko wazi kwa maafisa waliofuzu na kuonyesha uwezo
wa kipekee na juhudi isiyo na kifani, au aliyeonyesha uwezo wa kumudu nafasi Fulani inayostahili kushikwa na mwenye cheo cha juu.Zingatio maalum litolewe kwa watumishi
wenye sifa hizo na wanapaswa kupendekezwa kupandishwa vyeo bila ya kutilia maanani suala
la umbela.

4. Sifa maalum za kuzingatiwa katika kufanya uteuzi kwa watumishi waliofuzu kupandishwa vyeo
katika orodha ya umbele ni kama ifuatavyo:-

(a) Tabia njema
(b) Elimu
(c) Ujuzi wa kataaluma
(d) Uwezo wa kuongoza
(e) Anayedhibiti hisia zake
(f) Tabia njema na muonekano mzuri
(g) Asiwe mlevi
(h) Kuhudumia watu kwa staha
(i) Siha njema na bidii ya kazi
(j) Juhudi na ufanisi wa kazi za Polisi

5. Mafanikio ya jeshi la Polisi, kwa kiwango kikubwa, unategemea weledi,uongozi, mwenendo
mwema, uwezo ufanisi wa maafisa na wakaguzi. Kwa hiyo umakini wa hali ya juu ni sharti
uzingatiwe wakati wa mapendekezo ya upandishwaji vyeo katka kada hizi. Ni wale tu wenye
sifa stahiki ndio wafikiriwe katika mapendekezo.

. 6. Maafisa walioajiriwa kwa kazi zenye ujuzi maalum, hawatafikiriwa kupandishwa vyeo ya
idara zao au wigo wa ajira zao. Maafisa wengine wote baada ya kupandishwa vyeo wanaweza
kuhamishiwa idara yoyote ndani ya jeshi na hakuna upandishwaji vyeo utakaofanywa
ukihusisha uanzishwaji wa muundo wowote ule.

P.G.O - 54
TARATIBU ZA AJIRA

Sehemu ya I -Uteuzi na kuthibitishaji wa Kuruta

Ili muombaji ateuliwe kwa mafunzo awali na kuwa konstebo ni sharti awe:-
awe na umri wa miaka kati ya 18 na 25

Urefu usiopungua futi 5 na inchi 8 (akiwa amesimama bila kuvaa viatu) na upana wa kifua inchi 33 () lakini isipokuwa kwa watahiniwa waliofaulu vizuri kiingereza na mtihani wa kidato cha nne (daraja la 3) au zaidi wanaweza kukubaliwa kama kimo chao hakipungui urefu wa futi 5 na inchi 6.

Waombaji wa kike wenye sifa sitahiki lakini wenye urefu wa futi 5 inchi 4 pia wanaweza kufikiriwa kwa mafunzo ya awali.

Waliothibitishwa na daktari wa serikali kuwa na afya njema kumudu majukumu ya Jeshi la Polisi, mwenye macho yanayoona vizuri bila kuvaa miwani kwa vipimo 6/6 R-6/6 L;

Mwenye tabia njema. Asiye na kumbukumbu za kutenda uhalifu Mwenye ufahamu wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na aliyehitimu kidato cha nne(daraja la 3) au elimu inayofanana na hiyo.

Awe raia wa Tanzania

2. (a) Taarifa za kuruta wanaodai kuwa walitumikia jeshi kabla ya kuajiriwa zitumwe makao
makuu ya jeshi . Waombaji waliofukuzwa kutoka jeshini, magereza,jeshi la kujenga
Taifa jeshi lolote la Polisi,polisi wasaidizi au kampuni binafsi za ulinzi hawatakubaliwa
endapo tathimini ya tabia zao itakuwa chini ya'' nzuri sana''

(b) Ni katika mazingira ya kipekee ajira ya mara ya pili kwa watumishi wa zamani wa jeshi zitakubaliwa rasmi tu na Inspekta Jenerali wa Polisi. Kwa hiyo afisa mtahini atafafanua mazingira ya ajira hiyo atakapokuwa anapeleka taarifa hizo Makao Makuu ya Polisi.Waombaji wa ajira ya mara ya pili hawatapelekwa chuo cha mafunzo ya polisi isipokuwa kwa idhini ya Makao Makuu.

3. Kwa mamlaka aliyo nayo /Inspekta Jenerali wa Polisi anaweza kumpokea mwombaji yeyote
mwenye sifa ambazo ataona zafaa.
(a) Afisa wa Polisi mwenye cheo cha kuanzia mrakibu msaidizi wa Polisi atamtahini kila
mwombaji. Na atawapitisha wale tu wenye sifa za msingi. Pia atawafafanulia masharti ya kazi. Kwa wale wenye sifa za kuhudhuria mafunzo ya awali watachunguzwa afya zao. Daktari wa serikali atajaza fomu ya uchunguzi namba 35 na kuirudisha kwa afisa mtahini.

(b) Kabla ya kupelekwa chuo cha mafunzo ya Polisi waombaji waliochaguliwa watahitajika kuweka saini kwenye shahada kwamba wao si wanachama wa chama chochote cha siasa au kundi au kutoa msaada wowote wa wazi au wa siri kwa taasisi yoyote au mchango wa fedha ,mikutano au shughuli nyinginezo. Waombaji walioteuliwa kwa mafunzo watakaofichua ushiriki wao wa siku za nyuma katika chama chochote cha siasa wanaweza kuruhusiwa kujiunga na jeshi ilimradi wamechukua hatua ya ya kusitisha uanachama wao katika vyama hivyo kabla ya kuthibitishwa kwa mafunzo.

(c) Inspekta Jenerali wa Polisi anaweza kuweka masharti ya nyongeza yatakayozingatiwa kabla mwombaji hajakubaliwa n akupelekwa chuo cha mafunzo.

4. Waombaji waliopimwa afya zao awali na kufaulukama ilivyoelezwa katika aya ya 4(a) hapo
juu watashughulikiwa kama ifuatavyo:-

(a) watachukuliwa alama za vidole katika fomu ya Polisi namba 31 A ikiwa katika nakala tatu na kuwasilishwa maabara ya kisayansi kwa ajili ya uchunguzi . fomu hizo zitakuwa na maandishi "Mkataba wa mwombaji: Tanzania,nakala nne za alama za vidole zitatumwa.

(b) Sehemu ya I,II na III ya fomu namba 161 ya maombi ya kuajiriwa itajazwa na kutumwa kwa njia ya haraka kwa Mkuu wa Chuo cha Polisi.

(c) Kamanda wa kituo kinachotuma fomu hizo atamwarifu mkuu wa chuo cha Polisi kwa njia ya simu ya upepo idadi ya kuruta wanaopelekwa na tarehe wanayotarajiwa kufika

Moshi.

5. Kuruta hawataruhusiwa kuongozana na wake na familia zao kwenda chuo cha mafunzo wala
hawataruhusiwa kuungana nao wawapo mafunzoni.

6. (a) Baada ya uchunguzi ,nakala tatu za alama za vidole zitarudishwa kwa Mkuu wa Chuo cha
mafunzo ikibainika kuwa kuruta alishawahi kupatikana na hatia ya jinai mku wa chuo atajulishwa kwa njia ya simu ya upepo ikieleza tarehe , mahali na kosa alilolifanya. Ikiwa
itabainika mwombaji alishawahi kufanya kazi ndani ya Jeshi la Polisi taarifa zitapelekwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi.

(b) Mkuu wa chuo cha mafunzo atarudisha nakala moja ya alama za vidole kwenye maabara ya uchunguzi ikiwa na namba za jeshi za kuruta mara tu zinapotolewa. Nakala ya tatu itatumwa makao makuu ya Polisi pamoja na fomu ya Polisi namba 104 A mara baada ya kumaliza mafunzo ya awali.

7. (a) Kuruta watahojiwa mara watakapowasili chuo cha mafunzo, ambapo taarifa zao zitakaguliwa. Kifungu cha 27 cha fomu ya Polisi namba 161 sehemu ya IV itakamilishwa
ikionyesha eneo alilokuwa anaishi kuruta miaka mitatu ya nyuma. Fomu ya Polisi 161 itapelekwa kwa kamanda kitengo cha uchunguzi, ambaye atairudisha pasipo kuchelewa
ikiwa imekamilishwa katika kifungu cha 27.

(b) Hatimaye baada ya kuthibitika kuwa kuruta hana tatizo la kiafya na kihalifu na kiusalama
atathibitishwa na afisa mwenye cheo kuanzia Mrakibu wa Polisi,ambapo masharti ya ajira
yatafafanuliwa kwake tena.Kisha atapatiwa namba ya kijeshi.

(c) Tarehe ya ajira itakuwa ni ile ambayo kuruta alipokelewa na kusajiliwa katika chuo cha
Polisi na Mkuu wa chuo ataingiza tarehe hiyo katika rejista ya ajira (fomu ya Polisi namba
104)

(d) kuruta anastahili kupata mshahara na marupurupu tangu tarehe ya kusajiliwa.

(e) Kuthibitishwa kwa kuruta kutatangazwa bila ya kuchelewa katika Sehemu ya II ya Amri za
utendaji za jeshi.

(f) Kuruta hawaruhusiwi kupewa mkopo katika kantini mpaka hapo itakapokuwa

imethibitishwa na Mkuu wa chuo.

Sehemu II- Kumbukumbu, Kuachishwa au kukubaliwa kwa Kuruta

Kumbukumbu

8. (a) Baada ya kuthibitishwa, Mkuu wa chuo cha Polisi, atachukuwa hatua zifuatazo kwa kuruta:-

(i). Atatuma Makao Makuu ya Polisi Fomu ya Polisi namba 161 ikiwa imekamilishwa ipasavyo;

(ii). Ataandaa nakala moja ya rejista ya ajira(Fomu ya Polisi namba 104)

(iii)Ataandaa kadi tatu za kumbukumbu ya ajira (Fomu ya Polisi namba 104A)

(iv) Atafungua jalada binafsi likiwa na :-
Kadi ya kumbukumbu ya ajira (Fomu ya Polisi Na:104 A)
Fomu ya alama za vidole (Fomu ya Polisi Na: 31A)
Fomu ya kumbukumbu ya afya (Fomu ya Polisi Na: 31C)
Fomu ya vifaa vya Kijeshi (Fomu ya Polisi Na: 31D)
Kumbukumbu zote za maandishi zilizofanywa kumuhusu kuruta husika

(b) Baada ya kufikisha miezi mitatu ya mafunzo,Mkuu wa Chuo cha Polisi atapiga pich tano kwa kila kuruta (mabega na kichwa na kichwa kikiwa bila ya vazi lolote),na namba zao za kijeshi zikiwa zinaonekana vizuri juu ya picha hizo.
Picha hizo zitabandikwa kwa utaratibu ufuatao:-

(i). Picha moja itabandikwa kwenye rejista ya ajira
(ii). Picha moja itabandikwa kwenye kitabu cha malipo cha kuruta
(iii).Picha moja itatumwa Makao Makuu ya Polisi na kubandikwa katika Fomu ya Polisi namba 161
(vi). Picha mbili, pamoja na nagativu itatumwa Kitengo cha uchunguzi.

Kufukuzwa kabla ya kuthibitishwa tayari kwa mafunzo

9. Iwapo kuruta atakataliwa na Mkuu wa Chuo kujiunga na mafunzo kabla ya kuthibitishwa hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(a) Ataelezwa sababu za yeye kutokubaliwa kuendelea na mafunzo na atarejeshwa sehemu aliyoandikishwa kwa gharama za serikali, isipokuwa kama itagundulika kuwa alishawahi kupatikana na hatia wakati yeye alieleza

kinyume,katika mazingira haya Inspekta Jenerali kwa mamlaka aliyonayo,anaweza kuamuru ashitakiwe mahakamani na iwapo atatiwa hatiani hatakubaliwa kuendelea na mafunzo.

(b) Atalipwa posho ya kujikimu kwa kiwango kilichopo kwa wakati huo kwa siku kwa kipindi alichokaa chuoni na kwa siku za safari kurudi nyumbani.

(c) Gharama za Chakula zilizotolewa wakati akiwa chuoni zitakatwa kutoka kwenye malipo ya posho tajwa hapo juu.

(c) Kumbukumbu za sababu za kukataliwa,tarehe ya kuondoka na kiwango cha posho ya
kujikimu zilizolipwa zitaainishwa nyuma ya fomu ya maombi ya ajira,fomu ya Polisi namba 161, ambayo baadaye itatumwa Makao Makuu ya Polisi. Fomu ya Polisi namba 31A pia itarejeshwa kitengo cha uchunguzi kwa kuhifadhiwa. Pia sababu za kukataliwa kwake kujiunga na Jeshi zitaainishwa katika fomu ya Polisi namba 31A ili endapo ataomba tena kuajiriwa na Jeshi taarifa zake zipatikane.

Kuacha Mafunzo

10. Iwapo kuruta anataka kuacha mafunzo kwa sababu Fulani wakati wa mafunzo, ataruhusiwa kufanya hivyo. Iwapo kuruta anaacha mafunzo ya kajeshi katika hatua za awali, sababu za kuacha
mafunzo zitarekodiwa katika Fomu ya alama za vidole (Fomu ya Polisi namba 31A), pamoja na
mapendekezo endapo anaweza au hawezi kuajiriwa tena.Fomu hii, ikiwa imejazwa, itatumwa kitengo cha Uchunguzi.

Kufukuzwa Wakati wa Mafunzo

11. Iwapo kuruta amefukuzwa Jeshini wakati wa mafunzo ya awali, sababu ya kufukuzwa kwake zitaandikwa katika Fomu ya alama za Vidole(Fomu ya Polisi namba 31A), pamoja na mapendekezo endapo anaweza au hawezi kuruhusiwa kuajiriwa tena. Fomu hii, ikiwa imejazwa kikamilifu itatumwa kitengo cha Uchunguzi wa Makosa

Taarifa za Mwisho za kuhitimu Mafunzo

12. (a) Kabla ya kumaliza mafunzo ya awali ya kuruta. Mkuu wa Chuo ataitaarifu Makao Makuu ya
Polisi idadi ya kuruta waliopo kwa ajili kupangiwa vituo vya kazi. Maelekezo ya kupanga vituo
vya kazi yatatolewa na Makao Makuu ya Polisi.

(b) Baada ya kupata maelekezo ya kupanga vituo vya kazi, Mkuu wa Chuo,ataandaa utaratibu ufuatao:-

(i) Rejista za ajira zikiwa zimejazwa kikamilifu, zikihusisha taarifa za kupandishwa daraja na kituo alichopangiwa kuruta.

(ii) Kadi za kumbukumbu za ajira zikiwa zimejzwa kikamilifu, kama ilivyo katika aya ndogo ya (i); kadi moja itapelekwa Makao Makuu ya Polisi,pamoja na nakala moja ya Fomu ya Polisi namba 31A P.G.O.NO.54 *(inaendelea.)*

(iii) Rejista ya Ajira na Kadi ya Kumbukumbu ya Ajira zitumwe Makao Makuu ya Mikoa ambako kuruta wamepangiwa. Kamanda wa Mkoa atabaki na Kadi ya Kumbukumbu ya Ajira na kuituma Rejista ya Ajira katika vituo ambavyo kuruta wamepangiwa.

((iv) Karatasi ya vifaa vya Kijeshi iliyokamilika(Fomu ya Polisi namba 31D) na seti kamili ya sare na vifaa vyote vikiwa katika hali nzuri kulingana na vipimo vilivyoainishwa katika Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi Namba 172, vitagawiwa kwa kuruta kutoka Chuo vha Polisi kabla ya kupangiwa vituo vya kazi.

(v) Kuruta watalipwa mshahara kama inavyostahili. Madeni ya kantini na mesi ıswa kulipwa kabla ya kuondoka Chuoni.

(vi) Taarifa za mafunzo ziandaliwe katika nakala mbili kwa kila kuruta. Yaliyoandikwa

ndani ya taarifa hizo yajulikane kwa kila mhusika na nakala zote zitumwe kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa ajili ya kuzipitia na kutoa maelekezo yoyote kwa jinsi aonavyo inafaa. Baada ya Inspekta Jenerali kuipitia taarifa hiyo, itasambazwa kama ifuatavyo:-

Nakala halisi:- Itawekwa katika jalada la mtumishi lililopo Makao Makuu ya Polisi.

Nakala:- Itatumwa kwa Kamanda wa Mkoa/Kikosi ambako kuruta amepangwa kwa kuipitia na baadaye itapelekwa kwa Mkuu wa Kituo au Kitengo alichopangwa na kisha itawekwa kwenye jalada binafsi la mtumishi.

Kumbuka:- Mkuu wa Chuo ataandika katika taarifa hiyo akieleza Mkoa alikopangiwa mtumishi huyo. Taarifa hii itajumuishwa katika sehemu ya “Maoni ya Mkuu wa Chuo kwa taarifa ya Makao Makuu ya Polisi”

(vii) ataandaa utaratibu wa kuwasafirisha Konstebo wote hadi Makao Makuu ya Mikoa walikopangiwa kufanya kazi, kwa maelekezo ya kuripoti kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa. Amri ya Kuondoka (Fomu ya Polisi namba 58) itatolewa kwa kuruta hao.Iwapo ataona ni muhimu,Mkuu wa Chuo atamjulisha Kamanda wa Polisi wa Mkoa kwa Simu ya upepo kuhusu tarehe ya askari kuondoka na tarehe wanayotarajia kuwasili mkoani.

Malipo

13. Kuruta atakapopandishwa daraja na kuwa Konstebo, kwa kawaida ataingia katika daraja la chini la ngazi ya mshahara wa konstebo, lakini ispekta Jenerali wa Polisi anaweza kumteua kuruta katika ngazi ya juu ya mshahara kutokana na sifa maalum alizonazo au utendaji kazi uliothibitishwa wa siku za nyuma.

P.G.O - 55
KUONGEZA NA KUSITISHA MKATABA

Kuongeza Mkataba

1. Taratibu za kuongeza mikataba kwa askari wenye masharti ya muda ya ajira ndani ya Himaya yatashughulikiwa na au kusimamiwa na Mkuu wa himaya husika, ambaye atapitia mkataba wa kila askari kabla ya kuidhinisha kuupitisha.
2. Taratibu za kuongeza mikataba kwa wote wanaohitaji ambao kuwamo kwao Jeshini ni kwa hiari, zitaongozwa chini ya Kanuni B.12.5 ya Kanuni za ajira ya Jeshi la Polisi
3. Askari wote ambao hawamo katika masharti ya kudumu ya ajira watachunguzwa afya zao na Daktari wa Serikali mwezi mmoja kabla ya kuomba kuongezwa mkataba na kuthibitishwa kuw a afya zao ni nzuri kumudu kazi za Polisi.
4. Askari ambao hawamo katika masharti ya kudumu ya ajira wanaoomba kuongeza mkataba wataweka saini katika fomu ya kuongeza mkataba (Fomu ya Polisi namba 190) . Zitaandaliwa fomu hizi katika nakala tatu na kukamilishwa na afisa anayeomba kuongezwa mkataba, Daktari na Mkuu wa Polisi wa sehemu husika ataidhinisha maombi hayo. Nakala moja ya mkataba itapelekwa Makao Makuu ya Polisi kwa kutangazwa katika Amri za Ute ndaji za Jeshi na kuwekwa katika jalada. Nakala zinazobakia zitawekwa katika Jalada binafsi la askari husika katika Makao Makuu ya Mkoa/Idara na Wilaya/Kikosi.
5. Wakuu wa Polisi katika maeneo husika wanawajibika wao wenyewe kutathmini kwa makini kumbukumbu za tabia na utendaji kazi wenye ufanisi wa askari wasio na masharti ya kudumu ya ajira kabla ya kuidhinisha maombi ya kuomba kuongezewa mikataba na kuhakikisha kwamba maombi ya kuongezewa mkataba yamepitishwa kwa kuzingatia vigezo vya msingi.
6. Wakuu wa Vituo na Vikosi wataomba kwa Makamanda ruhusa za kuwaongezea mikataba Askari wa Vyeo vya Chini mwezi mmoja kabla ya tarehe ya kuongeza mkataba na atajumuisha mapendekezo yake katika fomu ya mkataba pamoja fomu ya uchunguzi wa afya iliyokamilika.
7. Makamanda wa Polisi wanapaswa kuhakikisha kuwa askari wa Vyeo vya Chini ambao hawamo katika masharti ya kudumu wanakumbushwa kila wakati kuwa kuongezwa mkataba kunategemea tabia njema na ufanisi katika utendaji kazi.
8. Askari ambao hawamo katika masharti ya kudumu ya ajira na ambao hawana sifa za kuongezwa mkataba watasitishiwa kuongezwa mikataba muda utakapokwisha wa mkataba uliopo.
9. Taratibu zifuatazo zitafuatwa kwa Askari wa Vyeo vya Chini ambao hawana masharti ya kudumu ya ajira inapoonekana wamekosa sifa za kustahili kuongeza mkataba;

(a) Askari wa Vyeo vya Chini wasio na masharti ya kudumu ya ajira ambao haipendekezwi kuongeza mkataba watafahamishwa kimaandishi, miezi mitatu kabla ya tarehe ya mkataba wake uliopo kwisha; na

(b) Kama askari huyo ana nia ya kukata rufaa kupinga maamuzi kutoongezwa mkataba rufaa yake ya maandishi pamoja na taarifa ya

Kamanda wa Polisi wa Mkoa na maelezo mengine na kadhalika, yatapelekwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa uamuzi wa mwisho.

10. Askari wote wa Vyeo vya Chini wasiokuwa na masharti ya kudumu wanapaswa kuongeza mkataba kila baada ya kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

P.G.O. NO.55(inaendelea)

11. Chini ya kifungu cha 36 (1) cha Kanuni za Utumishi za Jeshi la Polisi Mamlaka ya Inspekta Jenerali wa Polisi yamekasimiwa kwa Makamanda.

Kufukuzwa Kazi

12. Kufukuzwa kazi kwa askari wasio na masharti ya kudumu ya ajira kwa sababu zozote tofauti na muda wa mkataba kuisha zinahitaji kuidhinishwa na Inspekta Jenerali wa Polisi kufukuzwa kazi hakutatekelezwa mpaka idhini kutoka kwa Inspkta Jenerali imepatikana.

13.Katika mazingira yote ambayo kanuni namba 38 ya Kanuni ya ajira ya Jeshi la Polisi itatumika,Makamanda watawasilisha mapendekezo yao kwa Inspekta Jenerali kwa kuidhinishwa.

14.Taarifa za kufukuzwa kazi zitajumuishwa katika marejesho na kutangazwa katika Amri za Utendaji za Jeshi.

Taratibu za Kuachishwa kazi katika kituo

15. (a) Endapo Kamanda anapendekeza kumuachisha kazi askari wa Cheo cha Chini, chini ya masharti yaliyoyopo katika kanuni namba 38 (2)(b) ya Kanuni ya Utumushi ya Jeshi la Polisi, 1995, ataliwasilisha jambo hilo kwa Daktari wa Wilaya ambako askari huyo anafanya kazi na kupata taarifa ya Daktari ikionyesha kama afya yake inaruhusu au hairuhusu kuendelea na kazi. Taratibu hii itatumika kupata taarifa kwa mtumishi ambaye anaweza kuwa na sifa za kulipwa fidia chini ya sheria ya fidia kwa wafanyakazi isipokuwa tu kama kuna sababu za msingi zitakazohitaji Bodi kukutana.

(b) Taarifa ya Daktari itawasilishwa kwa Inspekta Jenerali kwa Uamuzi.

(c) “Daktari wa Serikali” maana yake ni Daktari aliyesajiliwa, kwa maana alitangazwa katika gazeti la Serikali kuwa aliyefuzu kufanya kazi Tanzania.

16. (a) Iwapo mtumishi wa Jeshi asiye na masharti ya kudumu ya ajira atafukuzwa kwa sababu yoyote Mkuu wa Kituo atachukua hatua zifuatazo:-

Sare na Vifaa vya Jeshi- Mali zote za Serikali, vifaa vya Jeshi na vifaa vya bohari alivyokuwa amekabidhiwa vitakusanywa. Mali za Kituo au Kikosi alizokuwa amekabidhiwa kwa muda zitarudishwa kituoni au Kikosini.Mali zilizo salia (kwa maana ya, sare za kazi na vifaa vya Jeshi alivyokabidhiwa) vitarudishwa Makao Makuu yaMkoa yaliyokaribu au Bohari iliyo idhinishwa ambako vitahifadhiwa.

(b) Nyaraka:-Atakamilisha nyaraka zote muhimu zinazohitajika kwa mtumishi kufukuzwa kazi na kufukuzwa huko kujulikane rasmi. Nyaraka zilizokamilishwa, Jalada binafsi la mtumishi(na kwa askari wa upelelezi na askari kanzu,kadi za kumbukumbu za wahalifu) kisha vitatumwa Makao Makuu ya Polisi kwa ajili kuweka kumbukumbu.

Zingatio-Umakini wa pekee utazingatiwa katika mambo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha fomu ya polisi namba 31A(fomu ya alama za vidole).

(ii) Rejista ya utumishi.

(iii)Shahada ya kuachishwa kazi

(iv) Hati ya kusafiria.

Hati ya Kuachishwa kazi

17. (a) Hati ya kufukuzwa/kuachishwa kazi(fomu ya Polisi namba 33) itatolewa kwa afisa mwenye cheo chini ya ngazi ya Mkaguzi Msaidizi wa Polisi baada ya kufukuzwa. Hati ya kufukuzwa kazi haitatolewa kwa kuruta waliofukuzwa wakiwa katika kipindi cha uangalizi cha mafunzo katika Chuo cha Polisi.

P.G.O. NO.55(inaendelea)

(b) Hati ya kufukuzwa kazi (Fomu ya Polisi namba 33) itaandaliwa na afisa aliyehusika katika taratibu za kufukuzwa kazi.Hati iliyokamilika itakabidhiwa kwa mtumishi mwenyewe kabla hajaondoka.

(c) Endapo mtumishi anastahili kulipwa malipo ya bakhshishi, afisa aliyehusika katika kutekeleza kufukuzwa kazi kwa mtumishi atahakikisha kuwa anaweka kumbukumbu za anuani itakayotumiwa na mtumishi aliyefukuzwa (Namba za Sanduku la Posta zisikubaliwe). Jambo hili lina umuhimu mkubwa, na umakini wa hali ya juu unapaswa kuchukuliwa katika kuhakikisha kuwa anuani ya mtumishi ya siku za usoni imehakikiwa na kuhifadhiwa kwa usahihi. Kwa anuani za maeneo ya vijijini zitajumuisha kijiji, mahakama ya mwanzo, kiongozi wa Kata na kadhalika. Re jista ya utumishi na nyaraka nyingine binafsi za mtumishi aliyefukuzwa zitatumwa haraka iwezekanavyoMakao Makuu ya Polisi.

18.Hati ya kufukuzwa kazi itatolewa bila ya kufutwa au kubadilishwa na wote wanaopewa wataonywa kwamba kubadilishwa au kufutwa kwa hati hiyo kutapelekea kuwa batili. Pia wataonywa kuwa hati itakayokuwa imebadlishwa kwa kuongeza maneno ni kosa la jinai linaloweza kumfanya ashitakiwe mahakamani.

19. Hati za kufukuzwa kazi ambazo hazijatumika zihifadhiwe sehemu zenye usalama kwa kufungiwa kwa kufuli.

20. Iwapo N.C.O au Konstebo ameachishwa kwa sababu za kiafya, aina ya ulemavu/ugonjwa inapaswa kuongezwa kwenye sababu za kuachishwa kazi katika hati ya kuachishwa kazi, isipokuwa katika mazingira ambayo haitakuwa kwa maslahi ya mtumishi nyongeza ya sababu hizo hayatafanywa.

Tathmini ya tabia baada ya kuachishwa kazi

21. (a) Madhumuni ya kutoa cheti cha Tabia ni kumsaidia mtumishi kupata ajira katika maisha yake binafsi na kanuni za kuzingatia katika kufanya tathmini ya tabia ni kwa kungalia kumbukumbu zake alipokuwa askari Polisi. Hivyo afisa anayefanya tathmini ni sharti aandae cheti katika mazingira ambayo yatampa ukweli halisi mwajiri mwingine anayetaka kumuajiri mtumishi huyo.

(b) Nafasi ya mtimishi aliyekuwa Polisi kufanikiwa kapata ajira nyingine itategemea namna tathmini ya tabia yake ilivyofanyika. Hivyo ni wajibu wa afisa anayefanya tathmini ya tabia, kuhakikisha tahadhari ya hali ya juu inachukuliwa kwa kila tathmini inayofanywa kwa tahadhari na kuzingatia haki.Maneno yafuatayo ndiyo yatakayotumika:-

(i) Ya kuigwa/Mfano
(ii) Nzuri sana
(iii) Nzuri
(iv) Wastani

5. Kama atahitajika mtafsili, atatoa tafsiri yake ya mambo yaliyotokea katika Gwalide la utambulisho ushahidi huo utakuwa ule unaohusiana na uwepo wake katika gwalide hilo la utambulisho kwa tarehe hiyo na alikuwa mtafsiri kwa pande zote mbili za watuhumiwa na mashahidi.

Uangalifu utafanyika kuhakikisha kuwa hakuna madhara yoyote yatakayotokea wakati wa gwalide hilo la utambulisho.

PGO - 233

UPELELEZI – WATU WALIOPOTEA

1. Endapo itapokelewa taarifa katika Kituo Polisi ya kupotea mtu, maelezo kamili ya mazingira na maelezo ya kina ya wasifu wa mtu huyo lazima yapatikane. Kumbukumbu ya taarifa hiyo itaingizwa katika Kitabu cha Ripoti.

2. Kama hakuna sababu ya kushuku kuwepo kwa jambo baya,ni wajibu wa

maafisa wote waliopo zamu kujulishwa kumtafuta mtu huyo aliyepotea. Uchunguzi wote lazima ufanyike pia polisi watakuwa na mawasiliano ya karibu na ndugu wanaofahamika na marafiki marafiki wa aliyepotea.

3. Wakuu wa Vituo watachukua hatua zifuatazo kama mtu aliyepotea bado hajapatikana baada ya masaa 48 kupita :-

(a) Kuingiza maelezo kamili ya mtu aliyepotea, katika nakala tatu, katika daftari ya watu waliopotea na wanaotafutwa(PF 179). Nakala ya juu itaachwa katika Daftari kwa ajili ya kumbukumbu; nakala ya pili na ya tatu zitaondolewa na kubandikwa kwenye ubao wa matangazo wa kituo na wa utawala kwa ajili ya kuwapa taarifa askari na wananchi kwa ujumla.

(b) Tuma simu ya maandishi kuhusu mtu aliyepotea kwa Ofisi ya Upelelezi wa Jinai Mkoa, na Vituo vyote vya Polisi ndani ya Mkoa ambavyo vinaweza kusaidia katika kumtafuta mtu aliyepotea. Simu ya maandishi itaanzia na herufi 'MPT', ikifuatiwa na nambari ya utangulizi ya maelezo ya mtu aliyepotea kama ilivyo katika kumbukumbu ya daftari la waliopotea na wanao tafutwa. Mkuu wa upelelezi wa Jinai Mkoa atawajibika kusamabaza taarifa hizo nje ya mkoa kama akiona ni muhimu.

4. Wakuu wa vituo ambao wanapokea simu ya maandishi kuhusu mtu aliyepotea(rejea aya ya 3. (b) hapo juu) atanakili nakala tatu ya yaliyomo katika simu hiyo, katika daftari la kituo la watu waliopotea na wanaotafutwa, kasha ataondoa nakala mbili na kuzibandika katika ubao wa matangazo wa kituo na wa ofisi za utawala(rejea aya ya 3 (a) hapo juu). Kisha nao watachukua hatua zote zinazowezekana kumtafuta mtu aliyepotea.

5. Mkuu wa kituo ambaye amempata mtu aliyepotea atamtumia simu ya upepo au ya maandishi kumjulisha Mkuu wa Kituo aliyesambaza awali kwa njia ya simu ya maandishi taarifa za kupotea kwa mtu huyo. Kisha Mkuu huyo wa kituo aliyesambaza taarifa hizo awali atawajulisha wakuu wote wa vituo aliowasambazia taarifa hizi kuhusu kupatikana kwa mtu huyo, na ataingiza katika ukurasa husika wa daftari la Waliopotea na Wanaotafutwa kwamba mtu huyo amepatikana.Kisha ataziondoa nakala mbili za PF 179 kutoka kwenye ubao wa matangazo wa kituo na wa utawala na kuziteketeza.

6. (a) Wakuu wa Vituo wanaopokea taarifa za mtu aliyepotea watafanya juhudi zote zinazowezekana kupata picha kwa ajili ya kusambaza katika Vituo vile ambavyo vilitumiwa simu ya maandishi kuhusu mtu aliyepotea (rejea aya ya 3. (b) hapo juu).

(b) Wakuu wa Vituo ambao wamepata picha ya mtu aliyepotea wataituma kwa njia ya haraka iwezekanavyo moja kwa moja na Ofisi/maabara ya kiuchunguzi, akiambatanishwa na nakala ya simu ya maandishi kuhusu mtu aliyepotea ambayo itanakiliwa kwa vituo vyote vilivyosambaziwa simu hiyo awali.

(c) Kamanda wa Ofisi/maabara ya Kiuchunguzi atatuma nakala tatu za picha kwa kila kituo kilichonakiliwa simu husika.

(d) Kila Mkuu wa Kituo ambaye amepokea picha ataibandika nakala moja ya picha katika ingizo la daftari la Waliopotea na Wanaotafutwa na kasha nakala mbili zilizobakia atazibandika katika mbao za matangazo za kituo cha Polisi na Jengo la Utawala.

7. Watoto waliopotea na kukutwa na polisi watatunzwa kituoni mpaka anayemtafuta atakapoonekana. Kama anayemtafuta mtoto huyo hatatokea baada ya saa 24 kupita itatumwa simu ya maandishi kwa vituo vyote vya polisi vya jirani.Kama hata baada ya saa 48 kupita, mtu anayemtafuta mtoto huyo atakuwa hajatokea taarifa itatumwa kwa Mkuu wa Wilaya.

8. Wakuu wa Vituo wataziondoa fomu za daftari la Waliopotea na Wanaotafutwa (rejea PF 179 juu) kutoka mbao za matangazo za vituo vya Polisi na na majengo ya Utawala baada ya kupita mwezi mmoja tangu zilipobandikwa, vinginevyo zitabakia hapo kwa muda mrefu zaidi endapo wataona kuwa ni muhimu.

9.Daftari la Walipotea na Wanaotafutwa litatunzwa kwa uangalifu na usahihi na litakaguliwa katika kaguzi zote.

KITENGO CHA UKAGUZI WA MATUKIO YA UHALIFU

1. Kitengo cha ukaguzi wa matukio ya Uhalifu kipo chini ya Kikosi cha Forensic Bureau ambacho kinafanyakazi ya uchukuaji,utunzaji na uchunguzi wa alama za vidole katika eneo la tukio la uhalifu.

2. Kitengo hiki kinahifadhi kumbukumbu za alama za vidole za wahalifu sugu ambao wamehukumiwa kwa makosa mbalimbali ya kuwania mali.

Alama za vidole zinazopatikana au kupokelewa kutoka eneo la tukio zitachunguzwa na kulinganishwa na alama zingine za wahalifu zilipo kwenye kumbukumbu na kulinganishwa na zile zilizopatikana katika eneo la tukio.

3. .Makosa ya uvunjaji na makosa mengine makubwa yanaporipotiwa kwa mujibu wa kanuni za polisi kifungu cha 311, aya ya 3 afisa mkaguzi wa tukio mara anapogundua kuna uwezekanao wa kupata alama zozote ambazo zitasaidia katika upelelezi wa tukio mara moja amjulishe mkuu wa upelelezi wa mkoa kwa hatua zaidi.

4. Mkuu wa upelelezi wa Mkoa atafanya yafuatayo:-

(a) kutokana na aya ya 3 ya kanuni ya jeshila la polisi kifungu cha 224 Mkuu wa upelelezi wa mkoa atakagua eneo la tukio.

(b) Kutokana na aya ya 5 ya kanuni hii Mkuu wa upelelezi wa mkoa ataandaa namna ya uchukuaji wa vielelezo hivyo.

(c) Mujibu wa aya ya 6 ya kanuni hii vielelezo ambavyo haziwezi kuhamishika kupelekwa mahabara kwa ajili uchunguzi vitapigwa wataalum kutoka ofisi ya mkuu wa upelelezi wa mkoa picha na zitatunzwa kama vielelezo.

(d) Endapo vielelezo hivyo zitashindika kuchukuwa au kupigwa kutokana na uhaba wa rasilimali watu na vifaa

) Mkuu wa upelelezi wa Mkoa atamjulisha haraka iwezekanavyo Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kwa msaada wa wataalum kutoka kitengo cha ukaguzi wa matukio.

Uwasilishaji wa vielelezo

5. Kwa vielelezo vyote ambavyo zitahusishwa na alama za vidole isipokuwa vile ambavyo havihamishiki na vyenye kuchukua nafasi kubwa ubebaji zitapelekwa kitengo cha matukio kwa uchunguzi na ulinganifu kwa:-

(a) Vitapangwa kwa mujibu wa ukurasa wa 14 -20 cha British Home Office pamphlet''Notes on Finger and Palm prints ambayo hutolewa na kitengo hicho.

(b) hati ya polisi Namba 118 hujazwa kwa ukamilifu

(c) hati hiyo itajazwa kwa ukamilifu ili kutokupoteza uhalisia wa kielelezo

(d) ikijumuisha na alama za vidole PF 14A vy a watu ambao wanauhalali wa kugusa vielelezo na alama za vidole vya watuhumiwa wanaofahamika

(e) Hati zote zitatumwa chini ya uangalizi wa askari polisi

Mkaguzi wa tukio au mchukua picha kutoka ofisi ya mkuu wa uplelezi wa mkoa

6. (a) Ataandika kila kitu alichokiona kwenye eneo la tukio kwenye kitabu cha matukio cha Polisi namba 129

(b) Kila kesi itaonyeshwa kwa mpangilio wa namba zinazofuatana kwa mwaka kwa kutumia vifupisho vya mkoa kwa mfano N.R/F.P/1.62

(c) Kila kielelezo kitachopatikana katika eneo la tukio la uhalifu kitapewa herufi ya pekee itakayofuatiwa na namba ya kesi kama ilivyoonyeshwa kwenye kipengele b kwa mfano N.R./F.P./1/62/A- N.R./P.P./1/62/B.Mrejesho huu utakuwa umeandikwa kwa usahihi na kwa wino na kubandika kwa kielelezo karibu na eneo la mwisho la kielelezo. Alama ya kielelezo itachukuliwa na mpiga picha inapowezekana na picha ya mwenye alama hizo

(d) .Pale kielelezo kinapokuwa kikubwa na hakihamishiki kitapigwa picha na mpiga picha pande zote ili kuonyesha

) mahali kilipokuwepo.

(e) Alama zitapigwa picha kulingana na maelekezo ya mtaalamu wa alama za vidole

(f) Mikanda ya picha au vivuli vyake vitatumwa Idara ya upelelezi ya uchungu wa polisi kwa kuwekewa kumbukumbu namba au kwa kusindikizwa na polisi pamoja na P.F 118 iliyojazwa kikamilifu kwa alama za vidole kwa walioshika kilelezo hicho(P.F 14A) pale inapojulikana na T.C.R.O namba na majina au alama za vidole watiwa mashaka

Hatua zinazochukuliwa na Idara ya upelezi ya uchukunguzi katika eneo la uhalifu

7. Kitengo cha matukio kitazipokea vielelezo, mikanda ya picha au vivuli vya vielelezo ambavyo vilizochukuliwa kwenye eneo la tukio

(a) Atasajili kila kilelezo cha kesi kwenye P.F 129 nakuvipa namba zinazofuatana kwa mwaka

(Mara baada ya uchunguzi na ulinganifu na kuzitoa zisizohusika na kuzirudisha kwa mkuu wa upelelzi wa

b mkoa husika

)

Ulinganifu wa kila siku wa alama za vidole wa Idara ya uchunguzi wa makosa ya Jinai

8. All finger print forms (P.F. 14B) of criminals charged or convicted of breaking and kindred offences after routine search in the Main Collection will be passed to the Scenes of Crime Section for comparison with impressions found at scenes of crime.

Hati zote za alama za vidole P.F.14B za wahalifu walioshitakiwa au kuhukumiwa kwa makosa ya uvunjaji nay a kifamilia baada ya uchunguzi na kukusanywa kutoka eneo la tukio la uhalifu kwa ulinganifu wa alama za vidole zilizopatikana katika eneo la tukio la uhalifu

Action by Scenes of Crime Section on Identification of Impressions

Hatua zinazochukuliwa na kikosi cha matukio katika ugunduzi wa alama

9. Wakati utambuzi umefanywa wa alama za vidole au baada ya kukusanywa kutoka eneo la uhalifu mkuu wa kituo na mkuu wa upelelezi wa mkoa atajulishwa kwa simu. Na endapo mtuhumiwa atatambuliwa kwa kutenda kosa ambayo ipo katika himaya yake ya kiwilaya mkuu wa upelelezi wa wilaya au mkoa watajulishwa.

Hatua mabazo zitachukuliwa baada ya mtuhumiwa kukana kutambuliwa

10. (a) Wakati mtuhumiwa akikana kosa alilotuhumiwa mkuu wa kituo atafanya:-

(i) Atawaomba kitengo cha wataalam wa uchunguzi ili kundaa chini ya kifungu cha 154 (b) cha sheria ya makosa ya mwenendo wa jinai sura ya 20 kama ilivyofanyiwa mapitio upya mwaka 2002

(ii) submit on finger print form (P.F. 14B) two sets of accused's finger prints (care must be taken to ensure that the officer taking these prints will later be available to give evidence at the Court proceedings).

(b) The O/C. Forensic Bureau will instruct an expert to prepare the report and forward it to the O/C. Station concerned, together with the exhibit(s), if any, and the P.F. 14B of the accused.

Proving Expert's Report and Exhibits in a Case

11. (a) To prove an expert's report, it is necessary to prove first the exhibits, then the finger print form (P.F. 14B) after which the report may be put in as evidence.

(b) The Court or accused may wish to call the expert who signed the report. In this event the O/C. Station concerned

will request an adjournment in order to arrange with the CO. Forensic Bureau a date when the expert will be available to give evidence.

Action by O/C. Station – Result of Case

12. In every case where identification has been made, the result of the prosecution will be sent to the CO. Forensic Bureau quoting the F.P. Number.

Safe Custody of Exhibits

13. All exhibits bearing unidentified impressions will be retained in the scenes of crime Section for two years.

14. Valuable articles such as silver plate, etc., or articles which the complainant specifically requires will be returned to the station on request. An entirety photograph will be taken prior to dispatch.

UCHUNGUZI - MAELEZO

1. (a) Kila askari ana mamlaka chini ya kifungu 32 (3) cha sheria ya Jeshi la polisi na Polisi Wasaidizi Sura 322 kama ilivyorejewa mwaka 2002 kuwa askari polisi yeyote anamamlaka ya kuchukua maelezo toka kwa mtu yeyote ambaye kuna sababu ya kuamini kuwa anauelewa wa kusaidia upelelezi

(b)taratibu za kuhifadhi imeainishwa sehemu ya IIB ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20.

© askari polisi kabla ya kuchukua maelezo atajieleza jina lake, cheo na kituo chake cha kazi.

SEHEMU YA I

KUCHUKUA MAELEZO YA SHAHIDI

2. Maelezo yote yanayochukuliwa na polisi yatachukuliwa kwenye PF2A kama ifuatavyo:-

   Tarehe, muda na mahali.

   Maelezo…….(jaza jina)

   Kazi…….

   Makao……..

   Utaifa/kabila……..

   Dini……

   Umri…….

   MAELEZO; Uthibitisho chini ya kifungu 34B(2) (c) cha Sheria ya Ushahidi namba 6 ya mwaka 1967 kama ilivyorejewa mwaka 2002 kama ifuatavyo;

   Maelezo haya (yananihusu…….na kusainiwa na mimi) ni ya kweli kwa kuelewa na ufahamu wangu, na ninaelewa ya kuwa endapo yatahitajika kama ushahidi, nitawajibika kwa lolote ninaloliamini kuwa nila uongo au sio la kweli.

   Yamefanyika……..tarehe……siku ya …….

   Saini ……..

   Yanapochukuliwa maelezo ya mtu wan chi za nje hasa hati ya kusafiria ,visa, hati ya makao na hati zingine za Uhamiaji

zitaandikwa.

3. Isiachwe nafasi au misitali wakati wa kuchukua maelezo ya mtu na afisa anayechukua maelezo. Maelezo ya kila shahidi yatachukuliwa kwa kutenganisha kwenye PF2A sehemu zote zitatumika lakini maelezo ya tachukuliwa na kuandikwa namba.

4. Kila maelezo ikiwezekana yajumuishe;

(a) Shahidi kwa kulizwa maswali, tarehe muda na mahali na kama aliona, alifanya nk na nani alikuwepo.

(b) Shahidi ……..hatua gani alichukua, matokeo ya tukio nk, mfano alimfukuza mtuhumiwa, kumpa nafasi na kusaidia kumwita kwa msaada

(c) Mambo yote yanayohusiana na tukio

(d) Uelewa wa nguma wa shahidi juu ya vielelezo

(e) Uelewa wa nguma wa shahidi juu ya shahidi kama yupo

(f) Uelewa wa nyuma wa mashahidi wengine n.k., mahusiano kama yapo

(g) Ushahidi unaofanana au kupingana

5. Maelezo yanapochukuliwa zaidi ya ukurasa mmoja mutu atasaini pembezoni kushoto kwa kila karatasi

6. (a) kila maelezo yataishia kwa:-

   “Maelezo yamesomwa na ni sahihi”

   Uthibitisho utakuwa mwisho wa maelezo mara baada ya kumaliza. Sahihi ya mchukua maelezo itakuwa upande wa kushoto ikiwa ni pamoja na jina lake namba na cheo vitanyeshwa kwenye hiyo karatasi ya maelezo. Sahihi ya mchukuliwa maelezo itakuwa upande wa kulia. Kama shahidi alikuwepo wakati wa kuchukua maelezo, basi mashahidi sahihi zao zitafuatia mwisho.

   Mkalimani

   (b) anapotumika basi atasaini mwisho wa maelezo na lugha iliyotumika ielezwe

   (C) endapo mutu anayechukuliwa maelezo hajui kusoma

wala kuandika alama za vidole zitatumika.

(d) afisa nayechukua maelezo atahitimisha umuhimu na uthamani wa shahidi

(e) maelezo yatachukuliwa kwa kiingereza au Kiswahili. Endapo maelezo ya lugha zaidi ya kiingereza yatatumika basi yatatafsiriwa kwa kingereza na jalada litatumwa kwa Mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai

(f) ionyeshwe tarehe na muda wa maelezo pembezoni mwa msitari

SEHEMU YA II

KUMUHOJI SHAHIDI AMBAYE AMEHUSISHWA

Kama afisa wa polisi anapomhoji mtuhumiwa ambaye amehusika kwenye kosa chini ya upelelezi mara moja aache kumhoji amjulishe mtu huyo kwamba ni mtuhumiwa kwa hatua hizi;

(a) Endelea kumhoji kama ilivyofafanuliwa sehemu ya nane hapo chini

(b) Anaweza akamuuliza zaidi kwa utashi wake

KUCHUKUA MAELEZO TOKA KWA MTUHUMIWA

8 (a) Afisa wa polisi wakati wa kuchukua maelezo ya shahidi anapofikia ufumbuzi kwamba mtu huyo ametenda kosa lakini kosa haliko wazi basi ataacha na atamhoji kwa maneno yafuatayo;

“ ni wajibu wangu kukuonya kwamba chochote utakachosema kitaandikwa na kitatumika kama ushahidi”.

Aelezwa kama atatoa maelezo yake kwa hiari afisa wa polisi atachukua maelezo mara moja kama ifuatavyo “ nimeonywa na ……kwamba silazimishwi kusema chochote isipokuwa kwa utashi wangu endapo nitasema chochote kitaandikwa na kuweza kutumika kama ushahidi”.

Ataendelea kuchukuliwa maelezo yatakayochukuliwa kwa maneno ya mtuhumiwa.

(b)Afisa wa polisi atakapojiridhisha kumshtaki kwa kosa hilo ataacha kuchukua maelezo na atamshtaki kwa lugha nyepesi na kumhoji kwa maneno yafuatayo;

Unalolote lakujibu kuhusiana na shtaka hili? Hulazimishwi kujibu lolote isipokuwa kwa hiari yako, lakini ulisemalo lolote litanukuliwa na kutumika kama ushaidi ©Mashtaka na onyo vitaandikwa yanapochukuliwa kama ifuatavyo;

“Ninashtakiwa kwa ……(kosa) na nimeonywa na ……(askari polisi cheo, na jina) kwamba silazimishwi kusema lolote isipokuwa kwa hiari yangu na lolote nitakalosema litaandikwa na kutumika kama ushahidi”

(d)Ndipo mtuhumiwa atatoa maelezo yake na askari polisi atayaandika.

SEHEMU YA III

KUCHUKUA MAELEZO KUTOKA KWA ALIYEKAMATWA NA MTUHUMIWA

9. Askari Polisi aliyeko kazini nje ya kituo chake atakapokuwa anamleta mtuhumiwa atamwelekeza sababu ya kumkamata na kumtahadharisha kwa maneno yafuatayo: “Mimi ni askari Polisi hulazimiki kusema chochote lakini lolote utakalosema litatumika kama ushahidi”

10. Afisa wa Polisiataandika kitakachosemwa na mshtakiwa katika kitabu chake cha kumbukumbu.

11. Mtuhumiwa atakapofikishwa kituoni, Afisa wa Poliai atakapoamua kabla ya kuchukua maelezo awe na ushahidi wa kujitosheleza kuandaa mashtaka. Atamshtaki mtuhumiwa na kumtaarifu kosa lake kwa lugha inayoeleweka na kumtahadharisha kwa maneno yafuatayo;-

“Unataka kusema lolote kuhusiana na shtaka lako? Hulazimishwi kusema lolote isipokuwa kama utasema kwa hiari yako, lakini lolote utakalosema litaandikwa na litachukuliwa kama ushahidi.

12. Mtuhumiwa atakapokuwa amekubaliana kutoa

maelezo, Afisa wa Poloisi ataandaa mashtaka na onyo katika karatasi ya maelezo kama ifuatavyo;_

" Nimeshtakiwa ……..(kosa) na nimeonywa nisiseme lolote isipokuwa nitakapohiyari, lakini lolote nitakalosema liataandikwa na kuchukuliwa kama ushahidi"

Afisa wa Polisi ataandika maelezo ya mtuhumiwa atakayosema.

13. Hakuna mazingira yoyote mtuhumiwa atakayohojiwa katika chumba cha siri.

Sheria za kuandika maelezo ya onyo

14. Kulingana na kifungu 53 cha mwenendo wa makosa ya jinai, mtu aliyechini ya ulinzi, Afisa wa Polisi asimhoji swali lolote, au asimtake kufanya lolote kwa madhumuni ya kuunganisha na upelelezi wa kosa isipokuwa;

PGO - 237

UPELELEZI – KESI ZINAZOENDELEA MAHAKAMANI.

1. Upelelezi hautafanyika pale ambapo taarifa ya lalamiko kwamba kuna kosa limetendeka na kwamba linahusiana na mambo yaliyojitokeza kwenye mwenendo wa kesi inayoendelea mahakamani.

2. Taarifa hizo zote zitapelekwa kwa utaratibu uliosahihi kwa

mkuu wa polisi wa wilaya, ambaye pia atapata ushauri kutoka kwa mahakama inayohusika na mienendo ya kesi hizo au kutoka kwa mkurugenzi wa mashitaka kupitia kwa mkurugenzi wa makosa ya jinai kama upelelezi ufanyike au usifanyike.

3. Kifungu cha 102 hadi 114A sura ya xi ya kanuni ya adhabu, sura ya 16 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002 ni makosa yaliyoainishwa yamo ndani ya upana wa amri au utaratibu huu.

PGO – 238

UCHUNGUZI- WATU WANAOTAFUTWA

Mtu anayetafutwa ni mtu yeyote ambaye bila shaka anatuhumiwa kuhusika katika kosa na waraka wa kumukamata umetolewa.

USAJILI NA UCHUKUAJI WA MAELEZO YA MTU ANAYETAFUTWA

Mkuu wa kituo ambacho kimepokea taarifa ya kwanza ya kosa la mtu anayetafutwa, atachukua hatua zifuatazo mara tu mtuhumiwa atakapotambulika au pale maelezoya kutosha yatakapopatikana ndani ya muda usiozidi masaa 48 baada ya hati ya kumkamata kutolewa.

Kuitumia hati ya ukamataji

Kuingiza maelezo kamili ya mtuhumiwa na kosa na sababu ya kutenda kosa kwa kutumia kichwa cha habari kilicho sahihi katika rejesta ya “watu waliopotea na wanaotafutwa” FP 179. Nakala ya kwanza itahifadhiwa kwenye rejesta, nakala ya pili

itabandikwa kwenye ubao wa matangazo ulioko kituoni na nakala ya tatu itapelekwa kitengo cha uchunguzi.

Kuingiza maelezo kamili katika FP 10 na kuipeleka katika serikali za mitaa katika wilaya.

Kutuma simu ya taarifa ya mtu anayetafutwa katika kitengo cha uchunguzi, makao makuu ya upelelezi mkoa na vituo vyote vya polisi vilivyopo mkoani ambavyo vinaweza kusaidia upatikanaji wa mtuhumiwa. Simu hiyo itaanzia na herufi “WPT” ikifuatiwa na namba ya tukio ikitoa taarifa za mtuhumiwa kama zilivyoandikwa kwenye rejesta. Kama namba ya TCRO inajulikana, pia itanukuliwa. Orodha ya vituo vya polisi vilivyopo na kupewa taarifa, vitaingizwa kwenye rejesta. Afisa wa upelelezi wa mkoa atawajibika kusambaza taarifa hiyo nje ya mkoa pale atakapoona inafaa.

Mkuu wa kituo atakayepokea “WPT” atafanya yafuatayo:-

Ataingiza taarifa za mtu anayetafutwa, kosa na sababu ya kutafutwa kwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa nakala tatu kwenye rejesta ya watu waliopotea na wanaotafutwa ambayo niFP179.

Nakala ya juu itaachwa kwenye rejesta ya watu waliopotea na wanaotafutwa.

Nakala ya pili itabandikwa katika ubao wa matangazo kituoni.

Nakala ya tatu itabandikwa katika ubao wa matangazo wa utawala.

Kuhakikisdha watu wote walikamatwa wanakaguliwa katika rejesta ya watu waliopotea na wanaotafutwa.

Mkuu wa kitengo cha uchunguzi anawajibika kutoa taarifa za mtu anayetafutwa katika chombo cha habari na gazeti la polisi. Maelezo yataandikwa nyuma kwenye kadi ya majina au kwenye picha ya mtu anayetafutwa.

PICHA YA MTU ANAYETAFUTWA

(a) Mtu anayetafutwa akishatambulika, harakati za kuweza kupata picha toka kwa marafiki zake, watu wanaomfahamu au kutoka nyumbani kwake.

Pale ambapo mtu anayetafutwa hajajulikana, lakini mlalamikaji au shahidi akiweza kutambua picha yake, afisa wa upelelezi atafuata taratibu zilizopo kwenye PGO namba 231 upelelezi - utambuzi kwa kutumia picha.

Picha ikipatikana itapelekwa haraka iwezekanavyo katika kitengo cha uchunguzi ikiambatanishwa na nakala ya simu ya mtu anayetafutwa ambayo inaonesha vituo ambavyo vimepewa taarifa

Kitengo cha uchunguzi kitapeleka picha ya mtu anayetafutwa katika vituo vyote vilivyopewa taarifa. Vituo vikipokea, vitaweka picha moja kwenye rejesta ya mtu anayetafutwa na picha nyingine itabandikwa kwenye ubao wa matangazo.

Kitengo cha uchunguzi kikipokea picha ya mtu anayetafutwa,

baada ya kuandaa kadi ya majina baadaye itatolewa na gazeti la polisi ikionesha nukuu toka kwenye kadi ya majina. Mkuu wa kituo akipokea picha ya mtu anayetafutwa, ataitoa na kuiweka nyuma ya kadi ya jina la mtu anayetafutwa ambayo aliipokea toka kitengo cha uchunguzi. Ikizingatia kipengele cha 4.

TARATIBU ZA UKAMATAJI WA MTU ANAYETAFUTWA

(a) Mkuu wa kituo, akipokea WPT ikimshauri juu ya ukamataji wa mtu anayetafutwa atafanya yafuatayo pale mtu anayetafutwa hahitajiki katika kituo kinachomkamata, atapanga askari kwa kuwasindikiza na kumtambua shahidi ambaye atawasilisha hati ya ukamataji wa mahaliambapo mtuhumiwa aliyekamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi.

(b)Pale ambapo WPT imehifadhiwa na inahitajika na zaidi ya kituo kimoja kwa makosa ya jinai, mkuu wa kitengo cha uchunguzi atamjulisha Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai ambaye atatoa maelekezo jinsi gani mashtaka yatasikilizwa.

(c)Pale ambapo WPT inatafutwa na kitengo cha uchunguzi na ikaonekana ipo:-

i. chini ya ulinzi wa Magereza.

ii. chini ya ulinzi wa polisi.

Mkuu wa kitengo cha uchunguzi atatuma taarifa vituo vyote vinavyohusika na kumjulisha Mkurugenzi wa Upelelezi wa

Makosa ya Jinai kwa kuchukua hatua zaidi.

TAARIFA YA KUKOMA KUTAFUTWA

Mtu anayetafutwa akiwa amekamatwa

Na kituo kingine ukiachilia mbali kituo kilichotuma WPT, mkuu wa kituo aliyepelekea ukamataji atamshauri kwa simu mkuu wa kituo kinachomtafuta mtuhumiwa. Taarifa hii itarudiwa kutumwa ktika kitengo cha uchunguzi ambacho kitasitisha utafutaji kwa kutumia gazeti la polisi.

Na kituo kilichoandaa WPT, mkuu wa kituo atashauri kitengo cha uchunguzi kwa kutumia simu ya upepo na kitengo cha uchunguzi kitasitisha utafutaji wa mtuhumiwa kwa kutumia gazeti la polisi.

Kila mkuu wa kituo anayepokea taarifa ya ukamatajai wa mtu anayetafutwa kama ilivyooneshwa katika kipengele cha 10 hapo ju, atasitisha uingizaji wa taarifa za mtu anayetafutwa katika rejesta kwa kuandika neno 2

PGO - 272

UKAMATAJI NA UPEKUZI

1. Sheria hii inahusu upekuzi wa haraka mara baada ya ukamataji kutoka masharti ya Sehemu ya 24 ya Sheria ya Makosa ya Jinai, Sura ya 20 yenye malekebisho ya mwaka 2002 ambayo imenukuliwa kama ifuatavyo:
   "Kila mtu aliyekamatwa-
   (a) na Ofisa wa Polisi chini ya hati ambayo haitoi dhamana,

au chini ya hati ambayo inatoa dhamana lakini mtu aliyekamatwa hawezi furnish dhamana; au

(b)bila hati au kwa mtu mwengine mwenye hati na mtu aliyekamatwa hawezi kupewa dhamana au hawezi kutimiza masharti ya dhamana kwa mujibu wa sheria,afisa polisi aliyefanya ukamataji au wakati wa ukamataji wa raia, afisa wa polisi atawajibika kwa raia huyo kuwa yeye ndie aliyemkamata anaweza kumpekuwa na kumweka chini ya ulinzi kwa mujibu wa sheria na kuhifadhi vitu vyote alivyomkutanavyo mtuhumiwa.

Maana ya kifungu hiki, wakati afisa wa polisi anapomkamata mtu yeyot kwa makosa madogo,mtuhumiwa asipekuliwe.Kwa wale waliokamata kwa hati ya mashitaka na kuhifadhiwa kwa ajiri ya taratibu za mashitaka wanaweza kupekuliwa.Taratibu za upekuzi katika kituo cha polisi inapatikana katika PGO 357

2. Kila mtuhumiwa ambaye alipekuliwa baada ya kukamatwa, atapekuliwa tena mara afikapo kituo cha Polisi.

3. Ni sera nzuri ya kuwa, wafungwa wa kiume kupekuliwa na afisa wa Polisi wa kiume isipokuwa hali ni kama kwamba hakuna afisa wa Polisi wa kiume wakati ukamataji unapofanyika.

4. Wafungwa wanawake watapekuliwa na police wa kike au mwanamke mwengine nje ya mbele ya umma na mali zao kukabidhiwa kwa afisa Polisi ambaye aliyewakamata .

TARATIBU ZA UPEKUZI

5. (a)Wakati afisa wa polisi anapotaka kumpekuwa mtuhumiwa,atamwambia kutanua miguu yake na anyooshe mikono juu ya kichwa chake.

(b)Afisa atasimama nyuma ya mtuhumiwa ili kuanza upekuzi.Hapaswi kumruhusu mtuhumiwa kutelemsha mikono yake wakati wa upekuzi.Afisa hatakiwi kusimama mbele ya mtuhumiwa wakati wa upekuzi ili kuzuia kutokushambuliwa.

(c)Upekuzi utaanzia kutoka kwenye kichwa kwenda hadi chini ya miguu,Kofia ya mtuhumiwa ndiyo ya kwanza kupekuliwa kama ipo, nywele zake , mdomo na mkoba wake.Upekuzi utaendelea juu ya nguo zake kwani anaweza kugundua kitu kilichofichwa kwa ndani,mwisho kama ni muhimu ampekuwe katika viatu na soksi pia.Upekuzi lazima

ufanyike kwa heshima na siyo mbele ya umma ikiwezekana katika kituo cha polisi au sehemu nyingine kama hiyo.

6. Afisa mwendesha upekuzi anatakiwa: -
(a) aweze kumiliki silaha yoyote, sumu, madawa ya kulevya, vibiliti au vitu vingine ambavyo vinaweza kutumika kama silaha;
(b) kuchukua na makini kuhifadhi vitu vyovyote au hati au mali izaniwayo ni ya wizi ambayo inaweza kuwa na uhusiano na kosa lolote;
(c) kuingiza kumbukumbu katika kitabu chake kinacho onyesha orodha sahihi ya mali zote alizopata toka kwa mtuhumiwa. Ahakikishe kuwa na afisa ambaye atamsaida kumlinda mtuhumiwa na orodha hiyo asifanye yeye pekee bila kuwa na afisa polisi mwingine ,hii kwa ajiri pindi mtuhumiwa anapotoloka.

(d)kutojimilikisha fedha au vitu vingine ambavyo ni mali ya mtuhumiwa isipokuwa kama ilivyoelezwa katika sehemu ya (a) na (b) hapo juu.

(e)kabidhi vitu vya mtuhumiwa kwa afisa wa chumba cha mashitaka ukiwa na mtuhumiwa katika kituo cha polisi kilicho karibu.

NAMNA YA UKAMATAJI WA WATUHUMIWA

7. (a)wakati wa ukamataji, afisa wa polisi atamgusa bega mtuhumiwa na kumfahamisha juu ya kosa lake , isipokuwa atakapo jisalimisha yeye mwenyewe kwa maneno au vitendo.

(b)kama mtuhumiwa anayetaka kukamatwa atakataa ukamataji kwa kutumia nguvu,atajaribu kuingilia ukamataji,afisa wa polisi atatumia njia zote za muhimu kuwezesha ukamataji.

(c)wafuatayo ni watuhumiwa wanaume wanaoweza kukamatwa kwa hati au bila ya hati ya kukamatia

(i)wale wote wakiyotenda makosa makubwa.

(ii)wale wahalifu wa hatari.

(iii)wale wanaojaribu kutoroka.

(d)kama afisa wa ukamataji hatapatiwa vifaa vitakavyo msaidia katika ukamataji, atatakiwa kuchukuwa tahadhari kubwa ili mtuhumiwa asimtoroke wakati anapompeleka kituo cha polisi. Siyo kwa mazingira yoyote atakayoweza kumwachilia isipokuwa mpaka wafike katika kituo cha polisi.

(e)vifaa vinavyo weza kumzuia mtuhumiwa

(i)pingu

(ii)mkanda mwili wenye pingu za chuma.

(iii) mkanda mwiliwenye kamba za ngozi.

(iv)kamba ya kifundo cha mguu.

(v)aina ya chuma cha kufungia miguu.

Kila kifaa tajwa hapo juu kitatumika kulingana na mazingira ya kosa na maelekezo toka kwa mkuu wa upelelezi wa makosa ya jinai.

MAKABIDHIANO YA WAFUNGWA

8. Baada ya kukamatwa na kupekuliwa, watuhumiwa watachukuliwa hadi kituo cha polisi kilichopo karibu na kukabidhiwa haraka iwezekanavyo. Mara moja baada yai kukabidhiwa kwa kituo cha Polisi wale ambao wanastahili dhamana wanapaswa kuwapa taarifa juu ya haki ya dhamana na waruhusiwe kuwasiliana na ndugu zao au wanasheria na kuwaeleza ukweli kwamba wao wapo katika kituo cha polisi baada ya kukamatwa . Hii ni kwa mujibu wa sehemu ya 54 ya Sura ya mwenendo wa makosa ya jinai 20 iliyofanyiwa malekebisho ya mwaka .2002 ambayo yanaeleza kwamba:

(1) Kwa mujibu wa kifungu kidogo (2), Afisa Polisi atatakiwa, kusikiliza maombi ya mtu ambaye yupo chini ya kizuizi, kumwezesha kuwasiliana na mwanasheria, ndugu au rafiki kwa uchaguzi wake.

(2) Afisa wa Polisi inaweza kukataa chini ya Kifungu kidogo (1) kutoa mawasiliana na mtu, jamaa au rafiki wa mtu ambaye yupo chini ya kizuizi, kama Afisa Polisi anaamini juu

ya misingi ya busara kwamba ni muhimu ili kuzuia mtu ambaye yupo chini ya kizuizi kuwasiliana na mtu wa nje kwa lengo la kuzuia: -

(a) asitoroke msahidizi wa mtu ambaye yupo chini ya kizuzini; au

(b) hasara, uharibifu au upotoshaji wa ushahidi kuhusiana na kosa. "

Hivyo tu kwa sababu za halali mawasiliano na mwanasheria au jamaa yanaweza kukataliwa kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 54 iliyonukuliwa hapo juu.

PGO – 273

BAADHI YA AYA ZINAKOSEKANA(ZIJAZWE)

10.Kama ndege itakuwa imeanguka katika mazingira tatanishi na ni mbali kutoka kituo cha ndege ni mhimu taarifa hizi zikafika katika kituo kikuu cha anga haraka iwezekanavyo, kama

(a) aina na alama ya usajili wa ndege

(b) uraia wa ndege

(c) jina la mmiliki au kukodiwa kwa ndege

(d) jina la rubani

(e) muda na saa ya ajali

(f) muda wa kuondoka kwa ndege

(g) muda uliodhaniwa kufika kwa ndege

(h) eneo lililogunduliwa kupotea kwa ndege

(i) idadi ya watu waliokufa

(j) idadi ya majeruhi

(k) taarifa kamili kuhusu kuanguka kwa ndege wakati ikipaa, ikiwa imepaa au inatua

(l) hali ya ndege

(m) maelezo ya hali ya ndege

(n) kama kuna moto umetokea ndani au nje ya ndege

(o) idadi ya wahudumu wa ndege

(p) idadi ya abilia

(q) hali ya hewa wakati ndege ikipata ajali

11. wakati taarifa zinatumwa kutoka chumba cha mawasiliano ni lazima kunukuu alama sahihi ikifuatiwa na taarifa kamili mfano “j” ikimanisha watu wanne wamejeruhiwa sana.

SEHEMU TA III

KUTAFUTA KWA NDEGE ILIYOPOTEA

12.Askari polisi yeyote atakayepokea taarifa kuhusu kupotea kwa ndege yeyoe atamjulisha kamanda wa polisi mkoa pasipo kuchelewa na kamanda wa polisi mkoa atafanya yafuatayo;

(a) atajulisha vikosi vyote katika himaya yake.

(b) ataamuru uchunguzi

(c) atamjulisha mkuu wa mkoa na mganga mkuu wa mkoa

(d) ataanza kutafuta ndege iliyopotea kulingana na taarifa alyoipata.

13. Kamanda wa Polisi atahakikisha taarifa zinasambazwa sehemu zote pia atapokea taarifa zote na kuzihakiki na kuzituma makao makuu ya polisi

14. Kamanda wa Polisi wa mkoa atahakikisha majeruhi wote waliopatikana wanahudumiwa mahitaji ya mhimu kama maji chakula matibabu na malazi na vitu vingine mhimu katika uhitaji wa wahanga hao. Pia atahakikisha kuwa wahanga wote wanakuwa katika mazingira mazuri ya hali ya hewa, pia atakuwa na ufahamu wa mambo yote yaloyotokea kama inavyoonesha kwenye jedwali “B”.

15. Maelezo na ratiba kuhusu mawasiliano ya anga na mifumo yake katika kuwasiliana moja kwa moja na kituo cha anga na kituo cha kitaifa cha uokoaji kilichopo Dar es salaam kama inavyoonesha kwenye jedwali”A”.

JEDWALI “A”

MAWASILIANO YA ANGA NA MIFUMO YA MOJA KWA MOJA NA MAKAO MAKUU YA UOKOAJI KILICHPO DAR ES SALAAM

DAR ES SALAAM	MTWARA
TABORA	MBEYA
TANGA	MOSHI
ARUSHA	SONGEA
DODOMA	MWANZA
IRINGA (NDULI)	

JEDWALI “B’

ALAMA ZA MAWASILIANO NA UTAFUTAJI WA NDEGE ARDHINI

IDADI	TAARIFA	ALAMA ZA ISHARA
1.	Operesheni imekwisha	LLL
2.	Tumepata watu wote	LL
3.	Tumepata baadhi ya watu	11/11
4.	Hatutaweza kuendelea na tunarudi kituoni	XX
5.	Tumegawanyika katika sehemu mbili kila kundi na eneo lake	
6.	Tumepokea taarifa kuwa ndege iliyopotea ipo uelekeo....	
7.	Hakuna kilichopatikana tunaendelea kutafuta	NN

Utafutaji wa ndege ardhini utategemea zaidi vifaa maalumu vya alama hapo juu. Hii ni nyongeza kwa radio zinazobebeka.

PGO - 274

APPENDIX "A"

(TO P.G.O. NO. 274)

MATUMIZI YA NGUVU

Lengo.

1. Kiambatanisho hiki kinampa ofisa chanzo cha rejea juu ya r
ya nguvu. This appendix provides officers with a source of r
on the use of force.

2. Maofisa wote walio na mamlaka ya kubeba silaha lazima
ufahamu juu ya mwongozo ufuatao kushughulika na mwon
matumizi ya nguvu yaani continuum of force. All officers
authorised to carry weapons shall become familiar
following guidelines dealing with the use of force continuum

Mwongongozo wa kutumia Nguvu - Tafsiri.

3. Mwongozo wa Matumizi ya nguvu maelezo ya kimchoro wa
yanatotoa taswira ya kutumika au kutotumika kwa
inayostahili na askari polisi kufuatia matendo yaliyofar
mtuhumiwa au mhalifu. Mwongozo huu unaonyesha ju
kisheria la ofisa wa polisi kutumia nguvu halali inyostahili
tishio lililotambuliwa na ofisa akiwa na sababu za msingi.

4. Kiwango cha Nguvu inayofaa kinachoweza kutumiwa na
polisi kumdhibiti mtu itategemea mazingira Fulani amba
ataona wakati huo nguvu itumike. Kigezo muhimu cha ku
wakati wa kuamua kiwango cha nguvu gani itumike kudhibi
machafuko ni pamoja na umri, ukubwa, uimara, uzoefu,
cha ujuzi nguvu uliyonayo idadi ya maofisa na watu
waliohusika katika tukio.

   (a). Matumizi ya muundo. Wakati wa kushughulikia watu
   na wahalifu, maofisa wajaribu kufuata muong
   matumizi ya nguvu, kuanzia kiwango cha chini ka
   nguvu. Uwepo tu wa polisi wenye sare za polisi
   kutosha kuzuia matendo ya watuhumiwa. Endapo vu
   kugoma kutii amri halali kutajitokeza, ofisa atachuku
   kulingana na hatua ya nguvu inyostahili kuzuia h
   Kimsingi ofisa atumie nguvu ndogo inayofaa kuleta
   na utulivu wa hali husika.

(i) Kama udhibiti kwa nguvu ya kiwango cl umepotea au kushindikana, ofisa lazima kiwango kikubwa cha nguvu muhimu k udhibiti. Ni mukhimum kutambua hali in kumfanya ofisa aanzie kiwango cha juu kal nguvu., au aruke viwango vingine kutokana na vya mtuhumiwa. Kwa kutumia vizuri mv kutumia nguvu, maofisa watafanya kazi zac kwa kutumia nguvu inayofaa kudhibiti machafuko.

(ii) Vipengele mbalimbali vya maeneo vimeainis kujadiliwa kwa undani hapa chini.

5. (a) Mwongozo wa kutumia nguvu umegawanyika katika sita.

(i) Kuainisha tishio.

(ii) Kiwango cha ugomaji utii halali wa sheria.

(iii) Mbinu za nguvu.

(iv) Mbinu za udhibiti.

(v) Kuzingatia matumizi ya nguvu namna iliv isizidi kiwango stahili.

(vi) Sababu za msingi za kisheria, uhalali. Justifica

(b) Maeneo yaliyoelezwa hapo juu yanaelezwa kwa und chini. The above listed component parts are expl greater detail below.

6. (a) *Kuanisha tishio* t: Neno tishio. Linatumika kuel anayeweza kuleta madhara/majeraha makubwa na h Tishio lazima liwe na vigezo vifuatavyo kuhalalisha r ya nguvu. kimwili.

(i) Nia ovu. Intent;

(ii) Mbinu za uhalifu. Means; and

(iii) Nafasi ya kutenda kosa. Opportunity.

(b) Mtu asiyetishio anaweza kutii au kushindwa kuamu kutokutii.

7. *Kiwango cha kutotii, ugomaji:*

(a) *Kubakia jinsi alivyo. (Static).* Mfano kukataa kuu anazopewa na kubakia na silaha lakini kaishik mtindo ambao siyo tishio.

(b) *Mwenye pilikapilika (Active)*. Mfano mtu anakataa ofisa ya maneno na anjaribu kutumia nguvu kumsum anajaribu kukimbia, anaonyesha kushikilia sawasa nguvu vitu alivyobeba, au kushika silaha kwa unaotishia anapoamriwa kuiangusha.

(c) *Ominous (Ominou)s.* Mfanomtishiaji anapojariu ku yupo tayari kupambana kupitia maneno, vitisho, au vurugu.

d. *Hatari (Letha)l.* Mfano mtishaji anapokuwa na vitendakazi vya kusababisha madhara makubwa Vitenda kazi vyaweza kuwa silaha au mikono mitupu tishio kutumia silaha za kuua Bunduki ya mkono shank) au silaha hatari (kipande cha bomba la chum iliyovunjika, kuleta madhara ya kimwili au kmtishiaji vitish o kwa kuonyesha ukubwa wa silshs yake alizonazo au mbinu za kupambana.

8. *Viwango nguvu;* maneno na aya zifuatazo zinzelezea muhimu yanayoendana na mwongozo wa kutumia ngu following words and phrases describe important points a Force Continuum:

(a) *Uwepo (Presence)*. Kufika kwa maofisa wa polisi eneo la tukio. Katika mazingira yaliyo mengi, kuw askari polisi. Kunatosha kuzuia matendo ya uhalifu.

(b) *Amri za kuongea maneno (Verbal Command)s*. maswali watuhumiwa kujaribu kuwashawishi, au amri ya moja kwa moja.sauti na mwenendo wa ofisa wa maelekezo , na kuchagua maneno ni vigezo vina kutekelezeka kwa amri ya kuongea maneno.

(c) *Kugusa mwili (Physical contact).* Kuelekeza mtuhum kumgusa au kudhibiti na escort hold. Kama kutumia imeshindikana au haielekei kuzaa matunda ya udhib a atamua kumgshika ili kuleta udhibiti. . Ushi utakuwa wa kiungwana lakini imara kushika n mtuhumiwa ili kusafirisha au kumdhibiti. Endapo mt

atatii Kiwango cha nguvu kitapunguzwa kulingana n
anavyotiikutii, na kudhibitiwa katika kiwango muh
udhibiti.

(d) *Udhibiti kimwili (Physical control).* Ni pamoja na ku
maneo dhaifu ya mwili, kutengua maugo. Kama
mwili hakuzai matunda, ofisa aweza kutumia minu ya
kimwili ili kuleta udhibiti. .

(e) *Udhibiti kimwili hatari (Serious Physical control).* Ni
na kupiga mapigo ya wazi na kutumia silaha kama
Kirungu ni silaha ya kujilinda imetengenezwa kwa
kupiga. Matumizi ya virungu inikuzuia nguvu ya ku
anayekataa kukamatwa. Maofisa wote watakiwa
virungu vilivyotolewa kiofisi. Baada ya kufaulu vizuri
ya kutumia virungu. Nyaraka za kumaliza mafunzo y
zihifadhiwe kwenye faili la ofisa.

(f) *Nguvu ya mauaji (Deadly Force).* Ni pamoja na nguv
inayoweza kuua au kudhuru mwili vibaya kutol
mazingira itakavyotumika.

9. *Kanuni za kutumia nguvu (Method of Force):* kwa kuongeze
katika mawasiliano ya mdomo. Askari wawe na ufanis
mambo yafuatayo ya kanuni za kutumia nguvu.

(a) Kudhibiti kwa kuamuru au kulazimisha kuweka chi
alizobeba mtishiaji. (Control Holds/Takedowns).

(b) Kuwekavikwazo/vizuizi (Restraints). Kufunga mnyo
Pingu,kufunga kamba za mnyongonyo mikononi na
Matumizi sahihi ya pingu za kusimama, au kupiga m
pingu za hatari akiwa amelazwa na kushikizwa
sehemu mfano kitanda, au chuma kisichohamishika.
handcuffs, flex ties, leg straps/cords. Proper
cooperative handcuffing (standing) and uncoo
handcuffing (kneeling/prone) and high risk har
(felony prone).

(c) *Upekuzi. (Searching).* Simama na frisk, cursory anga
kuna silaha, pingu, pingu za kusimama, kupiga mag
kulala.Stop and Frisk, cursory check for weapons, ha
standing, kneeling and prone.

(d) *Virungu. Virungu vilivyonyooka na imara, au vifaa vir kudhibiti umati vilivyokubalika na kupitishwa. r sahihi ya mwanga mkali kwa ajili ya kinga.*

(e) *kupangua, usimamaji na upigaji. Closedfist/ope strikes,pigo la mbele, (Blocks, Stances and Strikes,* fist/open hand blocks, interview stance, combat closed fist strikes, open hand strikes, front kick, an rear kick, leg sweeps, knee and elbow strikes.

(f) *Ulinzi binafsi (Personal Defence).* Ulinzi dhidi ya ulivyobeba, vifaa vya muasho, kabari, kunjwa mi sjilaha za mikononi, ufundi wa kunyanganya silaha. M sahihi ya pingu na silaha za kujihami, mbinu za kutu na silaha za ncha kali.

(g) *Unyang'anyaji silaha toka kwa mtuhumiwa. (Disarı* Mbinu za kumnyang'anya silaha mtuhumiwa na silaha ya mkononi.

(h) *Utunzaji na usafirishaji (Custody and Transp* Kuhamisha vifaa vinavyotishia kutoka kwenye mtuhumiwa na kuviweka kwenye gari la doria, na combatant kutoka kwenya gari la doria.

10. *Kuzingatia upimaji wa nguvu gani itumike au (Considerations of Force Escalation/De-escalation):* Mazi sababu alizonazo ofisa wa polisi wa kati nguvu inatumika athiri kiwango sahihi vya nguvu ambayo ofisa ataitumia k na tishio. Miongoni mwa mambo yanayoweza kuathiri viwango vya nguvu stahili kwa mazingira yaliyopo ı yafuatayo:

(a) Kama mtishiaji alipata nafasi ya kutii na kutekele Kama amri zilitolewa sawasawa na zinatekeleka?.

(b) Je vitendo vya sasa vyaweza kufikia udhibiti?

(c) Je, tishio laweza kuleta madhara kwako au kwake mt

11. Kanuni za msingi za kuhalalisha/kuelezea matumizi ya nguv

(a) Kama kiwango cha nguvu ni halali/kin maelezo, ut au mfumo uliotumika hauna umuhimu.

(b) Kama kiwango cha nguvu kina uhalali/maelezo, kiwa majeraha anachoweza kupata mtishaji hakina umuhi

(c) Mara zote tishio ndiyo linatoa/linalazimisha kiwa nguvu itakayotumika. Kwa hiyo, mtishiaji anawajib jeraha/madhara yeyote ambayo matishiaji atayapat anakataa kutii amri.

(d) Ni wajibu wa ofisa aliyopo kuzuia na kupamb watishiaji wanaokataa amri halali haraka iwezeka kurejesha hali ya usalama.

PGO - 275

SILAHA

UTUNZAJI WA SILAHA ZA KIRAIA KATIKA VITUO VYA POLISI

1. Chini ya kifungu cha 15(1) cha shelia ya silaha na risasi za moto, mtu yeyote ambaye hataki kuwa na kibali cha silaha yake au ambaye amekaidi kupata kibali au kibali cha kumiliki silaha kimeisha, anaweza akaweka silaha yake kwa mtu yeyote aliyekathiminiwa au katika ghala la serikali au la kiraia hadi ambapo atakuwa tayari kuiuza au kusafirisha silaha hiyo, silaha hiyo itahifadhiwa kwa mujibu wa maelekezo ya mkuu wa jeshi la Polisi.

2. Vigezo ambavyo vinakubaliwa kwa silaha zote ambazo hazina kibali na zinaweza kukubaliwa kutunzwa Polisi ni kama ifuatavyo.

    a) Silaha zitakubaliwa tu kwa kituo cha daraja “A” na “B” kama tu kuna sehemu ya kutosha kuhifadhia silaha hizo.

    b) Utunzaji hautazidi miezi sita, kwa lolote litakalotokea hasara itakuwa kwa mwenye silaha na hakuna gharama yoyote ambayo itatozwa.

3. Kama kutakuwa hakuna nafasi ya kutosha katika vituo vya Polisi, mtu ambaye mwenye shida ya kuhifadhi silaha anatakiwa ashauriwe kuwa silaha ambazo hazina kibali kwa faida yao kuandaa sehemu au ghala la kiraia kwa utunzaji wa silaha hizo, kama hawataki kufanya hivyo silaha hizo zinaweza kupokelewa kituo cha daraja “A” na “B” ambapo tu

    a) Kuna sehemu ya kutosha ya kuhifadhia

    b) Wamekubaliana na vigezo vilivyowekwa kwenye jedwari A namba 2 na viambatanishi vinavyoonyesha muda wa juu kabisa unaohitajika kuhifadhi silaha hiyo.

4. Mtu yeyote ambaye ameruhusiwa kuhifadhi silaha na risasi za moto na Polisi lazima akamilishe na asaini nakala tatu za risiti ya kuhifadhia silaha (Fomu ya Polisi namba 14) ambayo inavitu vifuatavyo;

    a) Aina ya silaha

    b) Kibali

    c) Imetengenezwa wapi

    d) Namaba ya aliyetengeneza

    e) C.A.R namba

5. Afisa wa Polisi anyepokea silaha ataakikisha fomu zote zipo na atajza katika (Fomu ya Polisi namba 14) na kasha atasaini risiti katika nafasi zilizowazi, risiti halisi itaondolewa kwenye kitabu cha risiti na kupewa mtu aliyehifadhi silaha hiyo. Risiti ya pili itapelekwa kwa msjili mkuu wa silaha na risiti ya tatu itabaki katika kitabu cha risiti.

6. a) Mtu yeyote aliyehifadhi silaha anapaswa kuonyesha nakala ya risiti aliyohifadhia ili aweze kupewa silaha yake kutoka kituo cha Polisi na risiti halisi itabaki kwa aliyehifadhi, nakala itapelekwa kwa msajili mkuu wa silaha na nakala ya tatu itabaki kwenye kitabu cha risiti.

    b)umakini lazima uwepo katika ulinganifu wa risiti iliyoondelewa na risiti ya kuifadhia

7. Mkuu wa Polisi mkoa na mkuu wa Polisi wa wilaya wanatakiwa kuwa makini na kujua silaha zote ambazo zimehifadhiwa Polisi lakini hazina kibali na kuchukua hatua stahiki wakisaidiana na msajili mkuu wa silaha kuakikisha kuwa wamiliki wanachukuwa silaha zao baada ya miezi sita kupita.

Utunzaji Silaha katika vituo vya Polisi

8. Chini ya kifungu 3(1) cha sharia ya silaha na risasi za moto (utunzaji salama) iliyotangazwa kama G.N ya 1954

    1) Kisheria ni sahihi kuhifadhi silaha kitu cha Polisi baada ya kupokelewa na kiongozi wa Polisi katika kituo hich kama ilivyoelekezwa ktika jedwari hapo chini, silaha zote zenye kibali na risasi zake kwa vigezo hivyo kama ilivyoelekezwa na afisa wa Polisi inabidi iwe hivyo.

    2) Kisheria ni sahihi afisa wa Polisi au afisa wa Polsi yeyote katika uangalizi wake u kumiliki silaha kwa muda wowote ambao ilihifadhiwa nay eye kwa kufuata taratibu isipokuwa tu silaha hiyo au risasi hizo ziliachwa kwake kwa muda mrefu katika muda uliopaswa kuhifadhi silaha hiyo.

JEDWALI

Taratibu 3(1)Kituo cha Polisi Arusha, Dar – es – Salaam (kati), Dodoma, Iringa, Lindi, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Tabora na Tanga.

9. Taratibu zilizowekwa katika mtiririko 1-7 itakuwa sawa kwa watu wote wanaohitaji kuhifadhi silaha zao katika vituo vya Polisi vilivyotajwa hapo juu.

10. Silaha zote lazima ziwe na kibali zinazotolewa vinginevyo zinatakiwa kuhifadhiwa kwenye ghala la serikali au kiraia.

PGO - 277

UWEPO WA WARAKIBU WA POLISI NA WAKAGUZI WA POLISI

1. Warakibu wa polisi hawataondoka mikoani mwao, wilayani au vituoni mwao bila ya kupewa ruhusa isipokuwa kama itatokea dharura tu.

2. Kwa kawaida wahusika wataomba ruhusa na ruhusa hizo zitatolewa kama ifuatavyo:-

   (a) Maombi ya wakuu wa komandi, maombi yao yatatolewa ruhusa na mkuu wa jeshi la polisi Tanzania au kamishina wa polisi utawala na fedha au kamishina wa polisi Zanzibar.

   (b) Makamanda wa polisi wilaya, makamanda wa kikosi cha kutuliza ghasia wa mikoa, kamanda wa upelelezi mkoa na wakuu wa mawasiliano mkoa ruhusa zao zitatolewa na makamanda wa polisi mikoa .

   (c) Wakuu wa vituo maombi yao ya ruhusa yatatolewa na makamanda wa polisi wilaya.

   (d) Askari wanaofanya kazi makao makuu ya polisi, ruhusa zao zitatolewa na kamishina msaidizi mwandamizi wa polisi makao makuu.

   (e) Warakibu wa polisi na wakaguzi wa polisi ambao hawakujumuishwa katika aya 2(a) na (b) PGO 277 maombi yao ya ruhusa yatatolewa na wakuu wa komandi.

3. Makamanda wa polisi wa mikoa hawataondoka makao makuu yao ya mikoa zaidi ya masaa 24 bila kutoa taarifa makao makuu ya polisi tarehe na sababu za kina za kuondoka kwao.

4. Makamand a wa polisi wilaya vilevile watoe taarifa kwa makamanda wa polisi mikoa na wakuu wa wilaya kuhusu kuondoka kwao katika makao makuu yao ya wilaya kwa kipindi kisichozidi masaa 24.

5. Warakibu wote wa polisi, wakaguzi na wakuu wa vituo ni lazima wapatikane wakihitajika muda wowote.

6. Vitabu cha uwepo wa maofisa vitatunzwa katika vituo vyote, makamanda wa polisi wa wilaya watahakikisha vitabu hivi vinatunzwa vizuri na amri ya utendaji itatoa utaratibu wa matumizi yake.

7. Warakibu wote wa polisi na wakaguzi wa polisi watahusika na kutoa taarifa zao sahihi za mahali watakapokuwepo na nambari zao za simu baada ya muda wa kazi na kurekodiwa katika kitabu cha uwepo wa maofisa hata kama hawapokazini au kambini.

8. Askari wa makao makuu, maofisa na wakaguzi wanaofanya kazi Dar-es-Salaam watatoa taarifa watakapokuwepo kama ilivyoelezwa kwenye aya ya 7 hapo juu ya afisa mwenye dhamana ya kazi ya siku husika. Polisi makao makuu watafanya kama amri ya utendaji ilivyotolewa maelekezo na polisi makao makuu.

PGO 278

UPATIKANAJI WA MAOFISA

MAOFISA WA ZAMU

1.Watu katika jamii wanaoishi katiaka miji mikubwa na katika maeneo ya kuishi wanayo haki ya kuwasiliana na maofisa wa polisi. Ofisa wa polisi anatakiwa kupatikana muda wote ili kushughulikia mambo mhimu na matukio ya ghafla.

2. makamanda wa polisi wa mikoa watapanga katika amri ya utendaji kuwa ofisa wa zamu atakuwa anapatikana kwa miito yote ya haraka katika kila kituo cha daraja A. Maofisa wa idara ya upelelezi mkoa na idara ya intelijensia mkoa watachukua nafasi ya maofisa wa zamu kama hakutakuwepo na maingiliano katika kazi zao za kawaida.

3. Maofisa wa zamu lazima wapatikane kwa simu zilizoko ofisini au nyumbani wakati wote wakiwa zamu (kwa kawaida masaa 24). Wanaweza kuwa nje kwa muda kidogo kwa huduma binafsi wakati

wakiwa zamu ambako wanaweza kupatikana kwa urahisi kwa simu lakini hawatakiwi kwenda disco, senema, baa nk.wanawajibika wenyewe kuhakikisha kwamba wama ,awasil;iano ya haraka na kituo cha Polisi ambacho wanahusika kuwa zamu.

4. Kama utaratibu wa kawaida ofisa wa zamu ataitwa tu pale ambapo ofisa mwenye wajibu na jambo hili la wakati huo hapatikani lakini makamanda wa mikoa watapanga mipango hiyo watakavyona. Wanaweza wakatumia maelekezo yao kama watakavyokubaliana na aya ya 2 ikitegemea kwamba wamehakikisha kuwa ofisa wa zamu atapatikana wakati wote atakapohitajika.

5. Kibao cha majina ya maofisa lazima kiwekwe katika chumba cha mashtaka kikionesha cheo, jina, namba ya simu ya ofisa ya ofisini na myumbani kama ilivyooneshwa hapa chini.

KITUO CHA DARAJA “A”

Kamanda wa Polisi wa mkoa

Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa

Mkuu wa Polisi wa Wilaya

Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya

Mkuu wa Kituo

Afisa wa zamu

Mkaguzi wa zamu

KITUO CHA POLISI DARAJA ‘B’

Kamanda wa Polisi wa Mkoa

Mkuu wa Polisi wa Wilaya

Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya

Mkuu wa Kituo

KITUO CHA POLISI CHA DARAJA ‘C’

Kamanda wa Polisi wa Mkoa

Mkuu wa Polisi wa Wilaya

Mkuu wa Kituo

Askari wa chumba cha mashtaka wataelekezwa namna ya kuwasilikiliza kwa makini watu kuhusu matumizi ya ubao huo kama wenyewe hawajaelewa kutokokana na ugumu wa lugha.

AFISA WA ZAMU WA MAKAO MAKUU YA DAR ES SALAAM

1. Kwa nyongeza ya mpangilio kama ilivyooneshwa katika aya ya kwanza hadi ya tano Afisa wa zamu Makao makuu atateuliwa na afisa rasilimali watu kushika zamu siku za sikukuu kwa kipindi cha masaa 24 na siku za mwisho wa wiki. Afisa yeyote mwenye cheo chini ya Msaidizi Kamishna wa Polisi anayefanya kazi Dar es salaam isipokuwa wale wenye kazi maalum na maofisa wnaofanya kazi chini ya komandi ya kamanda wa polisi mkoa wa Dar es salaam wataingia zamuk ama watakavyopangwa na afisa rasilimali watu wa makao makuu.

2. Afisa wa makao makuu atakayekuwa zamu atawajibika kuhakikisha kwamba jhatua sahihi zinachukuliwa kwa jambo/tukio lolote litakalotokea na pia watapatikana kwa wito wowote wa kituo cha polisi dare s salaam kama yulemafisa wa kawaidam(atakayeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 2) kama atakuwa hapatikani,

3. Hakuna afisa yoyote atakayeacha kuingia zamu yake isipokuwa udhuru utakaomridhisha afisa rasilimali watu makao makuu labda iwe ni sababu ambayo haitoweza kuepukika.

AFISA MPELELEZI MAKAO MAKUU

4. Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai anawajibika kuhakikisha kwamba afisa wa zamu atakuwepo kuhakikisha kwamba matukio ya idara ya upelelezi na idara ya intelijensia yanafanyiwa kazi kwa masaa yasiyo ya kazi.

